MABADILIKO YA VIONJO VYA KIUANDISHI KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI: ULINGANISHO WA RIWAYA ZA SHAABAN ROBERT NA SAID A. MOHAMED

Na

Arafa Jumanne

Tasnifu Iliyowasilishwa kwa ajili ya kukamilisha mahitaji ya Shahada ya Uzamili ya Sayansi ya Jamii katika Fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dodoma Chuo Kikuu cha Dodoma

Oktoba, 2016

ITHIBATI

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma tasnifu hii inayoitwa ***'Mabadiliko ya Vionjo vya Kiuandishi katika Riwaya ya Kiswahili: Ulinganisho wa Riwaya za Shaaban Robert na Said A. Mohamed'*** ikubaliwe kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dodoma.

……

Dkt. A.S. Ponera

(Msimamizi)

Tarehe ……

IKIRARI

NA

HAKIMILIKI

Mimi, **Arafa Jumanne** ninathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu halisi. Haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa minajili ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili au Shahada nyingine yoyote.

Saini ya Mtafiti……

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri wala kusambaza sehemu yoyote ya tasnifu hii bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Dodoma.

SHUKRANI

Ni wazi kuwa wapo wengi waliotoa mchango wao wa hali na mali katika mchakato wa kukamilisha tasnifu hii. Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na afya mpaka leo hii.

Pili, natoa shukrani zangu za dhati kwa msimamizi wangu, Dkt. Athumani Salum Ponera, ambaye alijitolea kwa moyo wake wote kunisimamia, kunielekeza na kuniongoza kwa kunipa mawazo mbalimbali yaliyochangia katika kumaliza tasnifu hii. Hakusita kunitia moyo pale nilipokata tamaa.

Tatu, nawashukuru wahadhiri wangu waliokuwa kama dira kwangu katika kipindi chote cha masomo ya shahada hii ya pili. Miongoni mwao ni Dkt. Muhammed Seif Khatib, Dkt. Zuhura Badru, Dkt. Rafiki Yohana Sebonde, na Dkt. Athumani Salum Ponera wote kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma.

Nne, napenda kuwashukuru wanafunzi wenzangu wa Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dodoma, hususa Grace Mbwambo, Martina Duwe, Rasuli Msangi, Bimkubwa Ali na Makame Pandu.

Tano, natoa shukrani kwa uongozi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kwa kunidahili na kuniwezesha kufanya utafiti.

Sita, napenda kuishukuru familia yangu kwa msaada na uvumilivu mkubwa waliouonesha katika kipindi chote cha masomo yangu hadi kukamilisha tasnifu hii.

TABARUKU

Tasnifu hii naitabaruku kwa Marehemu baba yangu mzazi, Almas Jumanne Chaponga, wewe ni baba bora pumzika kwa amani, pamoja na mama yangu mzazi, Fatuma Saleh Mchome, kwa kunilea na kunisomesha vyema.

IKISIRI

Tasnifu hii inahusu Mabadiliko ya Vionjo vya Kiuandishi katika Riwaya ya Kiswahili. Utafiti ulijigeza katika kulinganisha na kulinganua mabadiliko hayo katika riwaya za Shaaban Robert na Said A. Mohamed. Neno vionjo katika tasnifu hii limetumika kama hali ya kimajaribio au mwondoko wa utanzu fulani wa Fasihi kutoka sura iliyozoeleka kwenda sura mpya ambayo haijazoeleka. Mtafiti ameamua kuchunguza mabadiliko ya vionjo vya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili kwa sababu, kwa kiasi kikubwa bado dhana hii ya mabadiliko ya vionjo vya kiuandishi haijafanyiwa uchunguzi.

Utafiti ulifanyika maktabani na uwandani. Maktabani tuliyadurusu mapitio mbalimbali kama vile majarida, tasnifu, tahakiki, makala na vitabu. Uwandani tulitumia mbinu ya mahojiano ili kupata data za utafiti wetu. Utafiti ulitumia nadharia ya uhalisia ambayo humtaka mtunzi kutunga kwa kuzingatia suala la wakati pamoja na kujua historia ya jamii husika. Mabadiliko haya katika riwaya ya Kiswahili yanazingatia pia vitu hivyo.

Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa uandishi wa riwaya ya Kiswahili umebeba mabadiliko kadhaa katika uandishi wake. Mabadiliko haya katika vionjo vya kiuandishi yanachangiwa sana na vitu kama vile mabadiliko ya kijamii (historia za jamii), umajaribio, ongezeko la wasomi na hata maendeleo ya sayansi na tekinolojia kwa kiasi kikubwa. Mchango mpya wa tasnifu hii ni kuonesha vionjo vinavyotumiwa na waandishi mbalimbali katika utunzi hasa katika riwaya ya Kiswahili.

YALIYOMO

ITHIBATI i
IKIRARI NA HAKIMILIKI ii
SHUKRANI iii
TABARUKU iv
IKISIRI v
YALIYOMO vi
VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA xi

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI 1
1.1 Utangulizi 1
1.2 Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu Zilizotumika katika Utafiti Huu 1
1.2.1 Zama za Uandishi 1
1.2.2 Riwaya 1
1.2.3 Riwaya ya Zamani 2
1.2.4 Riwaya Mpya 2
1.3 Usuli wa Tatizo la Utafiti 3
1.4 Tamko la Tatizo la Utafiti 6
1.5 Malengo ya Utafiti 7
1.5.1 Lengo la Jumla 7
1.5.2 Malengo Mahususi 7
1.6 Maswali ya Utafiti 7
1.7 Manufaa ya Utafiti 8
1.8 Historia za Waandishi Teule 8
1.8.1 Historia ya Shaaban Robert 8
1.8.2 Historia ya Said A. Mohamed 13
1.9 Mipaka ya Utafiti 17
1.10 Muhtasari wa Sura ya Kwanza 17

SURA YA PILI :KIUNZI CHA NADHARIA NA MAPITIO YA MAANDIKO 18
2.1 Utangulizi 18
2.2 Kiunzi cha Nadharia ya Utafiti 18
2.2.1 Misingi ya Nadharia ya Uhalisia 18

2.2.2 Jinsi Nadharia ya Uhalisia Ilivyotumika 21
2.3 Mapitio ya Maandiko 21
2.3.1 Maandiko Yanayohusu Utunzi wa Kazi za Fasihi kwa Ujumla 21
2.3.2 Maandiko Yanayohusu Maendeleo ya Riwaya kwa Ujumla 25
2.3.3 Maandiko Yanayohusu Waandishi Teule 32
2.3.3.1 Maandiko Kuhusu Shaaban Robert 32
2.3.3.2 Maandiko Kuhusu Said A. Mohamed 40
2.4 Mapengo Yaliyopaswa Kuzibwa 44
2.5 Muhtasari wa Sura ya Pili 44

SURA YA TATU: METHODOLOJIA YA UTAFITI 45
3.1 Utangulizi 45
3.2 Mpango wa Utafiti 45
3.3 Eneo la Utafiti 45
3.4 Walengwa wa Utafiti 45
3.4.1 Wango Tafitiwa 46
3.4.2 Sampuli ya Watafitiwa na Upatikanaji Wake 46
3.5 Ukusanyaji wa Data 47
3.5.1 Njia na Zana za Kukusanyia Data 47
3.5.2 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data 47
3.6 Uchanganuzi wa Data 48
3.7 Itikeli za Utafiti 48
3.8 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti 49
3.9 Vikwazo vya Utafiti 49
3.10 Muhtasari wa Sura ya Tatu 50

SURA YA NNE :UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI 51
4.1 Utangulizi 51
4.2 Mikondo ya Kiuandishi katika Riwaya ya Kiswahili 51
4.2.1 Riwaya ya Kiswahili na Matapo ya Sanaa 51
4.2.1.1 Tapo la Urasimi Mkongwe 51
4.2.1.2 Tapo la Urasimi Mpya 55
4.2.1.3 Tapo la Ulimbwende 58
4.2.1.4 Tapo la Uhalisia 59

4.2.2 Mikondo ya Uandishi ya Riwaya ya Kiswahili 61
4.2.2.1 Uandishi wa Kiteokrasia/Kiaristostle..... 61
4.2.2.2 Uandishi wa Kidemokrasia 65
4.2.2.3 Uandishi wa Kimsaragambwe 66
4.3 Vionjo vya Kiuandishi katika Riwaya za Shaaban Robert na Said A. Mohamed 67
4.3.1 a) Muhtasari wa Riwaya za Shaaban Robert 67
4.3.1.1 Muhtasari wa Riwaya ya *Adili na Nduguze* 67
4.3.1.2 Muhtasari wa Riwaya ya *Utu Bora Mkulima*..... 69
4.3.1 b) Muhtasari wa Riwaya za Said A. Mohamed 70
4.3.1.1 Muhtasari wa Riwaya ya *Babu Alipofufuka*..... 70
4.3.1.2 Muhtasari wa Riwaya ya *Utengano* 72
4.3.2 Vionjo vya Kiuandishi katika Riwaya ya Kiswahili..... 73
4.3.2 a) Vionjo vya Kiuandishi katika Riwaya za Awali..... 73
4.3.2.1 Usimulizi wa Kimaonyo na Maadili 74
4.3.2.2 Matumizi ya Wahusika Bapa 74
4.3.2.3 Matumizi Makubwa ya Nduni za Fasihi Simulizi 74
4.3.2.4 Mianzo na Miisho ya Kifomyula 75
4.3.2 b) Vionjo vya Kiuandishi katika Riwaya za Sasa..... 76
4.3.2.1 Matumizi ya Wahusika wa Ajabu..... 76
4.3.2.2 Matumizi ya Mazingaombwe..... 76
4.3.2.3 Dhana ya Mapenzi na Ngono..... 77
4.3.2.4 Matumizi ya Nyenzo za Kisayansi na Teknolojia 77
4.3.2.5 Kuyajadili Maisha kwa Kina..... 77
4.3.2.6 Matumizi ya Ndoto 78
4.3.2.7 Dhima na Nguvu ya Asasi za Dini..... 78
4.3.3 Vionjo vya Uandishi katika Riwaya Teule 79
4.3.3.1 Vionjo vya Kiuandishi katika Riwaya ya *Adili na Nduguze*..... 79
4.3.3.1.1 Usimulizi wa Kimaonyo na Maadili 79
4.3.3.1.2 Matumizi ya Nduni ya Fasihi Simulizi 80
4.3.3.1.3 Matumizi ya Wahusika Bapa 81
4.3.3.2 Vionjo vya Kiuandishi katika Riwaya ya *Utubora Mkulima*..... 82
4.3.3.2.1 Usimulizi wa Kimaadili na Maonyo 82
4.3.3.2.2 Matumizi ya Wahusika Bapa 83
4.3.3.2.3 Matumizi ya Nduni za Fasihi Simulizi 83

4.3.3.3 Vionjo vya Kiuandishi katika Riwaya ya *Babu Alipofufuka* 84
4.3.3.3.1 Umazingaobwe..... 84
4.3.3.3.2 Matumizi ya Wahusika wa Ajabu 86
4.3.3.3.3 Dhana na Dhima ya Mapenzi Na Ngono 86
4.3.3.3.4 Matumizi ya Nyenzo za Kisasa na Teknolojia..... 87
4.3.3.3.5 Kuyajadili Maisha kwa Kina..... 87
4.3.3.3.6 Matumizi ya Ndoto 88
4.3.3.4 Vionjo vya Kiuandishi katika Riwaya ya *Utengano*..... 89
4.3.3.4.1 Kuyajadili Maisha kwa Kina..... 89
4.3.3.4.2 Dhana na Dhima ya Mapenzi na Ngono 90
4.3.3.4.3 Matumizi ya Ndoto 91
4.3.4 Kulandana kwa Vionjo vya Uandishi katika Riwaya za Shaaban Robert na Said A. Mohamed 91
4.3.4.1 Kulandana Kwao katika Vionjo vya Kimaudhui 92
4.3.4.2 Kulandana Kwao katika Vionjo vya Kifani 95
4.3.5 Kutofautiana kwa Vionjo vya Kiuandishi kati ya Shaaban Robert na Said A. Mohamed 97
4.3.5.1 Kutofautiana Kwao katika Vionjo vya Kimaudhui..... 97
4.3.5.2 Kutofautiana Kwao katika Vionjo vya Kifani 99
4.4 Sababu za Mabadiliko ya Kiuandishi katika Riwaya ya Kiswahili 102
4.4.1 Mabadiliko ya Kijami au Historia ya Jamii 102
4.4.2 Ongezeko la Wasomi 104
4.4.3 Umajaribio 105
4.4.4 Maendeleo ya Sayansi na Teknoloji 107
4.4.5 Kuibuka kwa Majanga na Magonjwa 108
4.5 Muhtasari wa Sura ya Nne 109

SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 110
5.1 Utangulizi..... 110
5.2 Muhtasari wa Utafiti 110
5.3 Hitimisho..... 112
5.3.1 Utoshelevu wa Nadharia Iliyotumika katika Utafiti 112
5.3.2 Mchango wa Mpya wa Tasnifu Hii..... 112
5.4 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo 113

MAREJELEO 115
VIAMBATISHO 119

VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

BAKIZA	:	Baraza la Kiswahili la Zanzibar
BBC	:	*British Broadcasting Cooperation*
BK	:	Baada ya Kristo
BYM	:	Baada ya Masihi
Bw.	:	Bwana
Dkt.	:	Daktari
DW	:	*Deutshe Welle*
KK	:	Kabla Kristo
KYM	:	Kabla ya Masihi
Ltd	:	*Limited*
MA	:	*Master of Art*
Mh.	:	Mheshimiwa
Mr.	:	*Mister*
Ph D	:	*Doctor of Philosophy*
Prof.	:	Profesa
SAW	:	*Swalla-llahu Alayhi Wasallam*
SMZ	:	Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
SUZA	:	*State University of Zanzibar*
SW	:	*Subuhana Wata'ala*
TAKILUKI	:	Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni
TTC	:	*Teacher Training College*
TUKI	:	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
UDOM	:	*University of Dodoma*
UDSM	:	*University of Dar es Salaam*
Uk.	:	Ukurasa
ZBC	:	*Zanzibar Broad-casting Cooperation*
ZU	:	*Zanzibar University*

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Utangulizi

Tasnifu hii inahusu Mabadiliko ya Vionjo vya Kiuandishi katika Riwaya ya Kiswahili Ulinganisho wa Shaaban Robert na Said A. Mohamed. Sehemu hii ya kwanza inatoa ufafanuzi wa istilahi mbalimbali muhimu zilizotumika katika utafiti huu. Pia, inatoa ufafanuzi kuhusu usuli wa tatizo la utafiti, tamko la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti huu, mipaka ya utafiti na mwisho ni hitimisho kwa sura ya kwanza.

1.2 Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu Zilizotumika katika Utafiti Huu

1.2.1 Zama za Uandishi

Zama za uandishi ni hatua au vipindi mbalimbali ambavyo Fasihi ya Kiswahili imepitia katika uandishi au utunzi wake. Kila kipindi cha uandishi kilikuwa na sifa zake ambazo ndizo zilitamalaki katika zama husika.

1.2.2 Riwaya

Senkoro (1987) anaeleza maana ya riwaya kwa kuzingatia sifa za riwaya kama ifuatavyo:

> Riwaya ni kisa ambacho urefu wake unakiruhusu kitambe na kutambaa mahali pengi na kuambaa vizingiti vingi vya maisha kama apendavyo mwandishi wake. Riwaya, basi ni hadithi ndefu ya kubuni, yenye visa vingi, wahusika zaidi ya mmoja, na yenye mazungumzo na maelezo anayozingatia kwa undani na upana, maisha ya jamii. Riwaya inatoa picha yote ya ujumla wa maisha ya mtu - toka nyumbani hadi katika kiwango cha taifa, na hata dunia nzima (uk. 73-74).

Fasili hii inatubainishia ya kuwa riwaya ni kisa ambacho kwa kawaida huzunguka maisha ya kila siku ya binadamu. Fasili hii inakanganya kidogo kwani mwandishi anaposema ya kuwa riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni ambayo huwa na maneno kati ya 75,0000, wakati zipo riwaya ambazo sio ndefu na bado zikaitwa riwaya kama vile *Nagon*a na

Mzingile. Kwa maana hiyo, kwa mujibu wa utafiti huu, istilahi hii ya riwaya inatarajiwa kutumika kama utungo ulioandikwa kwa lugha ya nathari, wenye masimulizi ya kubuni, mtiririko wa visa, mikasa na matukio, wahusika zaidi ya mmoja ambao wana tabia nyingi tofauti, migogoro mingi mikubwa na midogo. Riwaya husawiri ukweli wa maisha ya kikundi fulani cha jamii kwa madhumuni maalumu, ikihusisha mandhari mahususi na wakati maalumu.

1.2.3 Riwaya ya Zamani

Wamitila (2003:178) anasema kuwa riwaya ya zamani ni kazi ya kinathari au kibunilizi ambayo huwa na urefu wa kutosha, msuko uliojengeka vizuri, wahusika wengi walioendelezwa kwa kina, yenye kuchukua muda mwingi katika maandalizi na kuhusisha mandhari maalumu. Kwa maelezo hayo, riwaya ya zamani ni riwaya ambayo ilifungwa na kanuni katika usanaji wake. Ni riwaya ambayo ilifuata misingi na kanuni za Kiaristostle kama mhimili wa kutunga kazi ya Fasihi. Kwa minajili hiyo, istilahi hii itatumika katika utafiti huu kama riwaya isiyokuwa na upya (umajaribio) wowote katika utunzi wake. Ulifuata kanuni za kiutunzi ambazo zilisimikwa na wanafasihi kama akina Plato[1] na Aristostle[2] na katika utunzi huo wa riwaya, kila mtunzi alitakiwa kuzifuata.

1.2.4 Riwaya Mpya

Wamitila (2003:181) anasema kuwa, riwaya mpya hutumiwa kueleza riwaya ambayo inakiuka kaida za utungaji na muundo wa riwaya. Anasema kuwa riwaya za aina hii zina msuko, hadithi na wahusika wenye sifa zisizokuwa za kawaida. Kwa mfano, msuko

[1] Plato alikuwa ni mwanafalsafa maarufu sana huko Ugiriki na baadaye akawa maarufu dunia nzima. Inasemekana alizaliwa mwaka 427KK, mtaalam huyu alijikita katika taaluma mbalimbali kama vile falsafa na hesabu. Alikuwa mwanafunzi wa Socrates akisoma ushairi. Kwa kiasi kikubwa ametoa mchango mkubwa sana katika utunzi wa kazi za kifasihi (Finnbogason, 2007).

[2] Aristostle alikuwa ni mwanafalsafa aliyezaliwa katika eneo la Stagira Kaskazini mashariki mwa Aegen nchini Ugiriki. Alizaliwa 384KK na kufariki 322KK. Alikuwa mwanafunzi wa Plato na aliathiriwa vikubwa na Plato. Wakati wa uhai wake alikuwa mwalimu ambaye alifundisha misingi mbalimbali ya kiutunzi (Finnbogason, 2007).

huenda kuchanganya lugha ya msimulizi na mhusika, uakifishi huwa tofauti, wahusika hawana sifa zinazowabainisha waziwazi na hawana wasifu wa wahusika halisi.

Anaendelea kueleza kuwa, riwaya mpya pia huitwa riwaya ya kimajaribio ambayo ni dhana inayotumiwa kuirejelea riwaya iliyozuka Ufaransa katika miaka ya 1950 na kuakisi matumizi ya mbinu za kiubunifu za uandishi wa riwaya. Anafafanua kuwa, waandishi wa mkondo huu huwa na nia za kuziasi kaida za kijadi za uandishi wa riwaya, pamoja na kuyapinga baadhi ya mawazo waliyonayo wasomaji kuhusu fasili na hasa ya neno riwaya. Istilahi hii itatumika katika utafiti huu kufafanua riwaya ambayo ni ya kimajaribio hasa katika kuumba wahusika wake, vitushi vyake, mwendo wa kazi, maudhui na fani yake kwa kujiegemeza katika upya zaidi au katika umajaribio wa kuziasi kanuni zilizosimikwa katika kipindi cha urasimi. Mifano ya riwaya mpya za Kiswahili ni kama vile *Bina-Adamu* (2002) ya Wamitila, *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) za Kezilahabi, *Babu Alipofufuka* (2002) na *Dunia Yao* (2006) za Said A. Mohamed. Riwaya hizi zimetungwa kwa kutumia mbinu ya uhalisia mazingaombwe (ajabu) katika kuelezea matatizo mbalimbali yaliyopo katika jamii yetu.

Miongoni mwa sifa za riwaya mpya ni pamoja na matumizi ya uhalisia mazingaombwe, kutumika muundo wa kigeugeu au ambao umevunjikavunjika, mitindo ya masimulizi isiyo ya kawaida, dhana ya mhusika kuwa tofauti na ilivyo katika riwaya jadi na matumizi mengi ya ndoto katika utunzi wa kazi husika (Wanjiru, 2013).

1.3 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Fasihi au sanaa kwa jumla hukumbwa na kani mbalimbali za kimaisha kama ilivyo kwa kipengele chochote kilichopo hapa duniani. Kani hizo ni za kijamii, kiuchumi, kiteknolojia, kiutamaduni na kimtazamo. Kanuni za utanzu wowote wa Fasihi huambatana na kuamuliwa na maana ya utanzu huo. Tuongeapo kuhusu kanuni za uwanja fulani wa Fasihi hapohapo tunajaribu kuangalia yale mambo yajitokezayo mara kwa mara

katika uwanja huo. Pia, tunazingatia ukweli kuwa kanuni hizo hazibakii hivyohivyo kwani huweza kubadilika kufuatia mabadiliko katika utanzu unaohusika (Senkoro, 2011).

Kwa mujibu wa Khamis (2007) utanzu wa Fasihi hupata mtekenyo wa mabadiliko ili kuepuka kupooza na kushindwa kushawishi fikra na umbuji. Kanuni muhimu hapa ni kwamba; hatimaye, chenye mwanzo kina mwisho sharti kichoke na kipoteze nguvu na msisimko wake. Kwa mfano, mabadiliko ya ushairi wa Kiswahili ya kutotii sheria kali za arudhi na badala yake kunogea miundo huru, inasemekana angalau kwa baadhi ya washairi na wasomi, ni kutokana na kupooza kwa sulubu zake za ndani, mbali na sababu nyingine za nje. Pia, kwa upande mwingine tanzu za fasihi bila ya kuchoka au kupooza, huweza ukajikuta ghafla kutoweza kuhimili nguvu za matukio muhimu ya kihistoria, kitamaduni, kijamii, kisiasa, kielimu na hata kiuchumi; nguvu zinazolazimisha kubadilika kwake kifani na kimaudhui. Vivyo hivyo ndivyo, utanzu wa riwaya ulivyopokea mabadiliko kupitia sababu hizi.

Khamis anaongeza mfano mwingine kuwa, mabadiliko ya riwaya ya ramsia huko Ulaya kuelekea riwaya ya uhalisia ya akina Defoe, Richardson na Fielding inakubalika kwamba yalitokea kwa taathira zilizochangiwa na mapinduzi ya viwanda. Mabadiliko hayo yasichukuliwe kwa kubadilika kwa mifumo ya kiuchumi tu, bali mwenendo mzima wa maisha ya watu wa huko, mabadiliko hayo yahusishwe na mambo kama vile;

> Nyenzo za mauzo na manunuzi, usambazaji bidhaa, uhusiano wa mtu na mtu, kufa kwa fikra zilizoonekana kongwe pamoja na fikra za kuuangusha uungu zilizozushwa na wasomi kama Nietzsche; na hatimaye, kukua na kupata nguvu kwa ubinafsi na utashi wa vitu. Pia, Vita vya kwanza na vya pili vya dunia na matokeo yake ya kukatisha tamaa, yaliyopelekea kuzaliwa katika sanaa, usasa *(modernism)* na tena usasa baadaye *(postmodernism)* (uk. 17).

Fasihi ya Kiswahili, ikiwemo riwaya, pia haikuepuka kuelemewa na matukio makuu nje ya miundo ya tanzu zake. Kwa mfano, nchini Kenya waandishi wa Fasihi ya Kiswahili wanaoandika kwa misimamo wazi ya kisiasa hawapo wengi. Kinyume chake, nchini

Tanzania, tukitoa wale wanaoandika riwaya pendwa, ambazo kwa hakika nyingi zikichunguzwa zinazungumzia mambo fulani ya kijamii, wote wanajishughulisha moja kwa moja na matatizo ya jamii. Sababu zisababishazo tofauti hizi ziko wazi. Makali ya wembe ya siasa za Kenya dhidi ya siasa za kisoshalisti yalikuwa kila wakati yako tayari kumkata mwandishi aliyekataa kutetea mfumo wa kiuchumi wenye misingi ya kibepari. Kwa upande wa Tanzania waandishi kwa namna moja au nyingine, waliathiriwa na Azimio la Arusha na siasa za Ujamaa na Kujitegemea. Hapa pia, haikuwa rahisi kuandika dhidi ya sera rasmi.

Hali zote hizi ziliwekwa bila ya kutamka kanuni za kuandika kazi za sanaa ambazo ziliwahakikishia wasanii urahisi wa kufuata mkondo wa kanuni hizo bila ya kuingiliwa. Hii haina maana kwamba hakukuwa na waandishi waliozivunja kuta za makatazo na vizuizi. Khamis (2007) anatoa mifano ya kazi za kifasihi ambazo zilivunja mikatale ya kikanuni katika uandishi. Kwa upande mmoja kulikuwa na *Ngojera za Ukuta* za M. E. Mnyampala (1970), mkusanyo wa *Mashairi ya Azimio la Arusha* wa G. Kamenju ulivyoimba nyimbo za Azimio la Arusha. Kwa upande mwingine, tumeshuhudia *Mashetani* (1971) ya E. Hussein, *Gamba la Nyoka* (1975) ya E. Kezilahabi, *Njozi Iliyopotea* (1980) ya C. G. M. Mung'ong'o na *Nyota ya Huzuni* (1981) ya G. Liwenga zilivyokataa kuimba kikasuku nyimbo za aina hiyo. Lakini, hata kule kutofuata mkondo wa kisiasa na kanuni za uandishi zilizoteuliwa na tabaka tawala, kulimaanisha kunaswa katika mkondo huo pia. Kwa mfano, kauli ya Kezilahabi katika *Gamba la Nyoka* (1975: 150) haiwezi kujinasua kufuata hali hii kwa sababu lengo lake ni kujibu na kwenda kinyume na mawazo na sheria zilizotawala wakati.

Mabadiliko katika kazi za kifasihi yalianza pale ambapo wasomi walipoongezeka katika miaka ya 1980 na kuona ya kuwa hakuna haja ya kuendelea na kufungwa na silisila za kikanuni katika utunzi wa kazi za kifasihi. Ndipo walipojitokeza waandishi mbalimbali

ambao walikiuka kanuni katika tanzu kama vile ushairi, riwaya na tamthiliya. Khamis (2007) anaeleza ya kuwa mbinu hizi mpya katika uandishi zinakubaliana na kwenda sambamba na maudhui mapya katika utunzi huo. Huu ni wakati mzuri kwa uandishi wa riwaya, wakati ambao waandishi wamepata upeo mkubwa sana wa kufaidi vituko na miujiza. Kimaudhui, riwaya hii mpya ina mtazamo wa kuyaona matatizo yetu kwa msisitizo wa ndani zaidi kuliko nje. Nje inachukuliwa kuwa ni pembejeo tu la matatizo yote. Wakati mwingine, baadhi ya watunzi wa riwaya hii hujitoa kwa kiasi fulani katika kushughulikia matatizo ya ndani ya nchi na kutazama matatizo ya kidunia na kimataifa.

Pengine haya yalishughulikiwa kwa kiasi na wanariwaya wa Kiswahili hapo zamani, lakini si kwa msisitizo na vuguvugu hili la sasa. Katika mifano yote ya riwaya hii mpya, tunaziona na kuzisikia hasira kali za waandishi wake ambao wana tamaa kwamba watawakoleza wasomaji wao woga na hasira wanapoikumbusha hadhira kitisho wanachokijua.

1.4 Tamko la Tatizo la Utafiti

Riwaya ya Kiswahili imepitia katika vipindi mbalimbali vya kiuandishi hasa katika mtindo wake tangu enzi za akina Plato na Aristostle za kufungwa na mikatale ya kikanuni hadi sasa kwa kuvunjwa kwa silisila za ukanuni huo kama asemavyo (Senkoro, 1987). Hivyo basi, kutofanyika kwa utafiti kuhusu mabadiliko ya vionjo[3] vya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili kunawanyima wasomaji, wahakiki na watafiti wa kazi za Fasihi kuielewa riwaya ya Kiswahili kwa kiwango cha juu. Baadhi yao hujikuta wakizihakiki, kuzisoma na kuzichambua kwa jicho la Kiaristostle la kufungwa na ukanuni badala ya kuzichambua kwa kuangalia mabadiliko yaliyoko katika mtindo wake wa kiutunzi. Kwa maana hiyo,

[3] Neno vionjo linatumika kama hali ya kimajaribio au mwondoko wa utanzu fulani wa Fasihi kutoka sura iliyozoeleka kwenda sura mpya ambayo haijazoeleka na inaanza kujishikashika katika utumizi wake (Khamis, 2007).

wakati mwingine hufanya wasomaji, wahakiki na watafiti kushindwa kuzielewa riwaya hizo.

Hivyo basi, ili kuziba pengo hilo mtafiti aliamua kutafiti juu ya mabadiliko ya vionjo vya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili. Kwa kufanya hivi, mtafiti amewalinganisha Shaaban Robert na Said A. Mohamed katika riwaya zao ili kudhihirisha mabadiliko hayo ya riwaya ya Kiswahili, na riwaya hizo ni *Adili na Nduguze*, *Utu Bora Mkulima*, *Babu Alipofufuka* na *Utengano*.

1.5 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una malengo ya jumla na malengo mahususi kama yalivyoorodheshwa na mtafiti katika utafiti huu.

1.5.1 Lengo la Jumla

Utafiti huu unalenga kuchunguza mabadiliko ya kiuandishi yajitokezavyo katika vipindi mbalimbali vya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili.

1.5.2 Malengo Mahususi

a) Kubainisha mikondo mbalimbali ya kiuandishi inayojitokeza katika riwaya ya Kiswahili;

b) Kulinganisha na kulinganua vionjo vya kiuandishi katika riwaya za Shaaban Robert na Said A. Mohamed, na;

c) Kuchunguza sababu za kuwapo kwa mabadiliko ya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili.

1.6 Maswali ya Utafiti

a) Ni mikondo gani mbalimbali ya kiuandishi inayojitokeza katika riwaya ya Kiswahili?

b) Ni kwa namna gani kuna ufanano na utofauti wa vionjo vya kiuandishi kati ya riwaya za Shaaban Robert na Said A. Mohamed?

c) Ni sababu gani zinazofanya kuwapo kwa mabadiliko mbalimbali ya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili?

1.7 Manufaa ya Utafiti

Utafiti huu ni muhimu kwani utatoa dira kuhusu mabadiliko ya vionjo mbalimbali vya kiuandishi ambavyo riwaya ya Kiswahili imepitia hadi kufikia riwaya hii tuliyonayo sasa hivi. Pili, wasomaji wa utafiti huu watapata kujua sababu za mabadiliko hayo katika riwaya ya Kiswahili na athari zipi zitokanazo na mabadiliko hayo ya vionjo vya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili. Tatu, ni kuwahamasisha watafiti wengine waweze kumakinikia zaidi mabadiliko haya ya riwaya ya Kiswahili zaidi katika kipengele cha vionjo vya kiuandishi, sio tu katika riwaya bali hata katika ushairi na tamthiliya ambazo pia ni tanzu nyingine za Fasihi ambazo nazo zina vionjo mbalimbali vya kiuandishi. Nne, kuwawezesha walimu na wasomaji wa Fasihi kuijua zaidi riwaya ya Kiswahili kupitia utafiti huu hasa kwa waandishi hawa teule. Tano, kuonesha changamoto mbalimbali ambazo riwaya ya Kiswahili inakabiliana nazo hasa katika kupata maana halisi ya riwaya ya zamani na riwaya mpya. Sita, utafiti huu utasaidia zaidi katika kuongeza uhifadhi wa taarifa za waandishi teule.

1.8 Historia za Waandishi Teule

Historia hizi za waandishi teule zinafafanuliwa na mtafiti kutoka katika vyanzo mbalimbali ambavyo vilisaidia kupata historia za waandishi hawa.

1.8.1 Historia ya Shaaban Robert

Shaaban Robert kama ajulikanavyo historia yake aliweza kufika hapo alipo kwa sababu ya kazi zake za uandishi. Shaaban Robert alizaliwa tarehe 01 Januari 1909, huko vibambani

kusini ya Machui, yapata maili sita kusini mwa mji wa Tanga nchini Tanzania. Sehemu hiyo iliitwa vibambani kwa sababu kulikuwa na mimea ambayo iliitwa vibamba ambayo ilikuwa kwa wingi katika sehemu hiyo, hivyo kufanya mahali hapo kupewa jina hilo. Mimea hiyo ilitumika kutengeneza vikapu, mikeka na kutengeneza kifaa cha kuvulia na kuanikia samaki (Taib, 2009).

Baba yake Shaaban Robert aliitwa kwa majina matatu ambayo ni Bwana Ufukwe jina ambalo lilitokana na muktadha wa kiutamaduni (mila na desturi). Inasemekana mtoto huyo alizaliwa ufukweni wakati mama yake akitanda dagaa kwani walikuwa wakiishi karibu na mto katika kiunga cha mzee Kailembo kwa jina maarufu Mtoni, na ndipo hapo nyanya'ake Shaaban Robert akajifungua huko ufukweni na mtoto wake akapewa jina la babu yake aitwaye Yusuff bin Juma. Hii ndiyo asili ya jina la Ufukwe. Jina la pili ni Selemani ambalo linatokana na muktadha wa dini ya Kiislam; na jina la tatu ni Robert asili yake ni Juma ambaye alikuwa akifanya kazi ya upishi kwa mzungu mmoja (wa Kidachi) aliyekuwa padre huko Msimbazi Dar es Salaam. Baada ya mzee Juma kupelekewa taarifa kwamba mkewe amejifungua mtoto wa kiume, kwa furaha aliyokuwa nayo juu ya taarifa hiyo, ilimbidi amueleze tajiri yake habari hiyo ya kujaaliwa kupata mtoto wa kiume. Tajiri huyo akasema huyo rafiki yangu ataitwa Robert kwa sababu Padre huyo alikuwa na rafiki yake anayeitwa jina hilo. Kama ilivyo desturi ya matajiri na watu maarufu kwa wakati huo, akikupendekezea kitu huwa ni fahari kwa mtu wa hali ya chini ndipo jina la Robert lilipotokea (Taib, 2009).

Ponera (2010) anaeleza kuwa, babu yake Shaaban Robert aliitwa bwana Jumaa. Jina hili alilipata baada ya kukutana na msichana huko Tanga na kumpenda. Baada ya kumpenda ili ampate ilimbidi asilimishwe ndipo aweze kuozeshwa binti huyo. Ndipo alipobadili jina kutoka Kanduru na kuitwa Bwana Jumaa. Mama yake Shaaban Robert aliitwa bi Mwanamwema Bint Mwindau. Kwa jumla, Shaaban Robert ni muunganiko wa makabila

mawili yaani kwa upande wa mama yake ni Mdigo kutoka Tanga na upande wa baba ni Myao kutoka Ruvuma wilayani Tunduru. Mzee Selemani ambaye ni babu yake na Shaaban Robert katika ujana wake alikuwa karani serikalini, alihamia Machui Tanga. Huko akamuoa Mwanamwema bint Mwindau mama yake na Shaaban Robert. Alikuwa ni wa ukoo wa Mwamwende kutoka Msengenyani kabila la Akinagala. Kabila hili ni mchanganyiko wa kabila la Kizigua na Kidigo yaani mama Uziguani na baba Udigoni.

Baada ya baba yake Shaaban Robert kufariki ilibidi aende kuishi na babu yake Dar es Salaam. Baada ya kufika huko alianzishwa shule iliyoitwa Kichwele ambayo kwa sasa ni Uhuru Mchanganyiko mwaka 1922 hadi 1926. Huko alisoma vizuri na kushika nafasi ya pili kati ya wanafunzi kumi na mmoja. Kabla ya kuja Dar es Salaam alikuwa akisoma madrasa ambako alijifunza mambo mengi ya maadili ya Kiislam na alishawahi kwenda jandoni kufundwa mambo ya mila za Waswahili. Baada ya kuhitimu alifanya kazi katika serikali ya wakoloni akiwa na chini ya umri wa miaka ishirini na moja. Baba yake Shaaban Robert au kwa jina Seleman bin Juma alifariki Mnyanjani tarehe 14/9/1918 na mama yake alifariki tarehe 18/12/1967.

Shaaban Robert alifariki tarehe 20/06/1962 katika hospitali ya Bombo Tanga, na kuzikwa tarehe 22/06/1962[4] katika makaburi ya ukoo wa mama yake yaliyopo hapo hapo Vibambani Tanga. Alifariki akiwa na miaka Hamsini na tatu (53). Chanzo cha kifo chake kinatajwa kuwa ni kufanya kazi kwa muda mrefu bila kupumzika. Pia, baadhi ya watafiti wanataja kuwa ni kwa sababu ya homa ya Kifua Kikuu. Alilazwa katika hospitali hiyo kwa muda mrefu akianzia katika wodi ya Kawaida kisha alihamishiwa katika wodi ya wagonjwa mahututi na hapo ndipo umauti ulipomkuta jagina huyu wa Fasihi (Gibbe,

[4] Kuna ubishi kuhusu tarehe ya kuzikwa kwake. Mwanawe Ikbal S. Robert katika mahojiano na mtafiti alisema inasemekana alizikwa tarehe 21/06/1962 (Mazungumzo kati ya Ikbal Shaaban Robert na mtafiti yaliyofanyika tarehe 15/12/2015 mjini Dar es Salaam).

1978; Tib, 2009; Ponera, 2010). Shaaban Robert alifanikiwa kufanya kazi katika ofisi zifuatazo:

i) Alianza na kazi ya Ukarani wa serikali Forodhani Pangani mwaka 1926-1944.
ii) Idara ya hifadhi ya Wanyamapori (Mpwapwa) mwaka 1944-1946.
iii) Alifanya kazi katika Ofisi ya Mkuu wa Jimbo Tanga mwaka 1946-1952.
iv) Afisa wa kupima nchi Tanga (Idara ya ardhi) mwaka 1952-1960.
v) Pia kabla hajastaafu mwaka 1960, aliwahi pia kuhamishiwa Old Moshi.

Kutokana na juhudi alizoonesha Shaaban Robert katika kufanya kazi alifanikiwa kupata tuzo nyingi lakini miongoni mwa tuzo kubwa alizozipata ni;

i) Margaret Wrong Memorial Prize.
ii) Mwanafamilia wa himaya ya Uingereza (Member of British Empire) yaani (MBE).
iii) Mwandishi bora wa kazi za fasihi (Gibbe, 1978).

Taib (2009) anazungumzia juu ya maandiko ya Shaaban Robert katika uhai wake kuwa alifanikiwa kutunga kazi za kifasihi nyingi sana zaidi ya (20) ambazo zipo katika makundi mawili yaani nudhumu (ushairi) (14) na nathari (riwaya) (10) jumla ni kazi ishirini na nne ingawa inasemekana kuna kazi ya ishirini na tano. Aliwahi kuwa mwanachama wa ‘East African Swahili Language Committee’, ‘East African Literature Bureau’ na ‘Tanganyika Language Board’. Shaaban Robert anamchango mkubwa sana katika fasihi ya Kiswahili. Kazi hizo ni hizi zifuatazo;

a) Kazi za kinudhumu/Ushairi

i) *Mapenzi Bora* (1969), Nelson, Nairobi.
ii) *Tenzi za Marudi Mema na Omar Khayyam* (1973), TPH, Dar es Salaam.
iii) *Utenzi wa Vita vya Uhuru* (1961), Oxford, Nairobi.

iv) *Almasi za Afrika na Tafsiri ya Kiingereza* (1960), Art and Literature, Nairobi.

v) *Sanaa ya Ushairi (*1972), Nelson, Nairobi.

vi) *Mwafrika Aimba* (1969), Nelson, Nairobi.

vii) *Almasi za Afrika* (1972), Nelson, Nairobi

viii) *Koja la Lugha* (1969), Oxford, Nairobi.

ix) *Insha na Mashairi* (1967), Nelson, Nairobi.

x) *Kielelezo cha Fasili* (1973), Nelson, Nairobi.

xi) *Ashiki Kitabu Hiki* (1968), Nelson, Nairobi.

xii) *Pambo la Lugha* (1966), Oxford, Nairobi.

xiii) *Masomo Yenye Adili* (1959), Art & Lit, Nairobi.

xiv) *Mashairi ya Shaaban Robert* (1971), Nelson, Nairobi (Ponera, 2010).

b) Kazi za kinathari/Riwaya

i) *Adili na Nduguze* (1952), Macmillan, London.

ii) *Kusadikika* (1951), Nelson, Nairobi.

iii) *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* (1949), Nelson, Nairobi.

iv) *Kielelezo cha Insha* (1954), Witwatersand, Nairobi.

v) *Methali na Mifano ya Kiswahili* (1997), TUKI, Dar es Salaam.

vi) *Kufikirika* (1968), Oxford, Nairobi.

vii) *Utubora Mkulima* (1968), Nelson, Nairobi.

viii) *Siku ya Watenzi Wote* (1968), Nelson, Nairobi.

ix) *Wasifu wa Siti binti Saad* (1967), Nelson, Nairobi.

x) *Barua za Shaaban Robert* (2002), TUKI, DSM (Ponera, 2010).

Pia, kazi hizi za kinathari zimegawanyika katika makundi kadhaa kama vile, barua mfano *Barua za Shaaban Robert*, Insha mfano *Insha na Mashairi*, Riwaya za kiwasifu mfano

Wasifu wa Siti Binti Saad, na Riwaya za Kitawasifu mfano *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini.* Kataka uandishi huu wa Shaaban Robert kuna sifa zinazotofautisha makundi haya hasa ya Riwaya na Insha na sifa hizo ni Urefu (idadi ya maneno), uchangamani wa vitushi, lugha inayotumika, wahusika, dhamira, na mandhari. Kwa ufupi hiyo ndiyo historia ya jagina huyu wa fasihi hapa nchini na nje ya nchi.

1.8.2 Historia ya Said A. Mohamed

Said A. Mohamed ni miongoni mwa waandishi mashuhuri katika Fasihi ya Kiswahili. Mwandishi huyu anajitokeza kuvuma zaidi juu ya utunzi wake wa kazi za kifasihi kwa kutumia mbinu ya uhalisiamazingaombwe. Mtunzi huyu ni hazina kubwa ndani ya nchi na nje ya nchi katika kukikuza na kukiendeleza Kiswahili.

Said A. Mohamed[5] alizaliwa katika kisiwa cha Pemba tarehe 12/12/1947 huko Mwembeladu Zanzibar. Katika maisha yake ya utoto hakuwahi kulelewa na baba yake mzazi maana walitalakiana na mama yake mzazi tangu akiwa mdogo. Alipata bahati ya kulelewa na mama zake wakubwa ambao ni Bi Rukia na Bi Joha. Mama yake mzazi anaitwa Bi Fatuma Said Seleman akitokea kisiwa cha Unguja na baba yeke mzazi akitokea kisiwa cha Pemba. Kutokana na mila na desturi za kwao mtoto akizaliwa huwa kwa upande wa baba, ikambidi akakae kwa upande wa baba yake mzazi Pemba. Mpaka sasa anakaa upande wa baba yake ambako ni Pemba.

Said A. Mohamed aliajiriwa na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1968. Alikuwa mwalimu katika shule ya msingi ya Kizimba ambapo alifundisha hapo baadaye akahamia katika shule ya sekondari ya Utaani. Katika shule hiyo alifundisha somo la Kiswahili na masomo mengine kama vile hesabu, bailojia na kemia. Shuleni hapo alifanya kazi kwa miaka saba akiwa kama mwalimu. Pia alifundisha chuo cha Ualimu cha Nkurumah

[5] Mazungumzo binafsi kati ya mtafiti na Prof. Said A. Mohamed yaliyofanyika tarehe 5/1/2016 mjini Zanzibar.

mnamo mwaka 1974, hapo akifundisha masomo ya sayansi na sanaa. Baada ya hapo alifanikiwa kuwa Mkurugenzi wa TAKILUKI mnamo mwaka 1985. Alifanikiwa kwenda kuomba kazi nchini Kenya katika chuo kikuu cha Moi mnamo mwaka 1987 na alifanikiwa kupewa cheo cha mwenyekiti wa Idara ya Kiswahili. Baada ya hapo alifundisha somo la Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi kwa muda wa miaka miwili. Mwaka 1990, aliitwa Japan katika Chuo Kikuu cha Osaka kwa lengo la kufundisha Kiswahili na huko ndiko alipotunukiwa Uprofesa. Baada ya hapo alienda kufundisha Ujeruma katika chuo Kikuu cha Bayreuth somo la Kiswahili. Said A. Mohamed alistaafu mnamo mwaka 2010 na kurudi nyumbani Zanzibar na mpaka utafiti huu ulipokuwa unafanyika alikuwa ameajiriwa SUZA akifundisha Kiswahili kwa wanafunzi wa Uzamivu. Lakini pia huwa anaitwa Ujerumani na Kenya kwa ajili ya kufundisha[6] (Haji, 2015).

Kwa mujibu wa Haji (2015) katika utafiti wake, maisha ya uandishi ya Said A. Mohamed yalianza tangu akiwa na umri wa miaka minane. Amerithi kipaji cha ubunifu na kiuandishi wa kazi za Fasihi, kwa mama yake mkuu aliyeitwa Bi Nyakanga. Bibi huyu alikuwa mwenye uwezo wa kuimba nyimbo za unyago na kuwa mtunzi mzuri wa Fasihi Simulizi, hasa hadithi na mashairi. Mohamed Alipata kipaji kupitia madrasa kwa kuimba na kughani kasda za kumsifu Mtume (s.a.w). Mwaka 1960, akiwa darasa la sita alitunga shairi lake la mwanzo lililoitwa "Nimfunge Ndege Gani Hata Nipate Salama". Hali hii ilimsababisha aandike mashairi mengi na kuyapeleka Sauti ya Tanzania Zanzibar, kwa sasa inaitwa ZBC Redio. Vilevile, alipokuwa akisoma Chuo cha Ualimu cha Nkuruma kilichopo Beit el Ras Zanzibar aliandika hadithi yake ya mwanzo aliyoiita "*Ndoa ya Wahindi na Wahindi*". Hadithi hii ilipata kusomwa na idhaa ya Kiswahili ya BBC.

[6] Kwa sasa Said A. Mohamed hutumia muda wake mwingi katika kuandika kazi mbalimbali za kifasihi akiwa nyumbani kwake huku akifundisha somo la Kiswahili ndani ya nchi na nje ya nchi, kwa kuwa ameshastaafu hivyo huombwa kila mara kusaidia kufundisha somo hilo (Mazungumzo kati ya Profesa Said A. Mohamed na mtafiti yaliyofanyika tarehe tarehe 5/1/2016 mjini Zanzibar).

Halikadhalika, hadithi hii inapatikana katika kitabu chake cha *Sadiki Ukipenda* ameipa jina la *Mapenzi ya Ugunduzi*.

Vilevile, Haji (2015) anaendelea kuzungumza katika utafiti wake kuwa, Said A. Mohamed alipata hamasa kubwa ya kukiendeleza kipaji chake cha utunzi na uandishi. Kipaji chake kilichochewa na Mohamed Abdullah na kikundi cha Bw. Abubakar, ambao walikuwa wanampa ushauri zaidi wa kuandika. Vilevile, alipata hamasa kubwa zaidi baada ya kitendo chake kizuri cha kuanza kuandika mashairi na kuyapeleka idhaa ya Kiswahili ya BBC huko London. Pia, idhaa ya Kiswahili ya DW iliyopo mji wa Born Ujerumani. Idhaa hizi mbili zilianzisha mashindano ya kuandika hadithi fupi. Kupitia nafasi hii Said Ahmed alipata bahati ya kushinda, na ndipo kituo cha BBC kilimpa pongezi kubwa kwa kumtia hamasa na moyo wa kuzidi kuandika kazi za fasihi. Aliweza kupata wazo la kuandika kazi yake ya mwanzo ya riwaya ya *Asali Chungu* (1977). Hii ni baada ya kuzisoma na kuhamasishwa na riwaya ya *Kiu* (1972) na *Nyota ya Rehema* (1976). Riwaya hizi zilitungwa na Mohamed Suleiman Mohamed. Said A. Mohamed ni mtunzi mahiri wa kazi za fasihi andishi ya Kiswahili. Pamoja na vitabu vingine ambavyo si vya fasihi. Vitabu vyake tunaweza kuvigawa katika makundi yafuatayo:

a) Kazi za Riwaya:

i) *Asali Chungu* (1978), Shungwaya, Nairobi.
ii) *Utengano* (1980), Longhorn, Nairobi.
iii) *Dunia Mti Mkavu* (1980), Longhorn, Nairobi.
iv) *Kiza Katika Nuru* (1988), Longhorn, Nairobi.
v) *Tata za Asumini* (1990), Longhorn, Nairobi.
vi) *Babu Alipofufuka* (2001), Jomo Kenyata Foundation, Nairobi.
vii) *Dunia Yao* (2006), Oxford University Press, Nairobi.
viii) *Nyuso za Mwanamke* (2010), Longhorn, Nairobi (Haji, 2015).

b) Kazi za Tamthiliya:

i) *Pungwa* (1988), Longhorn, Nairobi.

ii) *Kivuli Kinaishi* (1990), Oxford University Press, Nairobi.

iii) *Amezidi* (1995), East Africa Educational Ltd, Nairobi.

iv) *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2000), Oxford University Press, Nairobi.

v) *Janga la Werevu* (2011), Longhorn, Nairobi.

vi) *Posa za Bi Kisiwa* (2007), Longhorn, Nairobi.

c) Kazi za Ushairi:

i) *Sikate Tamaa* (1980), Longhorn, Nairobi.

ii) *Kina Cha Maisha* (1984), Longhorn, Nairobi.

iii) *Jicho La Ndani* (2002), Longhorn, Nairobi.

iv) *Nilipoanza Kusema na Mashairi Mengine* (2011) Longhorn, Nairobi (Haji, 2015).

d) Kazi za Hadithi Fupi:

i) *Si Shetani si Wazimu*

ii) *Mfuko Mtupu*

iii) *Sadiki Ukipenda*

iv) *Harusi ya Buldoza*

v) *Damu Nyeusi*

vi) *Kiti cha Moyoni*

vii) *Hapa na Pale*

viii) *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine* (2005), Longhorn, Nairobi.

e) Kazi za Vitabu vya Watoto

i) *Simulizi za Kibobu*

ii) *Masikini Bibiangu*

iii) *Kigari Changu na Chake*

f) Kazi za Vitabu vya Taaluma

i) *Vito vya Hekima, Simo na Maneno ya Mshangao* (1973), Longhorn, Nairobi

ii) *Misemo, Milio na Tashbihi* (1977), Longhorn, Nairobi

iii) *Kamusi ya Visawe* (1998), Hi- Tech Typsetters, Nairobi (Haji, 2015).

1.9 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu unajikita zaidi katika kuchunguza mabadiliko vionjo vya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili ulinganisho kati ya Shaaban Robert na Said A. Mohamed kwa uteuzi wa kazi zao za riwaya ambazo ni *Adili na Nduguze*, *Utu Bora Mkulima*, *Utengano* na *Babu Alipofufuka*. Kazi zao zilizo nje ya hizi hazitachunguzwa. Kama zitachunguzwa basi zitaangaliwa kwa jumla tu ili kupata picha halisi ya mabadiliko ya vionjo vya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili.

1.10 Muhtasari wa Sura ya Kwanza

Sura hii imechambua mambo mbalimbali yanayohusiana na utafiti huu. Istilahi muhimu zilizotumika katika utafiti huu zimefafanuliwa, usuli wa tatizo la utafiti, tamko la utafiti, malengo ya utafiti, manufaa ya utafiti kwa wataalamu wa fasihi na wanajamii kwa jumla na historia fupi za waandishi teule zimefafanuliwa. Sura inayofuatia inahusu kiunzi cha nadharia na mapitio ya maandiko.

SURA YA PILI

KIUNZI CHA NADHARIA NA MAPITIO YA MAANDIKO

2.1 Utangulizi

Sehemu hii inajadili nadharia iliyotumika katika kuchambua data za utafiti huu pamoja na mapitio mbalimbali yaliyotumika katika tasnifu hii ili kuziba mapengo yaliyojitokeza.

2.2 Kiunzi cha Nadharia ya Utafiti

Kila utafiti huongozwa na aina fulani ya nadharia ambayo husaidia kumuongoza mtafiti katika utafiti wake. Kwa kuwa mabadiliko haya ya kiuandishi yamekuja miaka ya karibuni basi kulikuwa na haja ya kutafiti kazi za riwaya za miaka ya 1950 na riwaya za miaka ya 1980-90 ili kuonesha mabadiliko hayo. Ndiyo maana mtafiti akawalinganisha Shaaban Robert kwa kutumia riwaya zake za miaka ya 1950 na Said. A. Mohamed na riwaya zake za miaka ya 1980-90 ili kuonesha mabadiliko hayo ya kivionjo hasa katika uandishi.

2.2.1 Misingi ya Nadharia ya Uhalisia

Mtafiti ameongozwa na nadharia ya uhalisia katika utafiti wake. Hivyo, ukusanyaji wa data, uchambuzi na uwasilishaji wake ulifanywa kwa kuzingatia nadharia hii. Wafula na Njogu (2007) wanasema neno uhalisia "*realism*" kwa Kiingereza lilitumiwa kwa mara ya kwanza kuzungumzia moja kati ya matawi mawili ya falsafa enzi za historia ya Kimagharibi. Kipindi cha enzi za kati kilitokea baina ya mwaka wa 1100-1500 BK. Kulingana na maoni ya Rene Wellek katika jarida *Neophilologus*, X1v (1961: 20), dhana ya uhalisia ilianza kutumika kwa maana hii mpya kutokea takriban mnamo mwaka 1790. Katika mwaka huo Emmanuel Kant katika chapisho lake lililoitwa *Critique of Judgment* aliitumia istilahi ya udhahania kama kinyume cha uhalisia.

Kwa mujibu wa Wamitila (2002) nadharia hii iliibuka katika karne ya 19 na hutumika mpaka leo hii. Uhalisia haukuanza kama nadharia bali lilikuwa ni tapo mojawapo maarufu katika ulimwengu wa Fasihi na lilikuwa na athari kubwa sana. Dhana hii ya uhalisia hutumika katika maana kuu mbili yaani, kuelezea tapo la kipindi maaluum cha kihistoria katika Fasihi za Ulaya. Pia, kuelezea aina ya mtazamo au tapo la kifasihi ambako kazi za kifasihi zinachukuliwa kama zinazohifadhi au kuakisi sifa za kimsingi zinazohusishwa na uhalisi. Hivyo basi, kazi zote za kifasihi zinazoangukia katika nadharia hii hazina budi kuwa akiso la maisha halisi ya jamii husika kiuchumi na kisiasa.

Kufikia mwaka 1798, wahakiki kama vile Schiller walikuwa wakitumia maneno haya yaani udhanifu (*idealism*) na uhalisia kuashiria kinyume. Kutokana na muktadha huu dhana ya uhalisia imekuja kuhusishwa na miktadha miwili. Kwanza, inatumiwa kama njia ya kutathimini hali au halia. Huu ni uhalisia wa maisha, uhalisia wa kifasihi unaashiria uwezo wa kusawiri au kwa kueleza hali kwa kuzingatia uyakinifu wa maisha. Hii maana ya pili pia ndiyo iliyotumiwa huko Ufaransa na waandishi kama vile Flaubert katika mwaka wa 1850 kuelezea kazi ya sanaa inayoonyesha maisha ya binadamu jinsi yalivyo. Uhalisia unahusu uigaji wa mazingira anamopatikana mwanadamu. Katika kitabu chake kinachoitwa *Aethetics*, mwanafalsafa Hegel alilitumia neno uhalisia kumaanisha kazi ya hali ya kisaikolojia iliyowazunguka. Hata hivyo, istilahi ya uhalisia imediriki kuhusishwa na mikondo mitatu kama vile mkondo wa mwelekeo, mbinu ya kisanii na mbinu ya kuhakiki (Wafula na Njogu, 2007).

Katika Wamitila (2002) muasisi wa nadharia hii ni George Lucas 1885-1971, anaona kuwa uhalisia ni usawiri wa uhalisi katika ukamilifu wake na kuchunguza undani wa picha inayoonekana kwa uhalisi. Msanii anatarajiwa kusawiri matukio, wahusika, matukio yanayokubalika na kuaminika katika jamii na wakati wake. Nadharia hii ina misingi yake ambayo iliwekwa na Hegel katika kitabu chake cha *Ethetics* akiona ya kuwa neno uhalisia

lilitumika kurejelea kazi za kijamii ambako kuna wahusika au mhusika anayetenda matendo kwa jinsi inayochochezwa waziwazi na hali aliyomo.

Misingi ya nadharia hii ni usimulizi wa kimuhakati (*Mimetic Narration*). Usimulizi wa aina hii ni usimulizi ambao unasimulia matukio kama yanavyotokea katika ulimwengu halisi au kwa namna inayokaribiana sana na hali iliyoko katika jamii. Mwandishi anapaswa kuyaakisi maisha ya kijamii katika ngazi ya kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa.

Wamitila (2002) anaona ya kuwa uchunguzi wa utanzu wa riwaya unaambatana na uhalisi kwa kiasi kikubwa hivyo haiwezekani kuizungumzia riwaya bila ya kutarajia mawazo yanayohusishwa na uhalisia. Wanauhalisia hufanya hili kwa kujifunga kwenye wahusika wa kawaida au wanaoweza kupatikana katika jamii halisi, kuyachunguza na kuyasimulia maisha yao na tajiriba zao, na kusawiri na kuonyesha mandhari na mazingira ya kawaida. Nadharia ya uhalisia ilichipuka baada ya kujitokeza kwa mapinduzi ya viwanda na mdororo wa uchumi. Kwa sababu kuna matatizo halisi ambayo yanaambatana na vipindi hivyo kama vile kutokuwepo kwa mitaji. Lazima mtu aijue dunia yake inayomzunguka na kuyajua mabadiliko yanayotokea katika jamii yake na dunia yake, msanii hana budi kuelewa dunia yake na vilevile hana budi kuelewa mabadiliko ya jamii ili aweze kupata masuluhisho ya kiuhalisia na kuyasawiri kama yalivyo katika kazi yake ya kifasihi. Hapo awali wasanii waliotumia nadharia hii waliwaona wana tapo la kilimbwende walitunga kazi za kinjozi katika kuyaakisi maisha lakini wao walipotunga kwa kutumia nadharia hii waliandika kuhusu uhalisia wa maisha halisi pamoja na tajiriba ambapo kazi hii imetungwa.

Ushabihi ukweli pia ni msingi mwingine wa nadharia hii. Dhana inayorejelea hali ya kutunga kazi kwa nia ya kuakisi ukweli au kukaribia ukweli uliomo katika jamii husika. Baada ya watunzi wa riwaya kuendelea ndipo ulipokuja uhalisia mazingaombwe ukielezea

maisha kwa namna ya ajabu na ya pindu zaidi katika kuelezea matukio yaliyopo katika jamii yao. Utunzi huu wa uhalisiamazingaombwe ndio umeshika hatamu sana katika zama hizi za kiuandishi na watunzi wengi ndio hutumia mbinu hii kama Said A. Mohamed alivyoitumia mbinu hii katika riwaya yake ya *Babu Alipofufuka* (Wamitila, 2002).

2.2.2 Jinsi Nadharia ya Uhalisia Ilivyotumika

Nadharia hii ya uhalisia ilitumika katika kuchunguza mabadiliko ya vionjo vya kiuandishi katika riwaya za Kiswahili katika kazi za Shaaban Robert na Said A. Mohamed. Utumizi wa nadharia hii kwa kuzingatia misingi ya nadharia, imesaidia katika kuzichambua kazi hizi kwani uhalisia ni maisha ya kawaida na ni maisha ya kila siku. Hivyo basi, nadharia hii ilituongoza katika kumuangalia mwandishi kwa kuwa hana budi kusawiri jamii yake kama ilivyo kwa kuzingatia ushabihi ukweli na utunzi wa kimuwakati. Kwa maana hiyo, mabadiliko haya ya riwaya ndivyo yanavyokweda sambamba na nadharia hii kwa kujigeza katika misingi yake.

2.3 Mapitio ya Maandiko

Maandiko yaliyopitiwa ni yale ya maktabani ambayo yalijumuisha tasnifu za watafiti mbalimbali, majarida na vitabu mbalimbali vilivyohusiana na utafiti huu.

2.3.1 Maandiko Yanayohusu Utunzi wa Kazi za Fasihi kwa Ujumla

Senkoro (2011) anazungumza juu ya utunzi wa kazi za kifasihi akijikita zaidi katika Fasihi ya Kiswahili ya kimajaribio. Namna ya utunzi wa kazi za kifasihi kwa sasa umebadilika kutoka watunzi walipokuwa wakitunga kwa kufuata misingi ya kanuni ambazo akina Plato na Aristostle walizisimika katika kutunga kazi ya kisanaa. Mabadiliko hayo yametokea katika ushairi, tamthiliya na riwaya kama Senkoro anavyosema:

> Kanuni za utanzu wowote wa Fasihi huambatana na kuamuliwa na maana ya utanzu huo. Tuongeapo kuhusu kanuni za uwanja fulani wa fasihi hapohapo tunajaribu kuangalia yale mambo yajitokezayo mara kwa mara katika uwanja huo. Pia tunazingatia ukweli kuwa kanuni hizo hazibakii hivyohivyo kwani huweza kubadilika kufuatia mabadiliko katika utanzu unaohusika (uk. 21).

Dondoo hili linatuonesha ya kuwa umajaribio huo unajitokeza katika utanzu wowote wa Fasihi. Senkoro amejikita zaidi katika tamthiliya ya Kiswahili kwa kupitia kanuni za kifasihi simulizi ambazo zinaelekea kuwa msingi wa mwimo wa mengi wa majaribio hayo. Kanuni hizo ndizo ambazo zimejidhihirisha hata katika Fasihi ya Kiswahili ya hivi karibuni ya waandishi waliofanya majaribio ya aina mbalimbali, wakiwemo wa tamthiliya, riwaya na hadithi fupi. Kanuni hizo ni kama vile: uelezwaji au utambwaji, sifa anazopaswa kuwa nazo mtambaji, hadhira na nafasi yake katika uelezaji/utambaji, taswira na ishara, mianzo na miisho ya kifomula, marudiorudio, taharuki, ucheshi, tanakali sauti, kuingiliana kwa tanzu, muundo na majina ya wahusika. Kwa mfano, katika tamthiliya ya *Lina Ubani* ya P. Muhando na *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi* ya E. Hussein. Pia, katika riwaya ni *Rosa Mistika* ya E. Kezilahabi (Senkoro, 2011). Andiko hili ni muhimu kwani limetoa dira kwa mtafiti kuhusu Fasihi ya Kiswahili ya kimajaribio ambayo ndiyo utunzi wa sasa hivi kwa kuwa kumekuwa na mabadiliko makubwa sana katika utunzi wa ushairi, tamthiliya na riwaya. Hivyo, kupitia andiko hili mtafiti amepata chachu ya kutafiti kuhusu mabadiliko ya vionjo vya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili.

Khamis (2007) anazungumzia kuhusu utunzi wa kazi za kifasihi kwa kujikita zaidi katika vionjo vya Riwaya Mpya ya Kiswahili. Neno vionjo analifafanua kama ifuatavyo:

> Neno vionjo linatumika kwa uwili wa maana hapa. Kwanza, hali ya kimajaribio au mwondoko wa utanzu fulani wa fasihi kutoka sura iliyozoeleka kwendea sura mpya inayoanza kujishikashika. Hali ya umajimaji inayotoa sifa bainifu fulani, lakini isiyo na mgando bado, na kwa hivyo kutoweza kuitwa mtindo kwa maana ya *trend* kwa Kiingereza. Pili, maana ya kuirambisha na kuionyesha hadhira kwa ‘viishira’ kukisia wapi riwaya mpya ya Kiswahili inalekea (uk. 11).

Dondoo hii inatubainishia ya kuwa, utunzi wa kazi za kifasihi umebadilika sana katika kutunga kwa nyakati hizi ndio maana Khamis ametumia neno vionjo akionesha upya katika kazi za Fasihi kama ushairi, riwaya na tamthiliya ingawaje yeye amejikita zaidi katika riwaya. Kama asemavyo Khamis kuwa:

> Ni kawaida kwamba utanzu wa fasihi hupata mtekenyo wa mabadiliko ili kuepuka kupooza na kushindwa kushawishi kwa fikra na umbuji. Kanuni muhimu hapa ni kwamba hatimaye, chenye mwanzo kina mwisho – sharti kichoke, lazima kipoteze nguvu na msisimko wake. Kwa mfano – mabadiliko ya ushairi wa Kiswahili ya kutotii sheria kali za arudhi na badala yake kunogea miundo huru, inasemekana, angalau kwa baadhi ya washairi na wasomi, ni kutokana na kupooza kwa sulubu zake za ndani, mbali na sababu nyingine za nje. Lakini kwa upande mwingine, utanzu wa fasihi, bila ya kuchoka au kupooza, huweza ukajikuta ghafla kutoweza kuhimili nguvu za matukio muhimu ya kihistoria, kitamaduni, kijamii, kisiasa, kielimu na hata kiuchumi – nguvu zinazolazimisha kubadilika kwake kifani na kimaudhui (uk. 11).

Majaribio haya yamekuja baada ya ongezeko la wasomi katika miaka ya 1980 kukataa kufuata kanuni zile zile zilizokuwepo awali ambazo zilimtaka mtu yeyote anayetaka kutunga ni sharti kuzifuata. Miongoni mwa wasomi hao ni kama vile E. Kezilahabi, Senkoro na Mulokozi. Mabadiliko haya huweza kutokea kutokana na kani mbalimbali za kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Hivyo, kufanya kazi ya kifasihi kubadilika na kukua zaidi. Andiko hili ni muhimu kwa mtafiti kwani, limemuonesha mabadiliko katika riwaya ya Kiswahili ambacho ndicho mtafiti ametafiti.

Khamis (2007) anazungumza juu ya utandawazi au utandawizi? Jinsi lugha ya riwaya mpya ya Kiswahili inavyodai. Katika andiko hili mwandishi anaizungumzia riwaya mpya ya miaka ya 1990, muda mfupi tu baada ya neno utandawazi kuingia masikioni na kuzama akilini mwetu kuanzia miaka ya 1980. Anaona ya kuwa, utandawazi ni neno ambalo ni dhahania na lenye utata mno kulingana na anayelitumia, utandawazi huu hapo awali ulijikita sana katika uchumi na siasa lakini sasa hivi upo hadi kwenye utamaduni. Kwa upande wa utamaduni anaona ya kuwa ni kuenea kwa tamaduni za kimagharibi ambazo zilikuwa hazipo awali na sasa kufanya jamii kuwa kama kijiji kimoja kutokana na

kuchangiwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Zipo baadhi ya riwaya mpya za Kiswahili ambazo kwa kiasi kikubwa zimeathiriwa na utandawazi baadhi ya riwaya hizo mpya ni *Nagona* na *Mzingile* za E. Kezilahabi, *Babu Alipofufuka* na *Dunia Yao* za Said A. Mohamed, *Ziraini* na *Zirani* ya Mkufya na *Makuwadi wa Soko Huria* ya Chachage. Sifa kuu ya riwaya hizi ni kushughulikia kwa kina matatizo ambayo yanaukabili ulimwengu wetu leo na kuwa namna nyingine hujadili jamii yetu kwa kuvuka mipaka ya kimataifa.

Anaendelea kujadili kuhusu matumizi ya lugha katika riwaya hizi mpya kwa kiasi kikubwa ni uhalisia mkavu. Sifa ya mwanzo na ambayo ni ya msingi ni ile ya usasabaadaye. Sifa ya pili ni utouzoefu akimaanisha kuwa uvunjaji wa kanuni ambazo zilizoeleka hapo awali. Ili kupata kazi ya kifasihi yenye upya ndani yake lengo kubwa likiwa ni kubadilisha mtazamo wa msomaji kwa kumwonesha ujumi wa lugha ambao utachukua makini ya msomaji, kumvuta kisanaa na kumfanya afikiri zaidi. Anatoa mfano katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* jinsi anavyocheza na lugha kwa Kiasi kikubwa. Anaendelea kuzichambua lugha za riwaya mpya kama vile lugha ya usasabaadaye, lugha ya uhakiki na mkemeo wa utandawazi, lugha ya ujengaji wa fantansia na uhalisia mazingaombwe na lugha ya mchanganyo ndini zote hizi zikiwa ni lugha zinazotumika katika riwaya hii mpya iliyoshamiri katika miaka ya sasa. Pitio hili ni la muhimu kwani limemsaidia mtafiti kujua ya kuwa kuna riwaya mpya ya Kiswahili ambayo ni tofauti na riwaya ya awali ambayo ilikuwa ikijikita zaidi katika ukanuni na hii mpya ina mkiuko wa ukanuni. Kwa kufanya hivi, bado tunaona utunzi wa kazi za kifasihi hasa katika riwaya ya Kiswahili umebadilika na kuwa na riwaya mpya ndio maana mtafiti akapata chachu ya kutafiti juu ua mabadiliko ya vionjo vya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili.

Vilevile, Khamis (2005) anazungumzia dalili za riwaya ya Kiswahili kuchukua sura mpya katika makala yake *Sign of New Features in the Swahili Novel*. Khamis anazungumzia juu ya matumizi ya mtindo wa kimajaribio katika riwaya ya Kiswahili. Mtindo huu ndio

ulioshika hatamu katika utunzi wa kazi za waandishi walio wengi kama vile Kezilahabi katika *Nagona* na *Mzingele,* Said A. Mohamed katika *Babu Alipofufuka* na Wamitila katika *Bin Adam*. Andiko hili ni muhimu kwani, linaonesha ni kwa jinsi gani utunzi wa kazi za kifasihi ulivyobadilika katika utunzi wake hadi kuja kutumia mbinu ya umajaribio ambayo ndio upya wenyewe katika utunzi wa kazi za kifasihi. Mbinu hii ndiyo ambayo inatumiwa na waandishi walio wengi siku hizi. Hivyo basi, kutokana na andiko hili mtafiti amepata shauku ya kuendelea kuchunguza mabadiliko ya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili.

Mulokozi (1996) anazungumzia juu ya umajaribio katika utunzi wa tamthiliya ya Kiswahili. Katika kipindi hiki kinachoangaliwa zaidi ni vipengele vya kifani hasa katika mtindo na lugha bila kusahau maudhui. Tamthiliya nyingi za awali zilikuwa zinazingatia mtindo wa Kiaristotle kitu ambacho kinazitofautisha na tamthiliya za sasa. Kuanzia miaka ya 1980, baadhi ya watunzi wa tamthiliya za Kiswahili walianza kubuni vipengele mbalimbali vya kifani vinavyofanya hizo tamthiliya za Kiswahili kutofautiana na tamthiliya za kizungu na kuitwa tamthiliya za Kiswahili za kimajaribio. Vipengele hivyo vya kimajaribio ni kama vile: utambaji wa ngano, majigambo, tendi simulizi na matumizi ya nyimbo katika tamthiliya. Andiko hili ni muhimu kwani linatuangazia kwa jumla ni kwa jinsi gani utunzi wa tamthiliya ulivyobadilika kutoka awali hadi sasa kuitwa tamthiliya za kimajaribio na litasaidia katika utafiti huu kwani mtafiti anajikita zaidi katika mabadiliko haya ya Fasihi ya Kiswahili husan katika riwaya ya Kiswahili.

2.3.2 Maandiko Yanayohusu Maendeleo ya Riwaya kwa Ujumla

Wataalamu wengine kama vile Bertoncin (1989) amedai kuwa riwaya ya Kiswahili ilianzishwa na Shaaban Robert (1951 na 1962). Alipoandika riwaya ya *Kusadikia* na kufuatiwa na riwaya ya *Kufikirika*. Ohly (1981) yeye anadai kuwa riwaya ya Kiswahili imeanzishwa na Kezilahabi 1974 alipoandika riwaya ya *Kichwa Maji*. Kutokana na

kuwapo kwa maelezo mbalimbali juu ya mwanzo wa riwaya ya Kiswahili ni dhahiri kwamba riwaya hiyo imepiga hatua kubwa kimaendeleo tangu ilipoanzishwa.

Maendeleo hayo yaweza kuonekana katika vipengele vya fani na maudhui. Kwa mfano riwaya za mwanzoni kuandikwa za Shaaban Robert (1951 na 1967) zilikuwa zikitumia aina ya muhusika wa namna moja ambaye alikuwa na nguvu za kishujaa huku akiwa na tabia ya aina moja kama ni mwema basi atakuwa mwema kuanzia mwanzo wa riwaya hadi mwisho wa riwaya na kama ni muovu vivyo hivyo atakuwa hadi mwisho wa riwaya. Baadaye aina hii ya wahusika ilibadilika na kuleta aina ya wahusika wa kimajumui ambao ndio wanaotumika kwa wingi katika riwaya za Kiswahili nyingi za siku hizi, kufuatana na watunzi kuangalia maisha kihalisi zaidi. Mfano wa wahusika wa aina hii wanapatikana katika riwaya za Said A. Mohamed na Kezilahabi. Mabadiliko hayo pia tunayoyaita ni maendeleo ya riwaya ya Kiswahili yanapatikana katika vipengele mbalimbali kama vile vya kimtindo, muundo, migogoro, dhamira na kadhalika (Mkubwa, 2012).

Beja (1980) akinukuliwa na Masingele (2012) amechunguza juu ya maudhui ya ujamaa jinsi yanavyojitokeza katika riwaya ya Tanzania. Andiko hili linamuonesha Shaaban Robert ya kuwa ni mwandishi wa mwanzoni wa riwaya ya Kiswahili katika kushadidia ujamaa. Mtafiti huyu pia, anaonesha ni kwa jinsi gani riwaya za mwanzoni zilivyokuwa zikishadidia suala la ujamaa katika jamii kwa kuwataka watu kuishi kwa pamoja na kutegemeana kwa kila kitu katika maisha yao ya kila siku. Shaaban Robert anajitokeza kama mshadidiaji mkuu wa ujamaa katika kuwataka watu kuishi kwa pamoja na kufanya kazi kwa pamoja katika jamii zao. Kutokana na pitio hili, mtafiti amefanikiwa kujua ya kuwa, Shaaban Robert alikuwa akihubiri suala la ujamaa katika kazi zake za kifasihi za mwanzoni ambazo mtafiti anajikita katika kuangalia mabadiliko ya riwaya ya Kiswahili kwa kumuangalia mwandishi huyu. Hii imesaidia katika kuzichambua vyema kazi hizo

alizozichagua katika utafiti wake kwa kuwa Shaaban Robert alikuwa akihubiri suala la ujamaa.

Kwa upande wake Masingele (2012) ameshughulikia suala la Mabadiliko ya riwaya ya Kiswahili kidhamira kuanzia mwaka 1970 hadi 2011. Katika kazi hii, amedhihirisha ya kuwa, riwaya ya Kiswahili huwa na mabadiliko ya kidhamira kwa kufungamana na matukio yanayoibuka kutokana na mwanadamu kupitia katika nyanja za kisiasa, kijamii na kiuchumi kwa wakati fulani na ulio maalumu. Hivyo, hufaulu kufichua ukweli wa hali halisi ijitokezayo katika jamii, kwa sababu Fasihi inatokana na jamii yenyewe ambayo kila kipindi cha maisha huwa na matukio yake maalum. Masingele akimnukuu Nyangwine na Masebo (2008:39) wanaeleza:

> Matukio hayo yanaweza kugusa jamii kwa uzuri au ubaya na kuwa dundo la moyo la kipindi hicho cha maisha, huwa pia ni mada kuu ya wakati huo kwa jamii inayohusika. Mada hiyo inaweza kujitokeza kinaganaga katika taaluma mbalimbali za jamii, fasihi ikichukua nafasi muhimu (uk. 39).

Wakizidi kuzungumza ya kuwa wakati Fasihi hii inapochukua nafasi yake muhimu, husababisha kusawiri mabadiliko hayo kupitia vipindi mbalimbali katika kutoa hali halisi jinsi ilivyo katika ulimwengu halisi. Dhamira katika riwaya hubadilika kutokana na mabadiliko katika jamii kwa kupitia vipindi tofauti tofauti kama vile Azimio la Arusha na mabadiliko baada ya serikali ya Tanzania kupitisha sera ya kuanzishwa mfumo wa vyama vingi. Utafiti huu ulikuwa ni muhimu kwani ulionesha mabadiliko hayo ya riwaya kuanzia mwaka 1970 hadi 2011. Andiko hili, lilituangazia mabadiliko hayo ambayo yalisaidia katika utafiti huu kwa kujua riwaya imebadilika vipi.

Selemani (2012) ametafiti juu ya riwaya mpya ya Kiswahili na masuluhisho ya changamoto za utandawazi. Katika utafiti huu mtafiti aliona ya kuwa, maudhui mengi yanayopatikana katika riwaya hii mpya mengi ni ya utandawazi. Maudhui ya riwaya mpya yanaakisi jamii ambavyo imo katika kasi ya mabadiliko makubwa kama ambavyo

tumekuwa tukishuhudia kuanzia miaka ya 1990 hadi leo. Riwaya mpya imekuja katika kipindi muafaka na ikiwa na malengo ya kutahadharisha jamii na kuweka bayana matatizo yanayoambatana na mabadiliko hayo, vile vile waandishi wa riwaya hii pengine wanatoa masuluhisho ya nini kifanyike ili kuepuka dosari zinazojitokeza.

Selemani anazungumza kuwa, katika miaka ya hivi karibuni waandishi wa riwaya mpya ya Kiswahili wamejikita katika kueleza changamoto zinazozikabili nchi zinazoendelea katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kiteknolojia. Changamoto anazozizungumzia katika utafiti wake ni zile za kiteknolojia, kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi na zote amezitolea masuluhisho yake katika utafiti wake. Utafiti huu umemsaidia mtafiti kujua ya kuwa kuna riwaya mpya ambayo ni tofauti na riwaya ya zamani ambayo ilikuwa ikitungwa kipindi cha mwanzoni ambayo kwa kiasi kikubwa haikujadili masuala ya kiulimwengu kama ilivyo riwaya mpya ya sasa. Kwa hivyo basi, hii inadhihirisha ni kwa jinsi gani kulivyo na mabadiliko katika riwaya tofauti na riwaya ya zamani hii ndiyo maana mtafiti amejikita zaidi katika kuchunguza mabadiliko ya vionjo vya kiuandishi katika riwaya za Kiswahili.

Vilevile Faustine (2012) ametafiti juu ya matumizi ya mtindo wa uhalisiamazingaombwe katika riwaya teule za E. Kezilahabi: Dhima na athari zake kwa hadhira. Utafiti huu unaonesha ni kwa jinsi gani mbinu hii ya uhalisiamazingaombwe ambao si mtindo uliojaa uajabu peke yake. Mwandishi wa kazi ya Fasihi huamua kwa makusudi kuweka mambo yasiyohalisika katika ulimwengu halisi ili kuwakilisha wazo fulani kwa hadhira. Hii inatokana na ukweli kwamba kazi yeyote ya kisanaa haiwi sanaa pasipokuwa na ubunifu. Kwa maana hiyo basi, matukio ya kiuhalisimazingaombwe ni matukio ambayo mwandishi huyafinyanga kiubunifu ndani ya mazingira halisi tunayoishi ili kuwasilisha jambo fulani kwa hadhira yake.

Anaendelea kueleza kuwa, uhalisiamazingaombwe ni mtindo katika fasihi ya Kiswahili ambao umewavutia wahakiki wengi wa kazi za fasihi, kutokana na mbinu zake za kifani zilizosheheni taswira na ishara mbalimbali. Wachunguzi na wahakiki kadhaa, wamechunguza na kuhakiki kazi za kiuhalisiamazingaombwe. Maswala waliyoshughulikia ni pamoja na kuangalia chanzo cha matumizi yake. Pia, wamegusia ni kwa namna gani mbinu za kifani zinazotumika katika kazi hizo zinavyofanikiwa kubeba maudhui ili kusawiri hali halisi ya maisha ya mwanadamu. Dhima kubwa ya mtindo huu ni kutaka kufikisha ujumbe kwa hadhira kwa njia ya kumfanya afikirie kwa kina nini kilichokusudiwa na mwandishi. Athari kubwa inayojitokeza katika kazi za kifasihi zilizotumia mbinu hii ya uhalisiamazingaombwe ni kutoeleweka kwa wasomaji walio wengi juu ya nini alichokikusudia mwandishi katika kazi husika. Utafiti huu ni muhimu kwani umeonesha ni kwa jinsi gani watunzi wa kazi za kifasihi walio wengi wa sasa hivi wanaitumia mbinu hii ya uhalisiamazingaombwe ambao ndio upya au mabadiliko katika riwaya ya Kiswahili.

Khamis (2007) akinukuliwa na Masingele amefafanua kuhusu mabadiliko mengine katika riwaya ya Kiswahili kuwa ni mwingiliano matini (*Intertextuality*), jambo ambalo linaufanya muundo wa riwaya hii kuwa wa kigeugeu. Mbinu hii hutokana na mtunzi wa hadithi kuchukua kifungu cha hadithi cha jamii tofauti na kuvichanganya kwa pamoja. Kwa mfano, katika riwaya ya *Nagona* Kezilahabi anasema ya kuwa:

> Mara kwa mara anaazima dhana za kivisaasili za ki-Afrika, visaasili vyenyewe, ploti na ngano za kifasihi simulizi. Hizi anazipiganisha na vitomeo vya falsafa za Kimagharibi, ishara na picha za Ukristo na Uislamu, simulizi za miungu ya ki-Giriki pamoja na kile anachokifinyanga kwa ubunifu wake yeye mwenyewe. Kwa mfano, ili *mimi* aweze kutekeleza lengo la kumpata Mwokozi wa Pili, lazima amnase paa wa kichawi kwanza. Usakaji wake wa paa huyo unaelezwa katika simulizi ya ki-Afrika ambapo mhusika mbabe anavishinda vikwazo vinne: msitu, jangwa, mto na mlima na halafu anayamudu matakwa magumu ya mfalme katika utekelezaji wake huo (uk. 18).

Mambo mengi ya ajabu na miujiza yanatokea katika simulizi inayoegemea mbinu inayoitwa *uhalisiamazingaombwe* ambamo Yesu na Muhammad wanafufuliwa na kuhuishwa. *Nagona* pia, kama riwaya za Mkangi na Mohamed, inatumia mkarara na marudiorudio kama inavyothibitishwa kwa mfululizo mkubwa wa maneno na vikundi vya maneno vinavyofanya kazi ya kisitiari, ishara na 'vitajwa' *(allusions).* Katika mfululizo na mkarara, maneno kama ukweli, mshumaa, vichaa, vicheko, ungamo kuu, ukimya, njia, barabara, mto, paa, ndege, mti (miti), msitu, milima, mabonde, duara, vitabu, ukosefu wa watu, paka, mkombozi, ajali, ndoto, maluweluwe, uta, na mshale, yanafanya kazi ya kutilia mkazo dhamira, mapuuza, uharibifu wa mazingira, unyonyaji, upumbavu, unafiki, vifo na falsafa za urasimu (Khamis, 2007). Andiko hili limetoa dira kwa mtafiti kwani mabadiliko ya riwaya ya Kiswahili ni pamoja na muingiliano matini katika riwaya zilizo nyingi kama sifa ya waandishi walio wengi kwa sasa.

Khamis (2007) anazungumzia kuzuka kwa riwaya mpya ya Kiswahili kunazungumziwa na wataalamu mbalimbali kama vile Wamitila (1991, 1997), Gromov (1998, 2004), Khamis (1999, 2001, 2004), Bertoncin (2000), Topan (2002) na Kinge'i (2002). Anaeleza ya kuwa kazi ya Fasihi huathiriwa na kile kinachotokea katika jamii yenyewe ambamo mwandishi huchota fikra, maudhui, falsafa, itikadi, jazanda, mitindo, maumbo na miundo lugha ambayo ipo katika kazi za kifasihi. Akiwanukuu Mutembei (2000) na Senkoro (1982) wanaoeleza kuwa Fasihi ni zao la jamii na haitoki kwenye ombwe tupu ndiyo maana kazi za kifashi hujadili masuala mbalimbali au matatizo yanayoizunguka jamii husika na kwa wakati husika. Naye Khamis ndivyo anavyoona ya kuwa mwandishi wa kazi ya Fasihi hatoki nje ya yale yanayomzunguka katika jamii yake na kuyaeleza kwa njia ya maandishi. Anaona ya kuwa, riwaya mpya ya Kiswahili inajishughulisha kwa kiasi kikubwa au kwa kiwango fulani na matatizo ya ndani ya nchi na jamii husika imekiuka mipaka ya kitaifa na kimaeneo. Kwa kufanya hivyo, utafiti huu umetoa mwanga

kwa mtafiti kuwa riwaya mpya inajadili zaidi matatizo ya kiulimwengu yaani huvuka mipaka ya kinchi.

Baada ya maendeleo haya kukomaa uandishi wa Riwaya ya Kiswahili kwa kiasi kikubwa umebadilika sana. Baadhi ya waandishi kama vile kina Kezilahabi, Wamitila, Said A. Mohamed na wengine wameanza kuandika kwa mtindo wa kamajaribio katika riwaya ya Kiswahili. Majaribio hayo ni uingizwaji wa vipengele vya fasihi simulizi kuingizwa katika riwaya hizo husika. Baadhi ya vipengele hivyo ni kama vile uchawi, taharuki, ucheshi, marudiorudio, taswira na ishara, kuingiliana kwa tanzu na majina ya wahusika yenye asili ya Kiafrika (Senkoro 2006). Andiko hili ni muhimu kwani limemuonesha mtafiti ya kuwa, kazi za riwaya ya Kiswahili zimebadilika kwa kiasi kikubwa katika utungaji wake na kuleta fani na maudhui mapya.

Gromov (2004) anaeleza kuwa, riwaya ya Kiswahili imefanikiwa kuchunguza jamii kwa kutumia mbinu mpya kabisa katika kueleza matatizo ya jamii mbalimbali duniani. Mbinu hizo ni mbinu za kifasihi simulizi ambazo hutumika katika fasihi ya Kiswahili ya majaribio. Riwaya ya Kiswahili imepiga hatua kwa kiasi kikubwa kwani umajaribio huo ulikuja miaka ya 1980. Waandishi wengi wa riwaya ya Kiswahili katika miaka hii hadi sasa wanatunga kazi zao kwa kufuata aina hii ya utunzi wa kimajaribio kwa kutofungwa na mikatale ya kikanuni. Makala hii ni muhimu kwa mtafiti kwani, imeonesha mabadiliko yanayojitokeza katika riwaya ya Kiswahili kwa kuitwa riwaya ya kimajaribio ambayo kwa kiasi kikubwa ina upya ndani yake wa kutokufungwa na ukanuni tofauti na ile ya mwanzo.

Mbatiah (1999:135) ameshughulikia suala la asili na maendeleo ya riwaya za kitasnifu za nchini Tanzania. Kazi hii ilituangazia jinsi utanzu huu wa nathari ulivyoanza ukihusisha vipengele mbalimbali kama vile hadithi fupi, ngano na visasili. Aidha, imetufunulia kuhusu kuzuka kwa nathari za kifutuhi mnamo karne ya 16. Nathari hizo za kifutuhi zinaendelea kutungwa hadi leo hii. Nathari hizo za kifutuhi zilikuwa zikitungwa tangu

hapo awali lengo likiwa ni kutokumchosha msomaji. Kumfanya pale anapokutana na vitu vya kutisha na kuchosha katika kazi ya kifasihi akutane na ufutuhi ili aweze kufurahi na kupata ahueni ya kujipumzisha kupitia ucheshi huo. Andiko hili ni muhimu kwani, limemsaidia mtafiti kujua asili na maendeleo ya riwaya hadi sasa.

Mlacha (1986) amefanyia uhakiki wa riwaya inayotumika kusawiri mabadiliko na migongano ya kimawazo kupitia utamaduni. Anabainisha namna kizazi baada ya kizazi kinavyouangalia utamaduni kwa jicho la tofauti kulingana na wakati unaopitia kizazi husika. Anazungumza ya kuwa, riwaya za karne ya miaka ya sabini zinaonesha jamii za Afrika Mashariki zikiwa katika migongano ambayo ilikuwepo katika jamii za asili. Kazi hii ilitusaidia kupata mabadiliko ya riwaya hasa katika kipengele cha utamaduni.

2.3.3 Maandiko Yanayohusu Waandishi Teule

Sehemu hii imepitia maandiko yanayowahusu Shaaban Robert na Said A. Mohamed kwa kuchambua baadhi ya maandiko yaliyotafitiwa na watafiti waliotangulia waliowatafiti waandishi hawa.

2.3.3.1 Maandiko kuhusu Shaaban Robert

Wapo watafiti na waandishi wengi waliojitokeza kumfanyia kazi au utafiti mwandishi huyu mashuhuri waandishi hao ni Gibbe, Senkoro na Mulokozi. Hawa hupenda kumuita Baba wa Fasihi. Shaaban Robert alikuwa ni msanii ambaye kiuandishi aliandika kuhusiana na maudhui mazito na yenye maonyo kupitia kazi zake za kinathari na kishairi hadi ikaletelezea kupewa lakabu ya muhubiri mimbarini. Shaaban Robert ametoa mchango mkubwa sana katika kuijenga jamii kimaadili, mwalimu wa lugha, mhubiri wa mimbarini kuhusu dini, mtetezi wa ujumi wa Kiafrika, mlezi wa familia, mtetezi wa maadili au mtetezi wa wanyonge (Ponera, 2010).

Khatib (2011) ametafiti juu ya chanjo na matakwa ya mwanaume katika mwili wa mwanamke ulinganisho wa ushairi wa Muyaka bin Haji na Shaaban Robert. Katika utafiti wake anafafanua ni kwa jinsi gani waandishi wengi wa ushairi wa Kiswahili wamedaiwa kuwa na matatizo katika kumtazama mwanamke katika kazi zao, hasa juu ya mwanamke na mwili wake. Muyaka bin Haji na Shaaban Robert kama washairi bora katika nyakati zao, wamekuwa wawakilishi wa matatizo hayo. Anaendelea kuzungumza kuwa, watafiti walio wengi waliochunguza juu ya mwanamke hawakutafiti juu ya dhana ya mkodoleo ambayo ndiyo ya kifeministi ya kumuangalia mwanamke kwa karibu sana. Mkodoleo huo hubainisha athari za uhusiano wa kisaikolojia juu ya nguvu ambazo mwenye kukodolea humzidi anayekodolewa.

Dhana ya chanjo inamaanisha athari zitokanazo na nguvu za sanaa ya ushairi, hasa katika upangaji wa maneno yake kishairi na taswira zinazobebwa katika kumueleza mwanamke hususan “uzuri” wa mwili na hivyo kumfanya mwanamke ajionee fahari. Khatib anaona kuwa beti nyingi zilizopo katika ushairi wa waaandishi hawa zinamsimanga na kumdunisha mwanamke kwa kiasi kikubwa. Mashairi hayo yanamfanya mwanamke aonekane kama ni patasi, dobi, yaya wa kulea watoto, mkaa jikoni, chombo cha starehe, mzalisha mali na mtenda thambi. Anaendelea kuzungumza ya kuwa hata baadhi ya mashairi ambayo yanamsifia mwanamke, siyo kwa lengo la kumsifia bali ni kutaka kumrubuni ili tu mwanaume aweze kutimiza matakwa yake au haja zake za mwili. Utafiti huu ni muhimu kwani unaonesha ni kwa jinsi gani mtafiti alivyoonesha msimamo wake juu ya Shaaban Robert kuhusu suala la wanawake, ingawaje wapo watafiti kama Ponera (2010) alizungumza juu ya kuwa Shaaban Robert alikuwa ni mpenda wanawake na huwapigania katika haki zao ijapokuwa wapo baadhi ya watafiti wanamuona Shaaban Robert ni kama panya anayeng’ata na kupuliza kuhusu hadhi ya mwanamke.

Senkoro (2011) amechambua riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote*. Katika uchambuzi wake wa riwaya hii ameona lengo kuu la mwandishi Shaaban Robert ni kuleta ujenzi wa jamii mpya endelevu. Akiitaka jamii yote iungane na kuwa kitu kimoja katika suala la dini ili kuleta jamii mpya ambayo italeta maendeleo. Anazungumza ya kuwa kuna umoja wa mataifa kwa nini pia pasiwe na umoja wa dini. Kutengana haina maana Mkristo na Muislamu wote ni kitu kimoja na inabidi kuunganika na kuleta maendeleo katika nchi husika kwa mfano anaposema:

> Siku ya Watenzi wote ni namna moja ya shani ambayo husimulia … juu ya ufanifu na ustawi na maendeleo; juu ya matamanio na haja mpya za watu wa sasa za kuwawezesha kuchukua na kuendesha maisha mageni, ambayo wameyafikia na kuandama, na kuchukuliwa kwa nguvu na, mkondo mpya wa mfululizo wa matukio… (uk. 9).

Dondoo hii inatuonesha ya kuwa ni kwa jinsi gani mwandishi alivyokuwa akiitaka jamii mpya endelevu. Katika kuileta jamii hiyo aliwataka watu kuungana yaani kuwa na muunganiko wa dini ili kuleta suluhisho la matatizo yetu hapa duniani. Muunganiko huu ndio njia nzuri ya ujenzi wa jamii mpya tuitakayo yenye usawa kati ya mtu na mtu. Pitio hili ni la muhimu kwa mtafiti kwani limesaidia kujua nini hasa alichokikusudia Shaaban Robert katika *Siku ya Watenzi Wote* ambayo nayo inatoa dira katika mabadiliko ya vionjo vya kiuandishi katika riwaya za Kiswahili husani ni kwa Shaaban Robert.

Ponera (2010) alitafiti juu ya Ufutuhi katika Nathari za Shaaban Robert maana yake, sababu za kutumiwa, na athari zake kwa wasomaji. Katika utafiti wake aliona ya kuwa, mbinu hii ya ufutuhi inatumika sana katika kazi za Shaaban Robert kwa lengo la kuondoa uchovu kwa hadhira au kwa msomaji. Pia, mbinu hii ya ufutuhi hutumika katika kuficha maudhui mazito yaliyomo ndani ya kazi hiyo husika. Maudhui hayo yanaweza yakawa ni ya kisiasa na kutokana na utumizi wa mbinu ya ufutuhi ya kutumia kejeli, maudhui hayo hufika kwa njia ya ufiche fulani na kufanya mtu asielewe moja kwa moja nini kilichokusudiwa. Akiendelea katika utafiti wake, anaona ya kuwa ufutuhi huu unatumika

katika majina ya wahusika kama vile mhusika Bora Mimi, Kaburi, Ujinga, Hasara na mengineyo mengi. Lengo kuu la utumizi wa mbinu hii ni kutofikisha ujumbe moja kwa moja ndiyo maaana msanii Shaaban Robert aliamua kutumia mbinu hii ya Ufutuhi.

Lengo kuu la kupitia andiko hili ni kwa sababu mtafiti alitumia riwaya ya *Utu Bora Mkulima na Adili na Nduguze* ambazo zinatumika katika utafiti huu pia. Pia, kwa sababu hizi ni riwaya za mwanzo za mwandishi Shaaban Robert ambazo kwa kiasi kikubwa zitatusaidia katika kupata picha halisi ya riwaya ya mwanzoni. Halikadhalika, jinsi ilivyokuwa hadi kuja kupata mabadiliko ya riwaya ya Kiswahili.

Chuachua (2010) alitafiti juu ya suala la itikadi katika riwaya za Shaaban Robert. Katika utafiti huo alilenga zaidi katika kuibua itikadi ya Shaaban Robert katika kazi zake za kinathari. Shaaban Robert katika kazi zake wengi huzichambua juu juu tu kwa kuchambua fani na maudhui. Katika utafiti wake alizichambua itikadi za Shaaban Robert kama vile itikadi ya Kijamaa na Kisoshalisti. Katika itikadi ya kijamaa Shaaban Robert alikuwa na lengo la kuwataka watu kuishi kwa pamoja na kushirikiana katika shughuli mbalimbali za kujenga taifa lao. Andiko hili, limemsaidia mtafiti kujua Shaaban Robert alikuwa na itikadi gani ambayo huchangia katika utunzi wa kazi zake za kifasihi.

Senkoro (1982:30) akinukuliwa na Ponera (2010) ametafiti juu ya ucheshi katika kazi za Shaaban Robert. Katika utafiti wake anasema kuwa ucheshi ni mbinu ya kifani ambayo wasanii huitumia katika kazi zao za kifasihi kuchekesha hadhira zao au walau kuzifanya hadhira hizo zitabasamu… Wengine hutumia ucheshi ili kuwafurahisha wasomaji, wasikilizaji au watazamaji wa kazi zao na wengine hutumia ucheshi ili kuiepushia uchovu hadhira ya kazi zao. Wako pia waandishi ambao hutumia ucheshi ili kujenga kejeli katika kazi zao, lengo likiwa ni kufikisha ujumbe uliokusudiwa katika hali ya ufiche. Andiko hili ni muhimu kwa sababu limemsaidia mtafiti kujua mbinu za ucheshi zilizotumika katika maandiko ya Shaban Robert.

Naye Taib (2009) amezungumzia juu ya Falsafa[7] katika kazi za Shaaban Robert. Katika uandishi wake Shaaban Robert alitawaliwa sana na falsafa ya kidhahania. Anaona kuwa, alifanya hivi ili dhamira yake itimie. Katika maandiko ya Shaaban Robert kuna falsafa kuu ambazo zinamtambulisha mwandishi huyu. Katika maandiko ya Shaaban Robert falsafa zinazojitokeza zaidi kulingana na utafiti huo ni tano. Falsafa ya kwanza inayopatikana katika maandiko ya Shaaban Robert ni maadili na dini ambayo ndiyo iliyotawala katika maandiko yake mengi aliyowahi kuyatunga au kuyaandika. Falsafa ya maadili inapatikana pale ambapo mwandishi Shaaban Robert alikuwa akihubiri na kuwataka watu kuishi maadili mema. Kwa kujadili suala hili la maadili lilimfanya mpaka akapewa lakabu ya muhubiri mimbarini kwa kuwa alikuwa akihubiri sana maadili. Maadili yanadhihirika kupitia maandiko yake kama vile, *Adili na Nduguze*, *Masomo Yenye Maadili*. Pia, hata katika baadhi ya maudhui yanayopatikana katika kazi zake yanahusu maadili kupitia wahusika wake kama vile Utubora na Karama.

Mtafiti huyu anaendelea kuchambua falsafa ya pili ambayo ni utu bora. Maandiko mengi ya Shaaban Robert yalijadili sana suala la utu katika maisha. Utu ndio msingi wa maisha katika jamii zetu. Suala la utu linajidhihirisha kupitia maandiko yake kama vile *Utu Bora Mkulima*, *Adili na Nduguze*, *Kusadikika na katika Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*. Kwa mfano utu aliokuwa nao Adili kwa nduguze, ingawa walimtendea mabaya mengi mno ya kupitiliza Adili aliwasamehe kwa kuwa alikuwa na utu kwa ndugu zake. Haya yanapaswa kuigwa katika maisha haya ya sasa. Mfano, mwingine ni nukuu kutoka katika *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* anasema;

[7] Falsafa ni taaluma ya kutafuta ukweli kwa njia ya kutafakari (Chuachua, 2010).

> Utu ulikuwa jambo la uashi lililohusu wanadamu wote, na kanuni ilikuwa tabia ya milele, haikufa; haifi wala haitakufa (uk 100)… Mwanadamu alikuw asi mnyama mchache wa wajibu na daraka; alikuwa kiumbe wa heshima na dhima ambaye alistahili ushirika wa adili katika ndoa. Ilikuwa nini kama si ujinga mtupu kutupilia mbali madaraka na wajibu wetu? Ilikuwa nini kama si ukosefu wa akili kujisawazisha sisi wenyewe na wanyama ilikuwa nini kama si aibu kubwa kuacha heshima iliyopambanua ubora wetu katika viumbe? (uk. 98).

Pia, falsafa nyingine inayopatikana katika maandiko yake ni falsafa ya siasa. Falsafa hii inapatikana kupitia riwaya ya *Kusadikika* akionesha kuhusu suala la uadilifu na kuelimisha uongozi ufaao. Anazungumza kuwa, hakuna maendeleo yanayopatikana katika nchi yoyote ile bila ya raia wake kushirikishwa. Pia, katika riwaya hiyo alikuwa akikosoa mfumo wa kikoloni kwa mfano katika riwaya ya *Kusadikika* anatuambia ya kuwa akina mama wote wa Kusadikika huzaa mapacha, hii ni jazanda ya utajiri uliokuwepo katika nchi ya kusadikika.

Falsafa ya mtetezi na mwalimu wa lugha ni miongoni mwa falsafa za Shaaban Robert. Katika utafiti huu mtafiti anazungumzia jinsi gani Shaaban Robert alivyokuwa mtetezi na mwalimu wa lugha kwa vitendo na kwa maandishi. Alikuwa akiwafundisha watu kutamka maneno mbalimbali ya Kiswahili, kwa mfano aliwafundisha watu wasiseme *ugari* bali waseme *ugali, kalata* bali waseme *karata*. Pia, kupitia maandiko yake inaonesha ni kwa jinsi gani falsafa hii ya mtetezi wa lugha ya Kiswahili inajidhihirisha wazi wazi. Kwa mfano shairi lake la “Titi la Mama” katika nudhumu ya *Pambo la Lugha* akizungumza juu ya kukipenda Kiswahili na kukifananisha na titi la mama ambalo kamwe halimuishi hamu. Katika *Koja la Lugha* na *Almasi za Afrika* pia amezungumzia suala hili kama mtetezi na mwalimu wa lugha ya Kiswahili. Alisisitiza zaidi kujua lugha ya Kiswahili ingawaje hata lugha nyingine hakuzidharau maana anasema zinaongeza maarifa zaidi katika ulimwengu huu. Falsafa ya ukombozi wa mwanamke na vita na ukoloni hizi zote pia ni miongoni mwa falsafa zinazopatika katika maandiko yake aliyokuwa akiyaandika. Kwa jumla falsafa ya

Shaaban Robert inasisitiza utu bora, uungwana, heshima, uadilifu, haki na usawa. Mawazo haya pia yamezungumzwa na (Njogu na Chimera, 1999).

Andiko hili limemsaidia mtafiti kujua falsafa ya Shaaban Robert ambayo inasaidia katika kujua au kuchambua kazi zake huku akiwa amejiegemeza katika falsafa yake na pia kujua mabadiliko hayo ya riwaya ya Kiswahili wakati mwingine huzingatia zaidi falsafa ya mtunzi ndio maana andiko hili ni la muhimu kwa mtafiti.

Vilevile, Khamis (2007:16) anaelezea uibukaji wa matumizi ya mtindo wa uhalisia mazingaombwe katika riwaya ya Kiswahili. Anaongelea kazi za mwanzo zilizotumia mtindo wa uhalisia mazingaombwe, hasa katika mwegemeo wake wa fantasia kuwa ni kazi za riwaya za Shaaban Robert. Riwaya hizo ni *Kusadikika* (1951), *Adili na Nduguze* (1952), *Kufikirika* (1967), *Siku ya Watenzi Wote* (1968) na *Utubora Mkulima*. Anaeleza kuwa mbinu hii ya uhalisia mazingaombwe ilianza kutumika hata katika riwaya za mwanzoni za mwandishi huyu ingawa kwa sasa mbinu hii imeshika hatamu na kukua kwa kasi na kutumiwa na waaandishi wengi kama Kezilahabi, Wamitila na wengine. Andiko hili ni muhimu kwani linaonesha ni kwa jinsi gani mbinu hii ya uhalisia mazingaombwe ilikuwa anatumika katika riwaya ya Kiswahili ya mwanzoni na hasa katika riwaya za Shaaban Robert kama vile *Adili na Nduguze* na *Utu Bora Mkulima* ambazo pia, zinatumika katika utafiti huu. Ijapokuwa kwa sasa ndio mbinu iliyoshika hatamu katika uandishi wa riwaya za Kiswahili ambayo ndiyo mabadiliko ya riwaya ya Kiswahili katika vionjo vya kiuandishi.

Naye Momanyi (2001) ameandika juu ya nafasi ya mwanamke katika ushairi wa Shaaban Robert. Momanyi anaona kuwa maisha ya kila siku ya mtunzi yanachangia katika uandishi wa mtunzi kwa kiasi kikubwa. Mazingira ya kihistoria, kijamii, kisiasa na kiuchumi nayo yanachangia pia. Maandiko yaliyo mengi ya Shaaba Robert yanazungumzia suala la mwanamke, ili kuleta jamii mpya alisisitiza na kukemea unyonge

wa mwanamke na lengo likiwa ni kuleta jamii mpya endelevu. Katika andiko hili mwandishi anachambua jinsi Shaaban Robert alivyokuwa akimchukulia mwanamke: kwanza ni kama pambo, pili mwanamke kama kifaa cha mwanaume, tatu mwanamke kama kiumbe asiyeaminika na nne ana unyenyekevu wa lugha. Andiko hili limetoa dira kwa mtafiti kwani amejua jinsi Shaaban Robert alivyokuwa anawachukulia wanawake katika kazi zake za kifasihi.

Kwa upande wa Oriedo (2000) amechambua kuhusu fani katika riwaya za Shaaban Robert: *Kusadikika*, *Utubora Mkulima* na *Siku ya Watenzi Wote* (Uhakiki wa Kiurasimikanuni). Katika utafiti wake alibainisha ya kuwa fani ndicho chombo cha kusafirishia ujumbe katika kazi ya fasihi bila ya fani hata maudhui nayo hayawezi kufikishwa ipasavyo. Kinachowatofautisha wasanii mbalimbali katika kuibua upekee wa kazi zao ni fani ya uandishi ya kila mmoja. Ndiyo maana akaamua kufanyia utafiti kuhusu fani katika kazi za Shaaban Robert kwani walio wengi walitafiti juu ya maudhui pekee. Hairidhishi kushughulikia maudhui pekee bila ya kujua mbinu za kisanaa zinazofinyanga na kuyawasilisha maudhui aliyokusudia mwandishi. Uhalisi unaoeleweka katika maudhui ya riwaya hizi huweza tu kuonekana wazi na kuiathiri hadhira iwapo msanii ametumia vizuri fani ya kazi yake ikilandana na kushonana vilivyo na maudhui hayo. Hivyo basi, kwa kufanya hivi mtafiti aliona ya kuwa si vyema kuchambua maudhui pekee bila ya kuchambua fani katika riwaya hizo za Shaaban Robert.

Utafiti huo ulibainisha mbinu mbalimbali za kisanaa au za kifani zilizotumika katika riwaya hizi za Shaaban Robert za *Kusadikika*, *Utu Bora Mkulima* na *Siku ya Watenzi Wote.* Fani ndio hutoa maana ya kazi nzima katika kazi za kifasihi na vipengele alivyovitafiti katika utafiti wake na vinavyojitokeza zaidi katika riwaya hizo ni muundo, msuko wa matukio, usawiri wa wahusika na mandhari. Katika kuhakiki alijikita zaidi katika uteuzi wa maneno, mikabala ya usimulizi, taswira, taharuki, monolojia, dayalojia,

semi za kitamathali, balagha na matumizi ya istiari jinsi yanavyojitokeza katika riwaya hizo teule alizozichagua mtafiti. Andiko hili ni muhimu kwani linatoa dira kwa mtafiti kuhusu mbinu mbalimbali za kisanaa au za kifani zilizotumika katika riwaya za Shaaban Robert ambazo baadhi yake zinatumika katika utafiti huu.

Palome akinukuliwa na Oriedo (2000) anamzungumzia Shaaban Robert ya kuwa alikuwa ni mtunzi aliyetuachia hazina kubwa na alikuwa ni mtunzi mashuhuri katika wakati wake huo. Hakusita kuzungumzia matukio mbalimbali yaliyokuwa yakitokea katika bara la Afrika kwa kina na kwa mapana zaidi ya hali ya juu huku pia akionesha mapenzi yake mema aliyokuwa nayo kwa bara la Afrika. Mapenzi yake na utamaduni wake, lugha yake ya Kiswahili na hili linajidhihirisha kupitia shairi la “Titi la Mama” li tamu halimuishi hamu kamwe ndiyo maana alikipenda na kukidhamini Kiswahili kama lugha yake iliyomkuza.

Gibbe (1978) pia anachambua maudhui yaliyomo katika ushairi wa Shaaban Robert. Katika uchunguzi wake anaenda mbele zaidi hata kukishughulikia kipengele cha fani katika kazi za Shaaban Robert. Mtaalamu huyu alijikita zaidi katika kushughulikia mbinu za kifani zinazojitokeza katika ushairi wa Shaaban Robert bila ya kuchambua kipengele cha maudhui kwa kina. Mbinu hizo za kifani alizozichambua katika ushairi wa Shaaban Robert ni kama vile wahusika, ubunilizi, naratolojia, msuko wa vitushi, lugha na mianzo na miisho ya kifomula. Uchunguzi huu umemsaidia mtafiti katika utafiti huu kwani mbinu za kifani zinazojitokeza katika ushairi wa Shaaban Robert ndio zinazojitokeza katika riwaya za Shaaban Robert na mbinu hizo za kifani zina vionjo vya kimabadiliko katika uandishi ambavyo ndiyo mabadiliko yenyewe katika uandishi wa riwaya ya Kiswahili.

2.3.3.2 Maandiko Kuhusu Said A. Mohamed

Said A. Mohamed ni miongoni mwa waandishi maarufu hapa nchini. Umaarufu wake unajulikana kutokana na utunzi wa kazi za fasihi ambazo kwa kiasi kikubwa zimeegemea

katika upya wa kiutunzi au umsaragambwe[8]. Tunapozungumzia upya katika kazi zake ina maana ya kuziasi kanuni ambazo zilikuwepo awali katika utunzi wa kazi za kifasihi za Kiswahili na yeye kuja kuzikiuka au kuzivunja katika utunzi wa kazi za kifasihi. Anajulikana kama mtunzi wa riwaya za kimabadiliko au kimajaribio katika utumizi wake wa mbinu ya uhalisia mazingaombwe kiasi kwamba baadhi ya watu husema kazi hizo ni ngumu kuzielewa. Wapo watafiti na wataalamu waliofanya utafiti kuhusu Said A. Mohamed na kazi zake kama wafuatao:

Haji (2015) ametafiti juu ya matumizi ya utanzia katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed. Mtafiti huyu alijikita zaidi katika kuangalia matukio ya kitanzia jinsi yanavyojitokeza katika kazi za riwaya za msanii teule huku akiangalia athari zinazojitokeza kwa msomaji baada ya kuyatambua matukio hayo ya kitanzia katika kazi husika za mwandishi Said A. Mohamed. Anazungumza ya kuwa utanzia ni hali ya matendo ya wahusika ambayo yanatoa athari ya huzuni, simanzi na woga kwa watazamaji. Mtafiti huyu aliona mbinu ya utanzia hutumiwa na waandishi walio wengi kwa lengo la kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa ijapokuwa zipo mbinu nyingine kama vile taharuki, taswira, uchawi, ushirikina na uhalisiamazingaombwe, mwingiliano-matini, matumizi ya ndoto, usayansi na matumizi ya kejeli. Anaendelea kuzungumza kuwa fani na maudhui ndio moyo wa kazi za kifasihi, hauwezi ukawa na maudhui bila ya fani, na fani bila ya maudhui. Utanzia ni kipengele kimojawapo kilichopo katika fani hasa katika mbinu za kibunilizi. Ndiyo maana mtafiti akaamua kutafiti juu ya dhana hii ya utanzia kwa kuwa, watafiti walio wengi wametafiti juu ya maudhui kwa kiasi kikubwa na kusahau fani. Na hata kama wametafiti fani basi ni kwa kiasi kidogo tu. Utafiti huu ni muhimu kwa kuwa umemsaidia mtafiti kujua mbinu za kifani katika kazi za mwandishi teule hasa katika

[8] Neno umsaragambwe katika tasnifu hii limetumika kwa maana ya zama za kiuandishi zilizotokana na zama za kiuandishi za kidemokrasia. Kwa kiasi kikubwa, uandishi wa zama hizi uligubikwa na kuakisi uhalisi wa maish; kwamba, maisha yenyewe si kitu chenye kanuni nyoofu bali ni changamani sana. Waandishi au wasanii wa kipindi hiki wakazongwa na kumezwa na ukweli wa kimaisha nao hutunga kiuchangamani (Khamis, 2007).

kipengele cha utanzia kwani fani ndiyo inayotusaidia katika kufikisha kile kilichokusudiwa na mwandishi kwa hadhira yake.

Naye, Wanjiru (2013) ametafiti juu ya uhalisia ajabu katika riwaya mpya ya *Babu Alipofufuka* ya Said A. Mohamed na *Watu wa Gehanna* ya Tom Olali. Utafiti huu unaonesha vipengele vya uhalisia ajabu ambavyo vinajitokeza katika riwaya hizo teule. Pia, ameonesha ni kwa nini mbinu ya uhalisia ajabu ni njia muafaka zaidi ya kusoma na kuzifahamu riwaya hizi mbili za waandishi hawa teule. Katika riwaya zao waandishi hawa wametumia lugha yenye ubunifu mwingi, uhusika usiozoeleka na mandhari ya kiajabu kusawiri kazi zao. Waandishi hawa wamekuwa wakitumia mbinu hii ya uhalisia ajabu katika kutunga kazi zao kitu ambacho kinaleta shida kati ya yale tunayoyajua katika uhalisia na yale ambayo hatuyaelewi katika ndoto, lakini yanaonekana kama mambo halisi. Utafiti huu ni muhimu kwani mtafiti ametafiti riwaya ya *Babu Alipofufuka* na kuonesha ni kazi ya kihalisia ajabu ambayo ndio mabadiliko yenyewe katika riwaya ya Kiswahili kwa kuwa hapo awali mbinu hii ilikuwa haitumiki sana kama inavyotumiwa kwa wakati huu na watunzi katika kusana kazi zao.

Daudi (2013) ametafiti juu ya nafasi ya kejeli na dhihaka katika tamthiliya teule za Said A. Mohamed. Katika utafiti huu mtafiti aliona ya kuwa kejeli na dhihaka ni vipengele ambavyo watunzi mbalimbali huvitumia katika kazi zao ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Vipengele vingine ni tamathali za semi, taharuki, ishara na picha. Vipengele hivi ni sehemu muhimu ya fani katika kazi yoyote ya Fasihi. Utafiti huu ulilenga kuchunguza na kuzibainisha kejeli na dhihaka katika tamthiliya tatu za Said A. Mohamed na kuchunguza matumizi ya kejeli na dhihaka yanavyosaidia kufikisha ujumbe kwa wasomaji wake. Mtafiti aliona ya kuwa kejeli na dhihaka ni mbinu muhimu inayotumika katika Fasihi kama jinsi ilivyotumiwa na Said A. Mohamed katika tamthiliya zake teule alizozichagua mtafiti ili kufikisha ujumbe wake aliokusudia kwa hadhira yake.

Makulla (2012) ametafiti juu ya athari za uhalisia mazingaombwe kwa msomaji katika kuzielewa kazi za fasihi za Said A. Mohamedi. Katika utafiti wake aliona ya kuwa uhalisia mazingaombwe ni mbinu ya kifasihi inayochanganya uhalisi na matukio ya ajabu ajabu ambayo hayazoeleki wala kuaminika kwa hadhira. Hali hii huzua taharuki kwa wasomaji na kutaka kujua nini maana yake. Hivyo, kuwavuta wasomaji kuendelea kuzisoma sura zinazofuata wakitaraji kubaini maana inayoashiriwa katika matukio hayo. Athari hiyo inajitokeza pale ambapo mwandishi ametumia mbinu hii kwa kuchanganya matukio ya kiajabu ajabu, wahusika wa ajabu ajabu na mandhari ambapo humtaka msomaji kuwa na umakini na upembuzi wa hali ya juu kufahamu juu ya nini kilichokusudiwa na mtunzi. Utafiti huu ni muhimu kwani umetuonesha ni kwa jinsi gani mbinu hii ya utunzi kwa kutumia uhalisia mazingaombwe ulivyoshika hatamu katika utunzi wa riwaya ya Kiswahili ambayo ndiyo mabadiliko yenyewe ya vionjo vya kiuandishi.

Pia, Ligopola (2012) amejadili kuhusu nafasi ya Mwanamke ambacho ni kipengele kimojawapo muhimu cha maudhui katika kazi za kifasihi katika uwasilishaji wa kazi za Fasihi. Waandishi wa kazi za Fasihi hutumia kipengele cha maudhui kusawiri mambo mbalimbali yaliyomo katika jamii. Anaonesha kuwa Said A. Mohamed katika kazi zake kama vile *Utengano, Asali chungu*, *Tata za Asumini* na *Babu Alipofufuka* ametumia ufundi wa hali ya juu katika kumchora mwanamke na nafasi yake katika jamii. Utafiti huu umetoa dira juu ya kumsawiri mwanamke katika kazi za Said A. Mohamed akionesha kumchora mwanamke katika hadhi tofauti tofauti kama vile chombo cha starehe, mtawa, mtu asiye na sauti na hata mwanamke yupo tu kwa ajili ya kutimiza matakwa na haja za mwanamume. Andiko hili ni muhimu katika utafiti huu kwani limemsaidia mtafiti katika kupata mwongozo wa kujua kizungumzwacho katika riwaya ya *Utengano* na *Babu Alipofufuka* maana ndizo kazi ambazo mtafiti alizitumia katika utafiti wake.

2.4 Mapengo Yaliyozibwa

Baada ya kupitia maandiko ya wataalam na waandishi mbalimbali waliotafiti juu ya mabadiliko ya riwaya ya Kiswahili na waandishi teule, mapengo yanayojitokeza ni haya yafuatayo: Kwanza, wataalamu hawa hawajatoa kipaumbele katika kuchunguza mikondo mbalimbali ya kiuandishi inayojitokeza katika riwaya ya Kiswahili. Pili, hawajachunguza sababu mbalimbali za kuwapo kwa mabadiliko ya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili kama ilizungumziwa basi walizungumzia juu juu tu.

Utafiti uliofanyika unakusudia kuziba mapengo kwa kuchunguza mikondo mbalimbali ya kiuandishi inayojitokeza katika riwaya ya Kiswahili huku wakilinganishwa kati ya Shaaban Robert na Said A. Mohamed katika riwaya zao teule ambazo ni *Adili na Nduguze*, *Utu Bora Mkulima*, *Babu Alipofufuka* na *Utengano*. Pia, kuchunguza sababu za kuwapo kwa mabadiliko ya kiuandishi katika riwaya za Kiswahili.

2.5 Muhtasari wa Sura ya Pili

Sura hii imejadili kwa kina kiunzi cha nadharia iliyotumika katika tasnifu hii pamoja na maandiko au mapitio mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti juu ya mabadiliko ya vionjo vya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili ulinganisho wa Shaaban Robert na Said A. Mohamed na baada ya hapo kuzungumzia mapengo yanayotakiwa kuzibwa na mtafiti. Sura inayofuata inazungumzia kuhusu methodolojia ya utafiti.

SURA YA TATU

METHODOLOJIA YA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inafafanua mpango wa jumla wa utafiti huu, eneo la utafiti, jamii za watafitiwa, zana na mbinu za kukusanyia data, uhalali na uthabiti wa matokeo ya utafiti, mchakato wa kukusanya data pamoja na uchambuzi wa data.

3.2 Mpango wa Utafiti

Utafiti huu ulifanyika maktabani na uwandani. Utafiti huu ni wa kitaamuli. Katika maktaba yalipitiwa maandiko na machapisho yanayohusu utunzi wa kazi za Fasihi kwa jumla, maandiko yanayohusu maendeleo ya riwaya kwa ujumla na maandiko yanayowahusu waandishi teule wa riwaya za Kiswahili waliochaguliwa na mtafiti, yaani Shaaban Robert na Said A. Muhamed. Uwandani mtafiti alikwenda kufanya mahojiano na baadhi ya watu ili kupata maoni kuhusu jinsi wanavyoona mabadiliko ya riwaya ya Kiswahili hasa katika vionjo vya kiuandishi.

3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika maeneo ya Dodoma, Dar es Salaam, Tanga na Zanzibar ambapo data za maktabani na uwandani zilikusanywa. Maeneo haya ya Dodoma na Dar es Salaam yameteuliwa kutokana na urahisi wa upatikanaji wa taarifa za kimaktaba pamoja na wataalamu waliobobea katika uga wa Fasihi kutoka katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM). Tanga na Zanzibar yameteuliwa kwa sababu ya upatikanikaji wa taarifa za waandishi hawa teule.

3.4 Walengwa wa Utafiti

Katika kipengele hiki kutakuwa na makundi mawili ambayo ni jamii ya watafitiwa na maandiko yanayohusiana na mada husika.

3.4.1 Wango Tafitiwa

Wango tafitiwa ni jumla ya vitu vyote ambavyo vinaweza kumsaidia mtafiti katika upatikanaji wa data za utafiti huu. Vitu hivyo huweza kugawanywa katika makundi ya eneo fulani la kijiografia, kundi la watu na maandiko yanayohusiana na mada husika. Jamii iliyohusika kutoa taarifa katika utafiti huu ni kama ifuatayo:

i. Riwaya mbalimbali za Shaaban Robert na Said A. Mohamed ambazo ndizo zitakazoonesha mabadiliko hayo ya vionjo vya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili.

ii. Ndugu, jamaa na marafiki wa Shaaban Robert na Said A. Mohamed ambao watasaidia katika kujua maisha halisi ya waandishi hawa.

iii. Wanataaluma mbalimbali waliowahi kuwafanyia utafiti au tahakiki za waandishi hawa teule ili kupata mitazamo yao juu ya maandiko ya waandishi teule. Pia, wanafunzi wanaosoma somo la Fasihi ambao wengi wao wameshazishughulikia riwaya hizi za waandishi teule.

3.4.2 Sampuli ya Watafitiwa na Upatikanaji Wake

Kothari (2002) anafafanua kuwa sampuli lengwa ni mbinu ambayo humtaka mtafiti kuchagua wawakilishi wa watafitiwa katika utafiti wake. Uchaguzi huo unaweza kutokana na jinsi gani wanaweza kukidhi haja na malengo ya utafiti huo. Mbinu hii ya sampuli lengwa hutumika zaidi katika data za kiufafanuzi zaidi. Sampuli yenyewe ilijumuisha yafuatayo:

a) Riwaya nne za waandishi hawa yaani mbili za Shaaban Robert ambazo ni *Adili na Nduguze* na *Utu Bora Mkulima* na mbili za Said A. Mohamed ambazo ni *Utengano* na *Babu Alipofufuka*.

b) Wanajamii watano watano kutoka Mkoa wa Tanga kwa Shaaban Robert na Zanzibar kwa Said A. Mohamed ambao watatueleza maisha halisi ya waandishi hawa.

c) Wataalamu na watafiti watano waliowahi kuwafanyika utafiti waandishi hawa teule ambao watapatikana kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).
d) Wasomaji na wahakiki kumi ambao walishawahi kuhakiki maandiko haya teule kutoka katika vyuo mbalimbali katika mkoa wa Dar es salaam na Dodoma.
e) Mtunzi mwenyewe Said A. Mohamed kwa sababu bado yupo hai.

3.5 Ukusanyaji wa Data

Sehemu hii inazungumzia kuhusu njia na zana mbalimbali zilizotumika katika kukusanya data na mchakato wa ukusanyaji na udhibiti wake.

3.5.1 Njia na Zana za Kukusanyia Data

Njia kuu zilizotumika katika kukusanya data ni mbili ambazo ni udurusu wa kimaktaba na mahojiano. Zana zilizotumika katika kukusanyia data za utafiti huu ni mwongozo wa udurusu wa tasnifu na vitabu mbalimbali vihusianavyo na mada hii, mwongozo wa mahojiano. Zana nyingine ni vijidaftari, kalamu, kamera na kinasa sauti. Zana hizi zilitumiwa kwa sababu ya kiini cha utafiti huu wenyewe kwa kuwa uliangalia elimu,upeo wa eneo la kijiografia la watafitiwa.

3.5.2 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data

Data za maktabani zilikusanywa kwa njia ya kudurusu, ambapo mwongozo wa usomaji ulitumika katika kusoma vitabu, tasnifu na majarida mbalimbali yahusianayo na mada husika. Data za uwandani zilikusanywa kwa njia ya mahojiano. Mtafiti alitumia njia ya mahojiano ili kuwahoji wanataaluma wa Fasihi ya Kiswahili pamoja na wataalam ambao waliwahi kuandika maandiko ya Shaaban Robert na Said A. Mohamed, pamoja na wakazi wa Tanga na Zanzibar. Pia, mtafiti aliwatumia wasomaji na wahakiki kumi ambao walishawahi kuhakiki maandiko haya teule kutoka katika vyuo mbalimbali katika mkoa wa Dar es Salaam na Dodoma. Mtafiti alimuhoji pia mtunzi mwenyewe Said A.

Mohamed. Daftari na Kalamu vilitumika kunukuu data zilizopatikana katika mahojiano. Kinasa sauti kilitumika kuwarekodi wahojiwa kwa yale wayazungumzayo kutokana na maswali ya mtafiti. Kamera ilitumika katika kupiga picha na vielelezo mbalimbali vihusianavyo na utafiti huu.

3.6 Uchanganuzi wa Data

Kwa kuwa utafiti huu ni wa kifafanuzi hivyo basi, uchanganuzi wa data na utoaji wa matokeo ulifanywa kwa maelezo. Uchambuzi wa data katika utafiti huu ulizingatia nadharia ya uhalisia kwa kujigeza katika mhimili mmoja wa utunzi wa kimuhakati. Data zilichambuliwa na kupangwa kulingana na malengo na maswali yaliyoongoza utafiti huu. Mbinu za ufafanuzi na uchambuzi wa matini ndizo zilitumiwa katika kuchambua data, kwani utafiti huu ni wa maelezo zaidi na si wa kitakwimu. Data za uwandani na maktabani zimewianishwa ili kutathmini ubora na uthabiti wake.

3.7 Itikeli za Utafiti

Utafiti huu umezingatia zaidi itikeli maalum za kiutafiti ili kulinda heshima ya wahusika watakaohusika katika utafiti. Itikeli za utafiti hujuisha masuala yafuatayo:

i) Kuwa na ruhusa maalum ya kufanya utafiti kutoka katika taasisi au asasi husika;
ii) Uombaji wa ridhaa ya watafiti;
iii) Kuwajuza watafitiwa malengo ya utafiti;
iv) Kuwajuza watafitiwa kuhusu uhuru wa kushiriki katika utafiti. Na kwamba, wanaweza kujitoa wakati wowote wajisikiapo kufanya hivyo;
v) Utunzaji wa siri za taarifa zitolewazo na watafitiwa;
vi) Ufichwaji wa majina ya watoa taarifa kadiri ya matakwa yao, na;
vii) Uzingativu wa maadili ya jamii za wahusika (Ponera, 2014).

3.8 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti

Uhalali wa utafiti maana yake ni hali ya utafiti kuwa na uwezo kupima jambo au mambo yaliyotakiwa kupimwa au kutafitiwa tu. Na kuhusu uthabiti wa utafiti, ni hali ya utafiti kuweza kutoa matokeo yanayowiana ikiwa utafanyika katika wakati mwingine, mahali pengine, au na mtu mwingine (Ponera, 2014). Mtafiti ametumia mbinu zaidi ya moja wakati wa kukusanya data kwa watafitiwa. Mbinu hizo ni kama vile hojaji na udurusu. Pamoja na hayo, mtafiti alichambua riwaya teule zilizotumika katika tasnifu hii. Kwa minajili hiyo, matokeo ya utafiti huu yana kiwango kikubwa cha uhalali na uthabiti.

3.9 Vikwazo vya Utafiti

Katika utafiti huu mtafiti alikumbana na matatizo au vikwazo vya aina nyingi. Miongoni mwa matatizo hayo ni kama ifuatavyo: Kwanza, uhaba wa fedha kama ilivyo kawaida suala la utafiti ni la mchakato mrefu linalohitaji fedha za kutosha. Kwa maana hiyo, ili kuja na majibu yaliyo na mashiko na usahihi zaidi. Uhaba wa fedha ulikuja kutokana na kuwa mtafiti alifinywa na bajeti anayopewa na taasisi ya utoaji wa fedha kwa ajili ya utafiti ya elimu ya juu. Taasisi hii hutoa fedha za utafiti bila ya kuzingatia bajeti ya mtafiti kitu ambacho kwa kiasi kikubwa kazi ya utafiti ni kubwa ikihitaji vitu kama gharama za usafiri kwa ajili ya kwenda kukusanya data, gharama za uchapishaji wa tasnifu na gharama za kujikimu kwa mahitaji kama vile chakula na malazi ambayo kwa maisha ya sasa ni ghali mno, hivyo, pesa hiyo haikuweza kutosha kwa kweli na kufanya suala la utafiti kwa mtafiti kwenda kwa kusuasua. Pili, wanafunzi walio wengi dhana hii ya vionjo ni ngeni masikoni mwao kiasi kwamba ilimbidi mtafiti walau atoe muhtasari kidogo kuhusiana na dhana hii ndipo ieleweke, wakati huo huo kwa upande wa riwaya ya Said A. Mohamed ya *Babu Alipofufuka* kwa kiasi kikubwa ilileta changamoto kutokana na wanafunzi au walio wengi kusema ni riwaya ngumu na isiyoeleweka na hata kama anatokea kuielewa basi huielewa juu juu tu. Tatu, baadhi ya watafitiwa hawakuwa na

utayari wa kutoa ushirikiano kwa mtafiti hasa sehemu za familia za waandishi teule kila mmoja akiwa na imani yake kulingana na kuhojiwa. Hali hii ilisababisha kukosekana kwa baadhi ya taarifa muhimu zinazohusu utafiti huu hivyo ikambidi mtafiti kutumia ushawishi wa hali ya juu na busara zake katika kulitatua suala hili ili aweze kupata data.

3.10 Muhtasari wa Sura ya Tatu

Sura ilianza kuonyesha mpango wetu wa utafiti huu. Data zilipatikana maktabani na uwandani. Katika ufafanuzi wa data njia ya maelezo ilitumika kwa kiasi kikubwa kwa kuwa ni utafiti wa kitaamuli. Pia, mbinu na zana za utafiti zimebainishwa vyema pamoja na maeneo teule ambayo ni mkoa wa Tanga, Zanzibar, Dar es Salaam na Dodoma. Sura ya nne inahusu uwasilishaji na mjadala wa matokeo ya utafiti.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha na kuchambua mjadala wa matokeo ya utafiti uliofanyika. Sura imegawanyika katika sehemu kuu tatu zinazolandana na maswali yetu ya utafiti. Sehemu ya kwanza inaeleza kuhusu mikondo mbalimbali ya kiuandishi inayojitokeza katika riwaya ya Kiswahili. Sehemu ya pili imechambua kulandana na kutofautiana kwa vionjo vya kiuandishi kati ya Shaaban Robert na Said A. Mohamed. Sehemu ya tatu inafafanua sababu za kuwapo kwa mabadiliko ya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili.

4.2 Mikondo ya Kiuandishi katika Riwaya ya Kiswahili

Kwa kuwa tunajadili na kuchambua mikondo ya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili basi hatuna budi kujadili kwanza matapo ya sanaa kwa sababu kubwa ya kumuonesha msomaji uhusiano mkubwa uliopo kati ya matapo haya ya sanaa na mikondo hii ya kiuandishi katika riwaya Kiswahili. Kwa kiasi kikubwa, mikondo hii imechangiwa au imetokana na matapo haya ya sanaa. Hivyo yanajengana na kukamilishana.

4.2.1 Riwaya ya Kiswahili na Matapo ya Sanaa

Sanaa ya kiulimwengu imepitia katika matapo mbalimbali. Matapo hayo kwa kiasi kikubwa yamechangia sana katika kukuza na kuendeleza Fasihi ya kiulimwengu. Fasihi ya Kiswahili nayo haikukwepa miegamo na vionjo vya kiuandishi ambavyo huendana na miondoko ya matapo haya ya sanaa. Kuna matapo ambayo Fasihi ya ulimwengu mzima imepitia na matapo hayo sio lazima kupitiwa katika Fasihi ya jamii au nchi fulani.

4.2.1.1 Tapo la Urasimi Mkongwe

Tapo hili la urasimi mkongwe inasemekana lilianza kati ya miaka ya (850-325 K.Y. M). Urasimi ni wakati maalumu ambapo misingi ya kazi ya sanaa huwekwa na kukubaliwa na

jamii kwamba ndiyo mizani bora kwa kazi nyingine katika muktadha wa jamii hiyo (Njogu na Chimerah, 1999). Hivyo basi, urasimi ni mkusanyiko wa mikondo ya kifikra au kimtazamo ambayo chanzo chake ni Fasihi na utamaduni wa Wayunani. Dhana hii ya urasimi kwa kiasi kikubwa ilikuwa katika usimikaji wa sheria na taratibu mbalimbali za kuongoza utendekaji wa sanaa au fasihi katika jamii husika. Historia ya urasimi inaonekana kuwa urasimi ni tapo lililokuwepo kuanzia miaka ya 850 hadi 325 KYM. Wawakilishi wakuu wa tapo hili ni kama vile Gorgias, Socrates, Plato na Aristotle.

Wanafalsafa hawa waliweka kanuni na misingi mbalimbali ya kazi za sanaa. Vilevile, waliegemeza mawazo yao mengi katika nadharia ya mwigo kama msingi ambao uliendelea kuzingatiwa na kazi nyingine zilizofuatia kipindi hicho. Urasimi una vigezo vyake muhimu na mahususi ambavyo misingi yake iko katika maandishi na matamko ya Warumi na Wayunani, wanazuoni na wahakiki wa mwanzoni. Katika kipindi hiki tunapata vipindi vitatu vya urasimi kama ifuatavyo:

Zama za Homer, ni zama ambazo visakale ndivyo vilivyotawala katika fasihi simulizi. Masimulizi hayo yalihusu vita na mashujaa kama vile *Trojan War*. Masimulizi hayo yalighanwa kwa mdomo na baadaye yalihifadhiwa katika maandishi; ambapo tunapata epiki za awali ambazo ni *Illiadi* na *Odssey*. Sifa kuu ya kipindi hicho ilikuwa ni vita na vurugu. Pia, kulikuwa na zama za kirasimi za Kiyunani (800-200) Kabla ya Masihi. Kipindi hiki kinatambuliwa kwa kuwapo kwa watunzi wa Kiyunani wa Kifalsafa kama vile Arisophanes, Socrates Aristotle, Plato na Sophocles. Kuanzia karne ya tano zilitokea kazi mbalimbali za kisanaa kama vile tamthiliya, ushairi na chimbuko lake ni mji wa Venas Ugiriki. Hali kadhalika, zama za kirasimi za Warumi (200-455) Kabla ya Masihi. Kipindi hiki, utamaduni wa Kiyunani ulibadilishwa na utamaduni wa Warumi. Sehemu kubwa ya tapo hili liliongozwa na nadharia ya mwigo (Njogu na Chimera, 1999).

Tapo hili linaongozwa na mawazo makuu yaliyotoka kwa wanaurasimi mkongwe kama vile akina Plato (427-347 KYM) na Aristosle (384-322 KYM) juu ya wao waionavyo sanaa na jinsi mtunzi alivyotakiwa kutunga kazi ya kisanaa ili ikubalike na jamii husika kwa kipindi hicho. Katika tapo hili, Plato anasifika zaidi katika kusimika sheria na kanuni ambazo kwazo mtunga mashairi yoyote yule ni lazima kuzifuata hadi kazi yake iweze kukubalika katika jamii hiyo. Kanuni hizo ni kama vile mtunga mashairi yoyote atakayetunga mashairi ni lazima ushairi huo upitiwe na kamati maalum ya watu wenye umri wa zaidi ya miaka hamsini, pili watunga mashairi wote lazima wawe na umri wa zaidi ya miaka hamsini na kuendelea, tatu ushairi lazima ueleze mambo mazuri tu kama vile juu ya mashujaa na watawala wa nchi, nne washairi wasitunge chochote kilicho kinyume na sheria za jamhuri na lazima mashairi yote yafuate urari wa vina na mizani. Bila sheria hizi ushairi haukukubaliwa katika kipindi hicho. Plato anasifika zaidi katika kutunga sheria za kisanii katika kumbo ya ushairi kwa kufanya hivi, ilimlazimu kila mtunzi kuzifuata sheria hizi na kwa kiasi kikubwa ziliacha athari kubwa sana katika utunzi wa nyakati hizo katika kumbo ya ushairi.

Kwa upande wa tamthiliya, Aristostle anajitokeza zaidi katika kusimika mihimili ya tamthiliya ambayo kwayo mtunga tamthiliya ilimlazimu kuifuata ndipo kazi yake ikubalike. Mihimili hiyo kama vile sanaa lazima iwe na hadhira mbili yaani nasaba bora (tanzia), na watu wa nasaba duni (ufutuhi), lakini, miundo itofautiane kama ni tanzia au ufutuhi, tatu kama ni tamthiliya lazima pawe na nguzo muhimu ambazo ni muundo, wahusika, nyimbo, wazo kuu, hadhira na lugha bora kulingana na hadhira. Hivyo basi, kikubwa katika tapo hili ni waandishi wengi waliokuwepo katika tapo hili ni wale waliofungwa na kanuni ambazo zilimlazimu kila mtunzi alipotaka kutunga katika tapo hili kufuata sheria na kanuni hizo za wanaurasimi kongwe ndipo kazi hiyo ikubalike kutumiwa katika jamii husika kwa kipindi hicho. Tapo hili kwa kiasi kikubwa lilikuwa na

vigezo kama vile kuzingatia fani mahususi, kuoana kwa fani na maudhui, kueleweka kwa kazi ya sanaa, urahisi, ulinganifu, kutiliwa maanani kwa muundo na mpango mahususi, mtindo mahususi, muungano na ulinganifu wa kazi. Pia, kuheshimu jadi, mwigo na kuzingatia mawanda yaoanayo na fani na maudhui ya kazi ya sanaa, bila ya kufuata vigezo hizi basi kazi ya kisanaa ilionekana kutokukidhi haja na matakwa ya jamii husika, na hivyo kazi hiyo haikukubalika (Senkoro, 1987).

Tapo hili lilijitokeza katika Fasihi ya Kiswahili pia. Senkoro (1987) ameainisha tapo hili kwa kuzingatia ushairi. Ushairi unaingia katika tapo hili kwani kanuni nyingi za kipindi hiki cha urasimi mkongwe zinatokana na ushairi kuliko kumbo yoyote ile ya Fasihi. Sababu kubwa ya ushairi na kanuni hizo kujitokeza zaidi katika kipindi hiki ni kutokana na upo muumano mkubwa wa kanuni kati ya ushairi wa kimapokeo na ule wa Kirumi na Kigiriki uliotawala katika kazi nyigi za watangulizi wa mwanzoni kama vile Plato, Arisostle na Socrates. Katika kipindi hiki kulikuwa na kanuni kama za urari wa vina na mizani katika ushairi. Ulazima wa kuwa na muundo mahususi wenye mwanzo ulio na dibaji unaomuhusiha msanii na Mungu, suala la kupagawa ambako kulimtaka mtunzi kupata nguvu kutoka kwa Mungu ndipo aweze kutunga kazi hiyo kwa kupewa hekima na Mungu. Lugha pia iliyotakiwa kutumika katika ushairi wa kirasimi ilitakiwa kuwa lugha rasmi na yenye ufasaha.

Tapo hili linaonekana kuacha athari kubwa hata kwa watunzi wa Fasihi katika Kiswahili kama vile Abdilatif Abdalla, Sheik Amri Abeid Kaluta, Saadan kandoro na Mayoka. Washairi wote hawa wanaonekana kufuata kanuni za wanaurasimi mkongwe ambazo ndizo ziliwaongoza katika kutunga kazi zao kwa kipindi hicho. Kipindi hiki cha urasimi mkongwe kilimtaka mtunzi yoyote wa kazi za kisanaa kufuata kanuni hizo ndipo kazi yake iweze kukubalika katika jamii. Wanaurasimi mkongwe waliona ya kuwa kama shairi halitafuata urari wa vina na mizani basi shairi hili halina maana ya kuwa shairi.

4.2.1.2 Tapo la Urasimi Mpya

Senkoro (1987) anaeleza kuwa, tapo la urasimi mpya inasemekana lilianza katika miaka ya (1680-1750 BYM). Ni tapo ambalo kwa jumla, lilisitiza sana kuhusiana kwa mantiki na mjadala katika kazi za sanaa baada ya kuzuka kwa washairi ambao ni dhahania kati ya miaka ya (1662-1680). Kati ya tapo hili na tapo la urasimi mkongwe tofauti yao kubwa ni kuzuka kwa washairi dhahania ambao walielezea mgongano kati ya mahitaji na mwili na yale ya roho. Katika kipindi hiki ndipo riwaya maarufu ya washairi wa kidhahania ilitungwa ya John Bunyan ya *Pilgrim's Progress* ambayo imefasiriwa kwa lugha ya Kiswahili kama *Safari ya Msafiri*. Kwa kiasi kikubwa tapo hili la urasimi mpya liliendeleza yale yale yaliyokuwepo katika urasimi mkongwe hasa kwenye kutunga kazi za kisanaa. Senkoro, (1987) analifafanua tapo hili kuwa, katika tapo la urasimi mpya mtu alionekana kuwa yu kiumbe ambaye hakukamilika, aliye na kasoro na ambaye alihitajiwa arekebishwe katika fasihi au sanaa.

Sanaa ya wakati huu ilisisitiza sana mpango mahususi, kuhalalisha kila kitu kielezwacho ndani ya sanaa, na kufuatwa kwa sheria za utungaji zilizoambatana na aina ya utanzu wa sanaa. Wanaurasimi mpya walisisitiza sana kuwa sanaa lazima iwe kwa ajili ya mtu, kuwepo kwa mpango mahususi katika kazi ya sanaa na kazi ya sanaa lazima ziwe na fumbo litakalomfikirisha hadhira.

Wanaurasimi mpya walisisitiza zaidi kufaulu au kutofaulu kwa sanaa ya kipindi hicho kwani haikuweza kumzingatia mtu. Baadhi ya waandishi maarufu katika tapo hili ni John Dryden, Alexander Pope na Nicholas Boileua. Tapo hili lina athari kubwa kama vile msisitizo katika uchaguzi mahsusi na mzuri wa maneno katika ushairi pamoja na umuhimu wa taswira katika ushairi na msisitizo kuhusu umuhimu wa matumizi ya akili badala ya jazba tu umesababisha kuzuka kwa utanzi wa kejeli katika fasihi andishi.

Njogu na Wafula (2007) wanaugawa urasimi mpya katika makundi mawili ambayo ni urasimi mpya wa Kimangaribi na ule wa Fasihi ya Kiswahili. Kwa kuwa katika sehemu hii tunajadili kuhusu matapo ya sanaa ya kiulimwengu basi tutauzamia zaidi urasimi huu wa Kimagharibi. Urasimi wa kimangaribi unaitwa hivyo kwa sababu kimsingi kanuni zake nyingi zimetokana na urasimi mkongwe katika sanaa. Katika kipindi hiki ndipo kulishuhudiwa ufufuajia wa kanuni na sheria zilizokuwa zikiheshimika na wanaurasimi katika fasihi. Kwa miaka iliyopita urasimi mpya ilionekana kutokuwa na mawanda ya kurejelewa katika fasihi. Kufikia karne ya 17 na 18 huku magharibi walikuwa tayari wameshapiga hatua katika maendeleo ya sayansi na uchumi. Kwa maana hiyo katika kipindi hiki njia za kisayansi katika kudadisi jambo zilikuwa zimeshika hatamu kwa kiasi kikubwa huko Magharibi.

Ndipo baada ya maendeleo haya ya kisayansi kulipotokea uhusishwaji wa Fasihi na urasimi mpya wa Kimagharibi ambapo wasanii wengi waliamini ya kuwa Fasihi nzuri ni ile ya Wagiriki na Waroma wa kale. Hivyo basi, sababu hii iliwafanya wasanii na wahakiki wa kazi mbalimbali za kisanaa kuzichambua na kuzihahiki kazi za watangulizi wao kwa kutumia sayansi kwa sababu kipindi hiko kilikuwa kimeshapiga hatua katika sayansi na hivyo walichunguza miundo na mitindo kisayansi. Walizichunguza kazi za wanaurasimi mkongwe kama vile Plato, Aristostle, Horace na Ovid huku wakiangalia sheria na mbinu zao walizokuwa wakizitumia katika kutunga kazi zao. Wahakiki muhimu wa kipindi hiki walikuwa Samuel Johnson, Alexander Pope na watunzi walikuwa ni Jonathan Swift, John Milton na Edmund Spenser (Njogu na Chimera, 1999).

Vilevile, tapo hili liliacha athari katika Fasihi ya Kiswahili. Huu ni wakati ambao kulitokea kazi za kirasimi zilizotokana na urasimi mkongwe. Hii ina maana kuwa kaida, kanuni na sifa za utunzi zilizotumika katika urasimi mkongwe ndizo zilizosisitizwa na kufuatwa katika kipindi hiki. Sababu za kurudi katika utunzi wenye kufuata sifa za

urasimi mkongwe ni kutokana na mwamko mpya miongoni mwa jamii kuona kuna umuhimu wa kurudia misingi na kanuni zilizowekwa wakati wa urasimi mkongwe. Urasimi wa fasihi ya Kiswahili ulifikia kilele chake baina ya karne ya 18 na 19. Kipindi hiki kilitawaliwa sana na ubora wa ushairi wa Kiswahili uliotungwa zaidi sehemu za Lamu kaskazini mwa mwambao wa Kenya. Hivyo ushairi ni uga uliotangulia kuweka misingi au vigezo vya utunzi wa kisanaa. Kazi za mwanzo kabisa za kipindi hiki ni pamoja na *Utenzi wa Tambuka* wa Mwengo Bin Athuman (1728). *Utenzi wa Hamziya* ulitafsiriwa na Said Aidarus (1749 na wengine husema ni 1690). Tungo nyingine za wakati huu ni kama *Al-Inkishafi, Fumo Lyongo, Mwanakupona.*

Katika kipindi hiki katika Fasihi ya Kiswahili walijitokeza watunzi wa ushairi kama akina Shaaban Robert, Amri Abeid Kaluta na Mathias Mnyampala. Hawa wanaonekana kuanza kuukacha ukanuni huo ingawaje bado walikuwa wakiutumia katika kusana kazi zao za kifasihi. Katika kazi za waandishi hawa urasimi mpya unaanza kuonekana, Kwa mfano shaaban Robert katika kazi zake anaonekana ni mrasimi mpya ingawaje sio kwa mara zote (Senkoro, 1987).

Njogu na Chimerah (1999) wanaujadili urasimi mpya katika Fasihi ya Kiswahili kuwa ulianza kutokea katika kipindi cha giza kati ya mwaka 1885 na 1945. Katika kipindi hiki ndio wakati ambapo mataifa ya Ulaya yalikuwa yakiling'ang'ania bara la Afrika na kulikuwepo vita kuu mbili za dunia. Kutokana na hali hizi hata uandishi nao ulikuwa ukisuasua kwa kiasi kikubwa. Kipindi hiki ndicho mwandishi wa Fasihi ya Kiswahili anajaribu kuandika kazi za kifasihi kwa kutumia uelewa wake na nafasi yake katika jamii.

Watunzi wa kipindi hiki wanaojitokeza zaidi ni Shaaban Robert, Amri Abeid, Khamisi Amani, Mathiasi Mnyampala na Ahmad Nassir. Watunzi hawa wanaonekana kutoa mawazo yao katika kazi zao kuhusiana na utunzi wa kazi za kishairi ambao pia unarudi kule kule katika urasimi mkongwe. Kwa mfano, Shaaban Robert anafafanua maana ya

ushairi kuwa ni kama sanaa ya vina inayojibainisha kama nyimbo, mashairi na tenzi huku yakifundisha jamii mwenendo unaofaa. Mnyampala anaona kuwa, sanaa ya ushairi ni msingi wa maneno ya hekima tangu kale. Kwa maana hiyo, urasimi mpya ulijikita zaidi katika kufufua kanuni zilizokuwepo kwa wanaurasimi mkongwe na ndiyo maana hata waandishi wanaojitokeza katika kipindi hiki kwa kiasi kikubwa wapo pande zote kwa urasimi mpya na mkongwe.

4.2.1.3 Tapo la Ulimbwende

Tapo hili lilianza kati ya miaka ya (1790-1870), ni tapo liloanzia barani Ulaya karne ya (18-19) na kushamiri karne ya (20) hasa baada ya mapinduzi ya Ufaransa. Tapo hili kwa kiasi kikubwa lilishadidia sana uhuru wa mtunzi au wa mwandishi katika kutunga kazi ya kisanaa. Katika tapo hili mtunzi yupo huru kuisana kazi yake atakavyo bila ya kufungwa na aina yoyote ya silisila za kikanuni katika utunzi wake, anaweza akatumia wahusika wa ajabu na mandhari ajabu katika kazi yake na ikakubalika katika jamii.

Ndipo katika tapo hili kwa kiasi kikubwa dhana ya Fasihi ya kimajaribio ya Kiswahili inapojitokeza kwani watu wapo huru kutunga watakavyo, suala la msingi ni hadhira ipate ujumbe uliokusudiwa na mtunzi wa kazi hiyo. Mathalani, hapa ndipo walipozuka watunzi wa ushairi huru au mashairi huria yasiyofungwa na mikatale ya kikanuni. Mashairi katika tapo hili hayakuzingatia ile kanuni ya urari wa vina na mizani na hata shairi si lazima liimbike, walichoangalia ni ujumbe tu umfikie hadhira aliyekusudiwa. Vigezo vya jumla vya wanaulimbwende ni kutilia mkazo mazingira halisi, kuandika au kusana kazi mbalimbali zilizowazunguka wahusika kuanzia utotoni, matumizi ya wahusika wa ajabu ajabu kama vile, shetani, kuruhusu matumizi ya ndoto zilizovuka mipaka ya uhalisi wa maisha. Kwa kiasi kikubwa hapa ndipo waandishi wengi walipoibuka kuandika kazi za kisanaa kwa kufuata mkondo huu na ndipo palipozua mjadala mkubwa wa wanazuoni na waandishi kuhusiana na fasihi inayotungwa katika tapo hili. Tapo hili ndilo lililochangia

kuzuka kwa watunzi wa zama hizi ambao wanaandika kazi zao kwa uhuru wa hali ya juu (Senkoro, 1987).

4.2.1.4 Tapo la Uhalisia

Muasisi mkuu wa tapo hili ni Hegel. Tapo hili lilijishughulisha na utanzu wa riwaya, katika tapo hili maisha yanaelezwa kama yalivyo katika uhalisi wake. Mkabala huu ni kinyume kabisa na ule wa wafuasi wa ulimbwende na matapo mengineyo. Katika tapo la uhalisia wahusika wa kazi za Fasihi husawiriwa katika uhalisi wa maisha yao ya kila siku kama yalivyo katika jamii husika. Tapo hili la uhalisia lisisitiza sana yale yanayotendeka katika fasihi lazima yasawiriwe katika maisha halisi ya kila siku. Hivyo basi, uhalisia ni maisha ya kila siku ya watu wanayotenda katika jamii yao.

Vigezo vikuu vya tapo hili ni sifa ya mtunzi ya sanaa/Fasihi, demokrasia katika fani na maudhui ya kazi za sanaa/fasihi na umuhimu wa kueleza mambo yanayotokea siku hadi siku katika maisha ya watu, mambo ambayo hayana budi yaelezwe kutokana na uzoefu wa wanaoyaeleza. Mtunzi wa kazi ya kifasihi katika tapo hili alitakiwa kueleza mambo kama yalivyo katika maisha halisi kwa kiasi kikubwa ili kazi hiyo iweze kukidhi vigezo vya tapo hili. Katika tapo hili msanii hana budi kuijua dunia inayomzunguka na mabadiliko yake huku akiusawiri uhalisi kwa ukamilifu wake. Hivyo basi, kwa jumla matapo haya ya Fasihi ya kisanaa yana mchango mkubwa katika Fasihi ya Kiswahili na kuacha athari kubwa kwa watunzi wanaotunga kazi za kifasihi kwa kufuata katika matapo haya haya ya fasihi. Matapo haya ndiyo yaliyochangia kuibuka kwa dhana ya majaribio na kuifanya Fasihi ya Kiswahili kuwa yenye mabadiliko ukilinganisha na fasihi ya awali iliyokuwa ikifuata mikatale ya kikanuni katika utunzi wa kazi hizo husika kama ni ushairi, tamthiliya na riwaya.

Nayo Fasihi ya Kiswahili imepitia katika tapo la ulimbwende na uhalisia. Katika tapo hili uhuru wa mwandishi unajitokeza zaidi katika kusana au kutunga kazi ya kisanaa. Uhuru huu unajitokeza zaidi katika ushairi wa Kiswahili ambao kwa kiasi kikubwa umezua mjadala mrefu kuhusu hasa ushairi huo na sifa zake. Mjadala huu ndio uliozaa mgogoro wa ushairi kati ya wanamapokeo au jadi na wanausasa au mamboleo wakikinzana juu ya nini hasa ushairi unatakia uwe ili uitwe ushairi wa Kiswahili (Senkoro, 1987).

Method (2013) anauzungumzia ushairi wa Kiswahili kuwa, unaweza ukaainishwa kwa vigezo tofauti tofauti na ndani yake ndipo tunapopata ushairi wa kimapokeo na ushairi wa kisasa. Hili lilitokana na maendeleo ya ushairi wa Kiswahili, na palizuka malumbano dhidi ya wale waliozingatia kanuni za utunzi yaani (wanamapokeo) na wale wasiozingatia kanuni hizo katika utunzi (wanausasa).

Ushairi wa kimapokeo ni ushairi ambao, kwa hakika, unazingatia au unasisitiza urari wa vina na mizani, mishororo minne, kuimbika, utoshelevu, beti, lugha ya kishairi na muwala. Kwa jumla, ushairi huu wa kimapokeo ulizingatia arudhi kama ndio uti wa mgongo wa shairi lolote lile. Baadhi ya wafuasi wa ushairi wa kimapokeo ni akiana Mayoka, Abdalatif Abdalah, Andanenga, Amri Abeid, Shaaban Robert, Shiragdini, Kandoro, Al-Amin Mazrui na Ibrahim Sharifu.

Kwa upande wa wanausasa wanajitokeza waandishi kama vile akina Jared Angira, Ebrahimu Hussein, Euphrase Kezilahabi, Crispin Hauli, Mugyabuso Mulokozi, Kahigi na Muhanika wakidai kuwa ushairi sio lazima ufuate urari wa vina na mizani cha msingi ni kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Ndipo baada ya kutokea kwa waandishi hawa ushairi wa Kiswahili ukabadilika na wakaanza kutunga kazi bila ya kuzingatia urari wa vina na mizani na ndipo kazi hizo zikaanza kutumika katika shule na vyuoni (Senkoro, 1987). Baada ya kuvunjwa kwa kanuni katika ushairi wa Kiswahili ndipo palitokea pia mapinduzi katika tamthiliya ya Kiswahili yakiongozwa na watunzi kama akina Ebrahimu

Hussein na Penina Mlama. Kwa upande wa riwaya wanajitokeza waandishi kama akina Kezilahabi, Wamitila, Said A. Mohamed na Senkoro.

Baada ya hapo zikaja kazi za kihalisia ambazo ziliyajadili maisha kwa uwazi na upana wake. Kazi hizi kwa kiasi kikubwa zimekuwa zikiakisi maisha kama yalivyo katika jamii kwa kuchambua matatizo mazito yanayoikumba jamii hasa katika kuleta jamii mpya. Hapa zinajitokeza kazi za waandishi mbalimbali kama vile riwaya za Mohamed Suleiman, Shafi Adam, Said Ahmed Mohamed zikizungumzia juu ya matatizo mbalimbali ya wanajamii (Senkoro, 1987).

4.2.2 Mikondo ya Uandishi ya Riwaya ya Kiswahili

Riwaya ya Kiswahili imepitia katika mikondo tofauti tofauti ya kiuandishi hadi kufikia riwaya hii ya sasa. Mikondo hiyo ni hii ifuatayo:

4.2.2.1 Uandishi wa Kiteokrasia/Kiaristostle

Mkondo huu ni mkondo ambao kwa kiasi kikubwa uligubikwa na uandishi kwa kufuata kanuni au zama za kirasimi katika utunzi wa kazi za kisanaa kwa wakati huo. Kipindi hiki kwa kiasi kikubwa kiligubikwa na ufalme wa Kiungu, kwa kuwa, na kiasi kikubwa cha viongozi wa kidini na Wafalme waliopewa dhamana ya kutawala nchi kwa jumla. Kipindi hiki kilikuwa ni kipindi ambacho tawala za Wayunani na Walatini zimeshika hatamu (zama za Greek-Latino). Waandishi katika mkondo huu walilenga kutukuza Miungu waliokuwepo katika kipidi hicho, huku wakitukuza masuala mbalimbali yaliyokuwepo ya kidini wakati huo. Kipindi hiki kilijikita zaidi katika dini, falsafa, historia na sayansi kwa jamii husika. Mtunzi katika mkondo ilimlazimu kutunga kufuatana na kanuni zilizokuwepo katika mkondo huu bila ya kukiuka ili kukidhi vigezo na matakwa ya mkondo huu. Baada ya kumalizika kwa mkondo huu kuliibuka mkondo wa Kiaristostle ambao ulifuata misingi ile ile ya Kiteokrasia.

Mkondo huu wa Kiaristostle kwa kiasi kikubwa uligubikwa na ukanuni katika kutunga kazi za kisanaa. Kanuni hizo ni zile zilizokuwepo katika urasimi mkongwe. Wapo watu maarufu katika mkondo huu kama akina Aristostle na Plato. Waandishi hawa maarufu na mashuhuri katika utunzi wa kazi za kisanaa ndio waliotumika kuweka kanuni au mihimili kwa mtunzi yoyote wa kazi ya kifasihi kufuata kanuni au mihimili hiyo ya kiutunzi waliyoiweka katika kutunga kazi za kifasihi kama ushairi na tamthiliya, maana ndivyo vilivyokuwa vimeshika hatamu na baadaye kufuatiwa na riwaya (Senkoro, 1987).

Utunzi katika mkondo huu uligubikwa na mikatale mingi ya umri, aina ya maudhui, utabaka wa hadhira na aina ya sanaa. Plato anasifika zaidi kwa kuweka kanuni katika ushairi wa Kiswahili na kanuni hizo zilimtaka mtunzi yoyote anayetaka kutunga kazi ya kifasihi kuwa na umri unaozidi miaka hamsini, kusifu viongozi tuu, uongelee mambo mazuri tuu, na washairi kutoandika chochote kilicho kinyume na sheria za Jamhuri. Kwa upande wa Plato yeye alijikita zaidi katika tamthiliya kwa kutoa mihimili ya utunzi wa tamthiliya kwa kipindi hiko ambayo lazima kuwe na kichwa, kiwiliwili na miguu. Hivyo basi, kwa kiasi kikubwa katika mkondo huu wa uandishi kazi za kisanaa zilifungwa na mikatale ya kikanuni katika utunzi na kanuni hizo zilimlazimu mtu kuzifuata wakati wa utunzi kwa wakati huo katika kutunga kazi yoyote ya kisanaa ili iweze kutumika na kutumiwa na jamii husika (Senkoro, 1987).

Kwa mujibu wa Senkoro (1993) sanaa ya hapo awali ilikua na kuthibitiwa na yule tu aliyekuwa na mamlaka katika kipindi fulani au tabaka fulani. Pia, mamlaka yaliyofanya aamue kuwa kazi hii iruhusiwe au la ndiyo yaliyokuwa yakiumiza sana waandishi hasa wale ambao hawakufuata kanuni za urari wa vina na mizani. Kwa mujibu wa wanaurasimi mkongwe kanuni hizo zilikuwa ndio uti wa mgongo wa ushairi. Kwa mfano, mwandishi anasema:

> Ushairi umechujuka mara tatu kutoka katika ukweli; kwa hiyo kuanzia sasa washairi wanapigwa marufuku katika Jamuhuri yetu (Plato, *The Republic*) (uk. 37).

Mwandishi anazidi kushadidia hoja hii akisema kuwa waandishi hawako huru kuandika yale yanayowasibu, wao wanataka kuandika lakini sheria haimruhusu aandike hivyo kwa jinsi yeye anavyotaka, kufanya hivyo ni kinyume na sheria. Anasema:

> Sheria inaruhusu kuandika lakini kwa sharti moja kuwa niandike kwa mtindo usio wangu. Ninayo haki ya kuonyesha undani wa mambo, lakini nalazimishwa niuonyeshe undani huo wa mambo, kwa kupitia katika kauli isiyo yangu… Mimi ni mcheshi, lakini sheria inaniamrisha niandike bila mzaha wowote; mimi hupenda kusema mambo bila kuficha, lakini sheria hainitaki niandike hivyo (uk. 10).

Hivyo basi, kwa kuangalia mifano hii tu michache inaonesha ni kwa jinsi gani watunzi walivyobinywa na kufungwa na kanuni fulani ambazo tayari zilishasimikwa hapo awali kama ndio kipimo cha uandishi wowote ule. Ni lazima kila mtunzi anayetaka kusana kazi hizo za kifasihi kuzifuata ndipo kazi yake ikubaliwe na jamii husika bila ya hivyo hupigwa marufuku.

Kwa hiyo, suala hili la uhuru wa mwandishi analihususisha kwa kupitia katika vipindi mbalimbali kama vile ujima, umwinyi na baadaye ubepari. Ukiangalia katika vipindi hivi vyote Fasihi ilikuwa ni ya kitabaka yaani ya watu fulani ambao ni viongozi na watawala wa jamii husika. Fasihi ilipovumbiliwa katika vipindi hivi hasa Andishi, ilikuwa ni ya wateule fulani tu na hawa watawala walihakikisha kwa kila hali wanaidhibiti Fasihi ili kulinda utawala wao, na watumwa na watwana nao walikuwa na fasihi yao hasa fasihi simulizi. Katika vipindi hivi Fasihi ilidhibitiwa na kulikuwa na udhibiti kama vile wa kidini. Udhibiti huu ulifanyika hasa katika kumbo ya ushairi ambapo awali ulikuwa ni kusifu viongozi tu. Mtunzi tu anapobadilisha na kuandika kwa mambo mengine kazi hiyo ilidhibitiwa na kupingwa vikali. Katika Afrika kuna udhibiti mwingi kwa kuangalia waandishi ambao walizuiliwa kazi zao kama vile Ngugi wa Thiong’o mwandishi maarufu

kutoka nchini Kenya na kazi zake zilizodhibitiwa ni *Ngaahika Ndeenda* iliyomfanya hadi akawekwa katika mikono ya dola. Hili lilitokea baada ya kufichua maovu yaliyokuwa yakifanywa na viongozi wenye madaraka.

Wapo baadhi ya waandishi waliojaribu kuandika kwa kufichua maovu wakakemewa vikali na hata wengine kuteswa na baada ya kuachiliwa wakaamua kuhama miji yao. Mwandishi anaendelea kushadidia kuwa, waandishi wengi waliokuwa katika vipindi hivi vya kitabaka walifungwa na ukanuni wa uandishi wa kazi zao za kifasihi maana hakuna uhuru wa mwandishi. Walipaswa kuandika yale tu yaliyo mazuri bila kugusa tabaka tawala na pindi wanapoligusa tu ndipo vita inapoanza hata kufungwa gerezani na kazi zao kudhibitiwa.

Kwa upande wa udhibiti wa kazi za kifasihi, katika jamii ya Tanzania wapo waliodhibitiwa kazi zao, kwa mfano E. Kezilahabi na kazi yake ya *Rosa Mistika* iliyopigwa marufuku kutumika shuleni na vyuoni. Kazi nyingine ya *Mayai Waziri wa Maradh*i ilipigwa marufuku katika gazeti la *Mzalendo* baada ya hadithi hiyo kuzungumzia viongozi waliokuwa wakipenda uchawi ili wapate vyeo. Hivyo basi, hapo awali waandishi wengi wa kazi za fasihi walidhibitiwa na tabaka tawala ili tu waendelee kufanya uovu wao. Waliona ya kuwa wakiachia uhuru kwa waandishi hawa uovu wao utavumbuliwa na vita kali dhidi ya wanajamii itazuka (Senkoro, 1993).

Kwa mujibu wa Hug (1986) Fasihi ya Kiteokrasia hasa ya kikanuni sawa na maandiko matakatifu yaliyoko katika Biblia. Anasema kuwa:

> *Canon in its simple sense, a standard of judgment; a criterion. Conon is applied to the authorized or accepted list of books belonging in the Christian BIBLE by virtue of having been declared to be divinely inspired.*
>
> Undishi wa kikanuni kwa maana ya kawaida ni mkusanyiko wa mawazo na vigezo ambavyo hukubalika katika orodha ya vitabu vinavyomilikiwa na Biblia takatifu (Tafsiri Yetu).

Tafsiri hii inaonesha ni kwa jinsi gani uandishi wa namna hii ulivyokuwa umetuka na haukutakiwa kubadilishwa kama jinsi ilivyo kwa Biblia Takatifu. Hakuna anayeruhusiwa kubadilisha lolote katika Biblia Takatifu, ndiyo maana mwandishi huyu analinganisha uandishi huu na Biblia. Vivyo hivyo, utunzi katika mkondo huu ulipaswa kufuata kanuni zilizosimikwa na waasisi bila ya kubadilisha ili kazi hiyo iweze kukubalika.

4.2.2.2 Uandishi wa Kidemokrasia

Kwa kiasi kikubwa, zama hizo zilienda sambamba na ustawi wa ulimbwende katika Fasihi ya Kiswahili. Ulimbwende ulitokea katika karne za 18 na 19 hasa baada ya mapinduzi ya ufaransa, likianzia katika nchi za Uingereza, Ufaransa na Ujerumani. Msingi mkuu wa ulimbwende ulishadidia zaidi katika uhuru wa mwandishi katika kusana kazi ya kisanaa. Katika zama hizo kwa mara ya kwanza mwandishi alipata uhuru wa kutoka katika minyororo na silisila za sheria zilizokuwa zikisisitizwa nyakati za urasimi na urasimi mpya. Chimbuko la mkondo huu ni uandishi uliokiuka misingi ya sanaa ya kikanuni (uandishi holela). Kilichosisitizwa hapa ni kuhusu utu binafsi ulioambatana na mawazo ya kimaendeleo ya siasa ya nyakati hizo. Ujumi wake ulijikita zaidi katika mwelekeo wa upokezi wa kazi yenyewe aliyoitunga mtunzi. Hatimaye, kukawa na mlipuko wa mwelekeo tofauti wa kimaudhui na fani kutokana na uhuru aliokuwa nao msanii katika kusana kazi yake ya kisanaa. Hali hii ilipelekea kuzuka kwa maingizo mapya ya utunzi katika sanaa ambayo ni usawiri wa wahusika na maudhui yaliyowahusu walengwa duni katika maisha yao ya kila siku (Senkoro, 1987).

Senkoro (1993) anazungumza vizuri juu ya mtunzi anavyotakiwa kuwa huru katika kueleza jambo lolote atakalo kwa jinsi yeye anavyoona bila ya kupingwa na kipingamizi chochote kile. Katika kipindi hiki msanii alikuwa huru kujieleza na kuieleza jamii yake kadiri ya uwezo wake pasipo kubugudhiwa na mtu yeyote au jamii. Anasema serikali ni chombo cha mabavu. Kwa kuthibitisha hili mwandishi anasema:

> Kila mtu ana uwezo wa kusema kwa uhuru kabisa; na maneno ya kila mtu sharti yasikilizwe hata kama mwazo ya mtu yamepotoka kiasi gani au hayapendwi kiasi gani (*JK. Nyerere, Uhuru na Maendeleo*).

Lengo kuu la mwandishi hapa lilikuwa ni kujadili kuhusu uhuru wa mwandishi katika kusana kazi zake na ndilo lililopelekea mjadala mkubwa hadi sasa kuhusiana na uhuru katika utunzi wa kazi za kisanaa. Jamii iko huru, waandishi wako huru kuandika hisia zao kwa namna waonavyo wao. Lengo lao likiwa ni kuchoshwa na kusema hewala kwa kila kitu na kuanza kuandika kwa kuhakiki mifumo mbalimbali iliyopo katika jamii na kuibua maovu yanayotendwa na viongozi.

4.2.2.3 Uandishi wa Kimsaragambwe

Hizi ni zama ambazo zilitokana na kuwapo kwa zama za kidemokrasia ambazo zilizingatia zaidi uhuru wa mwandishi katika kutunga kazi ya kisanaa. Uandishi katika mkondo huu uliakisi kwa kiasi kikubwa maisha yalivyo katika jamii kwa kuwa maisha sio kitu kinyoofu cha kubaki vile vile kama kilivyo. Kuna kani mbalimbali kama vile za kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kijamii ambazo kwa kiasi kikubwa huchangia katika kuyabadili maisha katika mifumo yake. Kwa maana hiyo, hali hii iliwafanya watunzi wengi wa kazi za kisanaa katika mkondo huu kutunga kwa kadri maisha yalivyo na kufanya kutunzi ni changamani ili kuendana na kasi ya maisha kwa kadri yanavyobadilika katika jamii husika.

Katika mkondo huu ndipo dhana ya umajaribio katika fasihi ya Kiswahili inaibuka kwa wingi na kufanya watunzi wengi wa kazi za kifasihi kuwa huru zaidi katika uandishi wa kazi zao kwa kuingiza vipengele vipya ambavyo havikuzoeleka hapo awali katika fasihi ya Kiswahili. Ndipo hapa sasa katika mkondo huu waandishi wa fasihi mpya wanapotokea kama vile Kezilahabi katika riwaya, Mulokozi katika ushairi na P. Muhando katika tamthiliya lengo likiwa ni kuleta upya katika Fasihi ya Kiswahili (Senkoro, 2011).

Khamisi (2007) anazungumzia kuhusu utunzi wa waandishi baada ya kuamua kuanza kuuzungumzia ukweli wa maisha jinsi yalivyo bila ya kupindisha ukweli huo. Kuhusu suala hili mwandishi anasema:

> Waandishi wengi wa Kenya na Tanzania walipoanza kukataa kuitikia 'hewalla' kwa kila walichokiona na kukisikia. Pia walipokataa kuitikia kanuni na pingamizi za ubunaji na sanaa walizozikuta au walizowekewa. Mwanzoni, njia bora iliyoonekana ingefaa kutumika katika kazi za fasihi ni ile ya uhalisia, kwa sababu ya uwazi na mnyooko wake wa mantiki. Pia kwa sababu uhalisia ni mwelekeo au mtindo uliozoewa sana, si Afrika Mashariki na Afrika nzima tu, bali duniani kote. Ni mbinu iliyoota mizizi imara kwa muda mrefu. Na isitoshe, kwa sababu ya uwazi na kutobabaisha kwake, ilionekana ni njia bora kabisa ya kufichua na kuueleza umma matatizo ya kijamii na kisiasa kinagaubaga. Ilisemekana kwamba ilikuwa njia bora ya kuwasiliana na wananchi, hasa wananchi wa kawaida…Lakini, tokea kuanza kuvuma upepo wa mageuzi, inaonekana kwamba waandishi wamepata mwanya mkubwa zaidi wa uhuru wa kisanaa na kifikra. Sasa midomo mingi inaisemea siasa badala ya mdomo mmoja au michache, ingawa mara nyingi bila ya taathira kubwa. Nadhani dalili za uhuru huo ziko wazi (uk. 12, 13).

Mwandishi hapa anaonesha ni kwa jinsi gani maisha yalivyobadilika na watunzi kupata uhuru wa kuzungumza kwa uwazi na mkemeo wa hali ya juu. Maisha yanabadilika watunzi wanatunga kazi zao kihalisia kulingana na maisha yalivyo katika jamii husika.

4.3 Vionjo vya Kiuandishi katika Riwaya za Shaaban Robert na Said A. Mohamed

Sehemu hii inajadili vionjo hivyo vya kiuandishi katika riwaya za waandishi teule kwa kujigeza kwanza katika muhtasari wa riwaya hizo teule.

4.3.1 a) Muhtasari wa Riwaya za Shaaban Robert

Sehemu hii inatoa muhtasari wa riwaya za Shaaban Robert ambazo ni *Adili na Nduguze* na *Utu Bora Mkulima*. Hii itatusaidia kujua kulandana na kutofautiana katika vionjo vya kiuandishi kwa waandishi hawa teule.

4.3.1.1 Muhtasari wa Riwaya ya *Adili na Nduguze*

Riwaya ya *Adili na Nduguze* ya Shaaban Robert ilichapishwa mnamo mwaka 1952 na Macmillan huko London. Riwaya hii imegawanyika katika sura kumi na tano. Riwaya hii

inamzungumzia mhusika mkuu ambaye ni Mfalme Rai aliyekuwa akiwahimiza watu wake kilipa kodi kwa kutoa mnyama mmoja mmoja kila zizi kwa kila mwaka. Nchi hii ya Ughaibuni ilijaaliwa kuwa na mifugo mingi kama vile ng'ombe, mbuzi, kondoo, farasi na wanyama wengine. Wanyama hawa walizaa mapacha, hii ilionesha jinsi nchi hii ilivyokuwa imejaaliwa. Mfalme anamtuma mhusika Ikbali kwenda kukusanya kodi katika mji wa Janibu. Katika safari yake, Ikbali alifanikiwa kufika katika mji huo na kukutana na madhila mengi waliyokuwa wakiyapata nduguze Adili kwani waligeuzwa kuwa manyani baada ya kumrusha baharini kaka yao. Manyani hayo yalifungiwa katika chumba ambacho Adili alitakiwa kuyachapa manyani hayo kila siku. Mfalme Rai ilimbidi amuite Adili na kumtaka kuelezea yote yaliyotokea kwa kuwa alitoswa majini na nduguze kwa sababu ya wivu na tamaa ya msichana mrembo.

Mwandishi wa riwaya hii amemtumia Adili kijana aliyewapenda nduguze mpaka kufikia kugawana mali zao walizoachiwa na baba yao. Adili aligawa mali hizo theluthi ya mali kwa kila mmojawapo na akagawa tena kwa mara ya pili vivyo hivyo. Riwaya hii ina wahusika kama vile Adili, Mfalme Rai, Ikbali, Mrefu, Mwelekevu, Tukufu, Huria, Hunde, Mjeledi, Kabwera, Kisasi na Enzi.

Lengo kuu la mwandishi katika riwaya hii ni kutaka kuitimiza falsafa yake ya utuwema na siku zote wema huushinda ubaya. Anamchora mhusika Adili akiwa na utu bora; kwani licha ya kupata mateso mengi kutoka kwa ndugu zake, bado Adili alikuwa ni mtu mwenye utu na kuwapenda ndugu zake. Yale yote waliyomtendea aliwasamehe na wakaishi raha mstarehe na ndugu zake. Mwandishi analithibitisha hili kwa kusema:

> …Adili alikuwa si mtu ovyo, alikuwa na moyo mwema, usiokata tamaa, mvumilivu, mwenye huruma, uliotayari kusamehe. Kama nusu ya watu wa duniani wangekuwa na mioyo kama wa Adili nusu ya maisha yao ingetoweka na bila shaka wangeishi maisha ya peponi hapa katika ardhi… (uk. 44).

Si hilo tu lilikuwa lengo la mwandishi, bali pia anakiri yeye mwenyewe ya kuwa:

> Ingawa kitabu hiki hutaja habari za malaika na majini, na viumbe wa ajabu, lakini ni kwa sababu ya utunzi tu. Mambo hasa yaliyotiliwa mkazo ndani yake ni ardhi na mimea yake, machimbo na hazina zake, mifugo na mazao yake, biashara na faida zake, safari na manufaa yake, utajiri na baraka yake, ahali na heshima zao, na ndugu na matendo yao. Mambo haya huhusu watu wengi kama si dunia nzima (Muhtasari wa Shaaban Robert mwenyewe nyuma ya kitabu).

Hivyo basi, riwaya hii kwa kiasi kikubwa inajadili matatizo mazito yanayoikumba nchi kwa jumla yake na kuitaka jamii kuishi kwa umoja na amani kwani ndio chachu ya maendeleo ya jamii husika katika kupata maendeleo ya nchi yao kama Mfale Rai alivyokuwa akiongoza.

4.3.1.2 Muhtasari wa Riwaya ya *Utu Bora Mkulima*

Riwaya ya *Utu Bora Mkulima* ni riwaya iliyochapishwa mwaka 1954 ikichapishwa na Evans Brothers Limited Nairobi. Riwaya hii ina wahusika wakuu na wadogo kama vile Utubora, Radhia, Sheha, Ahmed, Bi Mkubwa, Liwali na Mke wa Liwali. Riwaya inaanza kwa kumzungumzia mhusika mkuu, Utubora ya kuwa anataka kuacha kazi kutokana na maneno ya walimwengu katika jamii yake. Utubora alikuwa ni mchapa kazi na mpenda watu wote wakubwa kwa wadogo. Riwaya inaendelea kuelezea jinsi Utu Bora alivyofanikiwa katika kazi yake aliyokuwa akiifanya na hata akafanikiwa kukutana na Radhia ingawaje wazazi wa Radhia walikuwa wakimkataa Utubora na mwishowe alipambana mpaka mwisho Utubora alifanikiwa kufunga harusi na binti huyu. Kwa jumla, mwandishi wa riwaya hii anaitaka jamii kuwa mpya kwa kuwataka wanajamii kuwa na utu katika maisha kwa kujaliana na kuheshimiana kwani mwandishi anaamini utu ndio msingi katika maisha. Mwandishi Shaaban Robert anafanya hivyo kupitia mhusika Utubora ambaye anamchora kwa sifa za utu, ujasiri, ukweli, uaminifu na ujasiri. Haya yanajidhihirisha kupitia mhusika Utubora:

> …Jambo hili la hasara lilikimbiwa siku zote na utubora hata akawa mtu wa matendo mengi mema. Kwa hivi, baada ya siku chache tu nyumba nzuri ya matofali ya kuchoma, paa la vigae, milango ya nakshi, madirisha makubwa, na sakafu ya seruji ilizuka kama uyoga juu ya kiwanja alichochagua kule Busutamu… (uk. 20).

Hivyo, katika dondoo hii, Shaaban Robert anamsawiri Utubora kama mhusika mwenye sifa nyingi njema zinazotakiwa kuenziwa na kutukuzwa na wanajamii wote ili kuwa na jamii yenye utu katika maisha. Utubora kwa kiasi kikubwa amelisadifu jina lake kwa kuwa alikuwa ni mtu ambaye kweli anawakilisha utu wema katika jamii na kwa kweli alipendwa na wanajamii wote kutokana na matendo yake mema aliyokuwa anayatenda. Si hivyo tu mwandishi anazungumzia suala la uongozi, uchapa kazi, hasara za ulevi, umuhimu wa kilimo katika jamii ya sasa kama ndio uti wa mgongo, dini, mapenzi na matabaka vyote hivi vimezungumziwa katika riwaya hii.

4.3.1 b) Muhtasari wa Riwaya za Said A. Mohamed

Sehemu hii imepitia muhtasari wa riwaya za Said A. Mohamed ambazo ni *Babu Alipofufuka* na *Utengano*. Lengo likiwa ni kulinganisha na kulinganua vionjo vya kiuandishi kwa waandishi hawa.

4.3.1.1 Muhtaari wa Riwaya ya *Babu Alipofufuka*

Babu Alipofufuka ni riwaya iliyotungwa na mwandishi Said A. Mohamed na kuchapishwa mnamo mwaka 2001 na Jomo Kenyatta Foundation Nairobi. *Babu Alipofufuka* ni hadithi inayosimulia juu ya K, kiongozi wa serikali aliyerithi madaraka baada ya kuondoka wengine. Katika riwaya hii, K anaandamwa na mzimu wa Babu yake aliyekufa zamani. Mzimu huu unasikiwa na K pekee yake. Mzimu unamlaumu K kwa kuiga mfumo wa maisha ambao umejaa ufisadi, usaliti, ubadhirifu, ubinafsi na kutojali. Pia, mzimu unamlaumu K kwa kuiga mambo ya kigeni yanayoletwa na mfumo wa utandawazi na kuhimiza utunzaji wa asili ya kitaifa. K anaandamwa mara kwa mara na mzimu wa Babu yake, ambao unamfanya K kupoteza fahamu na kuchukuliwa safarini na mzimu huo.

Anashuhudia hali yake ya utoto alipokuwa mtumwa wa Waarabu waliokuwa wanamiliki sehemu kubwa ya kisiwa cha Zanzibar, anashuhudia ujana wake na hatimaye nyakati za uongozi wake.

Baada ya safari hiyo, K anakabiliwa na hukumu. Anapatikana na hatia ya yote aliyoyafanya, na analazimika kuapa kwa jadi ya Kimasai na Kikamba. K anaporudi katika maisha yake ya kawaida, anafukuzwa kazi na kurejeshwa kijijini akiwa amekata tamaa. *Babu Alipofufuka* ni riwaya inayoangalia nyuma nyakati za historia zilizopita za nchi zinazoendelea, hususani za Kiafrika na kuweka wazi matatizo ya uongozi baada ya ukoloni na athari za utandawazi unaoongozwa na Marekani katika nchi zinazoendelea.

Riwaya ya *Babu Alipofufuka* imejaa msamiati ambao unamfanya mwandishi aweke sherehe ya ufafanuzi wa maneno mbalimbali yaliyotumika. Athari za utandawazi katika uchumi na utamaduni wa Mwafrika zimetapakaa katika riwaya hii. Lengo la mwandishi katika riwaya hii ni kuonesha athari za ubeberu na utandawazi katika nchi zinazoendelea. Mwandishi anazungumza juu ya utandawazi, kuwa ni mbinu nyingine mpya inayotumiwa na mataifa ya kibepari kuendelea kutawala nchi zinazoendelea kiuchumi, kisiasa, kijamii, kiutamaduni na kifikira. Mbinu hii inawezesha mataifa ya ulimwengu wa kwanza kuendelea kujipatia mahitaji ya viwanda vyao kama vile, malighafi, masoko kwa ajili ya bidhaa zao, maeneo ya uwekezaji na nguvu kazi rahisi ya uzalishaji. Kwa mfano, mwandishi anasema:

> Utamaduni mpya aliufwatia huko. Utamaduni ulioambatana na ufunguzi wa milango katika kila kitu. Hata heshima na utu wake au ile heshima ya nafsi yake isiyo nafsi tena. Na hayo si mafanikio madogo kwake (Uk. 10).

Mwandishi anazungumzia mambo mengine yanayoikumba jamii. Mambo hayo ni pamoja na athari za uchumi wa Soko huria, athari za uwekezaji katika nchi zinazoendelea, uporaji wa ardhi na umilikishaji kwa wageni, uongozi mbaya, kukwepa kodi kwa lengo la

kujilimbikizia mali, athari za utandawazi katika utamaduni na nafasi ya mwanamke katika jamii. Yote haya yanazungumziwa katika riwaya hii na kukemewa vikali.

4.3.1.2 Muhtasari wa Riwaya ya *Utengano*

Riwaya ya *Utengano* imetungwa na Said A. Mohamed na kuchapishwa mnamo mwaka 1980 na Longhorn Publisher. Riwaya hii ina wahusika kama vile Bwana Maksuudi, Kazija, Bi Farashuu, Maimuna, Mussa, Mama Jane, Bi Tamia, Bi Kocho, Dora, Denge, Bi Sururu, Shoka na Kabi. Riwaya inamzungumzia mhusika Bwana Maksuudi akiwa na familia yake huku akiwa na watoto wawili na mkewe; wakati huo, akiwa na mwanamke mwingine wa nje ambaye anamahusiano na mwanaye Mussa. Bwana Maksuudi anawakataza mkewe na mtoto wake wa kike hata kutoka nje ya nyumba yao, akiwataka kukaa ndani muda wote kiasi kwamba hata mkewe akitaka kujifungua haruhusiwi kwenda katika hospitali, bali hutakiwa kujifungulia tu nyumbani.

Kwa upande wake, Maimuna anashawishiwa na Bi Kocho ambaye alikuwa mtumishi wao aachane na utawa huo na kutafuta maisha ya uhuru. Baada ya kufanya hivyo, Maimuna anatoroka nyumbani kwao; na hapo ndipo utengano unapoanza katika familia hiyo. Jambo hili linasababisha Maimuna kupata shida za dunia hadi kufikia hatua ya kuuza mwili wake. Bwana Maksuudi, kiongozi mkubwa wa nchi, anayatumia madaraka yake vibaya kwa kujilimbikizia mali kwa maslahi yake na kusahau wananchi ambao walimchagua akawafanyie kazi. Mwisho wa riwaya, Bwana Maksuudi anaonekana akishushwa cheo kwa ubadhilifu aliokuwa akiufanya katika serikali yake. Wananchi wanaonekana kumkataa akiwa anaomba kura ili awaongoze tena. Mwandishi amezungumzia matatizo mbalimbali katika jamii yake kama vile uongozi mbaya, mapenzi, ubadhilifu wa mali, nafasi ya mwanamke katika jamii, ulaghai na hata kukemia mifumo ya kiuchumi iliyoko katika jamii. Msanii anaitaka jamii kuachana na tabia za

watu kama akina Maksuudi katika jamii hii ya sasa tuliyonayo kwani madhara yake ni makubwa sana. Haya yanajidhihirisha pale anaposema:

> …Muda si muda Maksuudi na Zanga walikuwa wakiongozwa na polisi huku wametiwa pingu. Huku nyuma, wananchi walimbeba Siwa wakaenda naye kwa shangwe Siwa, Siwa, Siwa… Njiani mazungumzo yalikuwa ya mwanamke Kazija aliyekuwa na ujasiri kuliko wanaume. Yeye ndiye aliyethubutu leo kumpa ukweli kiongozi (uk. 82).

Nukuu hii inatuangazia ni kwa jinsi gani wananchi walivyochoka kunyanyaswa na kuonewa na viongozi ambao wanajinufaisha wao wenyewe kwa maslahi yao bila kujali wananchi wao. Viongozi ndio wamepewa dhamana ya kuongoza nchi na wameaminiwa na wananchi, lakini bado wanawanyanyasa wananchi huku wanarudi tena kuomba kura kwa hao hao wananchi. Hali kama hii inakatisha tama kwa wananchi kiasi kwamba kiongozi anapoenda kuomba tena kura anafukuzwa kwa kuwa hawana imani naye tena kama alivyofukuzwa bwana Maksuudi.

4.3.2 Vionjo vya Kiuandishi katika Riwaya ya Kiswahili

Vionjo vya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili vimegawanyika katika makundi mawili. Ambayo ni vionjo vya riwaya za awali na vionjo vya riwaya za sasa. Vionjo hivi vinajitokeza kifani na kimaudhui katika riwaya hizo. Sababu kubwa ya kuanza kujadili vionjo hivi ni kumuonesha msomaji vionjo hivyo kwa ujumla vinavyojitokeza katika riwaya za awali na riwaya za sasa. Kwa maana hiyo, sio vionjo vyote vinajitokeza katika riwaya teule ndiyo maana vikajadiliwa vyote na baadaye kuvionesha kama jinsi vinavyojitokeza katika riwaya hizo teule. Vionjo hivyo ni kama ifuatavyo:

4.3.2 a) Vionjo vya Kiuandishi katika Riwaya za Awali

Riwaya ya Kiswahili ya awali ina vionjo vyake vya kiuandishi ikitofautishwa na riwaya ya sasa. Vionjo hivi kwa namna moja au nyingine ndivyo hutawala katika riwaya husika. Waandishi na watunzi takribani wengi hutumia vionjo hivi. Vionjo hivyo ni kama vifuatavyo:

4.3.2.1 Usimulizi wa Kimaonyo na Maadili

Suala la maadili lilikuwa nyeti sana kipindi hicho. Ndiyo maana watunzi wa hapo awali wa riwaya ya Kiswahili walijigeza kutoa simulizi zilizo na maonyo na maadili katika jamii. Kila mzazi na mlezi alipenda kuona mtoto wake akikua katika maadili. Kuna tofauti mkubwa kati ya watunzi wa awali na wa sasa. Utunzi wa riwaya za awali ulitamalakiwa kwa kiasi kikubwa na simulizi zilizolenga kuleta maadili katika jamii yoyote ile. Mtunzi husisitiza utuwema katika jamii akiamini ndio msingi wa maisha. Bila ya utuwema katika jamii ni sawa na kazi bure. Anaiasa jamii kupendana, kujaliana na kuheshimiana ili ujenzi wa jamii mpya upatikane haraka kutokana na kushirikiana vyema katika jamii. Ndiyo maana watunzi wa riwaya hizo wamejikita zaidi katika maadili hasa ya utuwema katika jamii kwani ndio chachu ya maendeleo.

4.3.2.2 Matumizi ya Wahusika Bapa

Senkoro (2011) anatoa maana ya wahusika kuwa ni watu, ama viumbe waliokusudiwa wawakilishe dhana, mawazo au tabia za watu, katika kazi ya Fasihi. Hivyo, wahusika ni viumbe ama watu waliobebeshwa uhusika wa watu halisi katika jamii. Wahusika bapa ni aina ya wahusika ambao hawabadiliki kitabia na kimatendo. Kwa kuwa lengo la watunzi wa wakati huo lilikuwa kuonesha suala la maadili katika jamii ndiyo maana walitumia wahusika wa aina hii. Watunzi wa riwaya za awali walitumia wahusika ambao ni bapa na hawakubadilika hata kidogo. Kama atakuwa mwema basi atakuwa hivyo mpaka mwisho wa riwaya. Na akiwa ni mwovu basi atakuwa hivyo mpaka mwisho wa riwaya. Sababu ya utumizi wa wahusika wa aina hii ni kutokana na kuonesha maadili ambayo hubebeshwa wahusika hao ili waonekane wenye tabia ya kuigwa katika jamii.

4.3.2.3 Matumizi Makubwa ya Nduni za Fasihi Simulizi

Fasihi Simulizi ni aina ya Fasihi ambayo hutolewa kwa njia ya mdomo. Fasihi hii imetoa mchango mkubwa sana katika Fasihi Andishi. Baadhi ya waandishi wa riwaya za

mwanzoni hutumia nduni za Fasihi Simulizi kama vile safari, ujini, wahusika wanyama, usihiri na utanzia katika kusana kazi za kifasihi. Ikumbukwe kwamba, wakati huo Fasihi Andishi ilikuwa bado haijakomaa kiasi cha kutosha ndio, maana hata watunzi nao wakajigeza kutumia mbinu hizi za Fasihi Simulizi kwa sababu tu ilikuwa imeshafahamika na kuzoeleka katika maisha ya kila siku. Mathalani, katika usimulizi wa hadithi ambayo ni Fasihi Simulizi msimulizi hutumia matukio ya ajabu pamoja na safari nyingi katika usimulizi wa hadithi yake. Humo ndani mhusika atakutana na matukio ya kitanzia na hata ya kufurahisha lengo likiwa ni kufikisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa. Hivyo basi, mbinu hii nayo hutumika katika kutunga riwaya za awali ambayo ni kionjo cha uandishi kwa riwaya hizo.

4.3.2.3 Mianzo na Miisho ya Kifomyula

Riwaya hizi zilikuwa na kanuni maalumu ya kuanza na kuisha katika usimulizi wake. Kuna tofauti kubwa baina ya riwaya za mwanzo na za sasa. Zile za mwanzo ziliakisi kwa kiasi kikubwa mianzo na miisho ya nathari simulizi. Mianzo na miishi hiyo twaweza kusema ilichukua matumizi ya vifungu vya kifomyula. Dhana ya vifungu vya kifomyula hapa yamaanisha utumizi wa neno, tungo, au aya kwa namna ya kuirudiarudia katika kazi moja au miongoni mwa waandishi tofauti.

Mathalani, kulikuwa na matumizi ya vifungu kama vile hapo zamani za kale, palikuwa na… Paukwa… pakawa… Hadithi… hadithi … na hadithi yangu yaishia hapo… Waliishi raha mustarehe… Hatimaye alifanikiwa sana. Kuhusu miisho, ingawa wanariwaya waliowafuatia wale wa awali wamejikwepesha na miisho ya kifomyula; bado miisho yao inalandana kimaudhui. Hii ni kwa sababu, kwa jicho la jumla, riwaya nyingi bado zinamalizika kwa namna ya kuonesha mafanikio. Mafanikio hayo ni yale yatokanayo na mivutano baina ya ama uwi na wema au ukale na usasa.

4.3.2 b) Vionjo vya Kiuandishi katika Riwaya za Sasa

Kuna tofauti kubwa ya vionjo vya kiuandishi kati ya riwaya za awali na riwaya za sasa. Tofauti hizo ndizo zinazoleta vionjo vya kuandishi katika riwaya hizo. Vionjo hivyo vya kiandishi katika riwaya za sasa ni kama ifuatavyo:

4.3.2.1 Matumizi ya Wahusika wa Ajabu

Matumizi ya wahusika wa ajabu hutokea katika usawiri wa majina yao na matendo yao. Riwaya za sasa hutumia kionjo hiki kifani ili kuusawiri ulimwengu kwa njia ya kiuajabu, lengo likiwa ni kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Mtunzi huteua majina ambayo yamebeba vionjo vya kimaajabu na matukio ya kimaajabu ili kuonesha ubunifu wake katika riwaya husika. Mbinu hii kwa sasa ndio imeshika hatamu kwa watunzi wa riwaya za sasa kama uhalisiaajabu. Mbinu hii husaidia kuelezea maisha kwa kina na kwa namna ya uajabu kiasi kwamba hata mtu anaposoma huona kama riwaya hizo ni ngumu kueleweka. Hii ni kwa sababu ya matumizi ya wahusika wa ajabu na matendo yao katika riwaya hizo. Wahusika wa ajabu wanaweza wakawa mazimwi, mashetani na mizuka ya ajabu.

4.3.2.2 Matumizi ya Mazingaombwe

Neno mazingaombwe limefasiliwa katika *Kamusi la Kiswahili Fasaha* (2010) likinukuliwa na Faustine (2012) kuwa ni ujanja wa kumdanganya mtu ili aone jambo au kitu ambacho sivyo vile kilivyokuwa mwanzo. Kwa maana nyingine, mazingaombwe hujulikana kama kiinimacho au uhalisiamazingaombwe. Katika riwaya ya Kiswahili, mazingaombwe hutokea pale ambapo matukio hutokea katika hali ambayo siyo ya kawaida. Mbinu hii ni mwendelezo wa mbinu zilizotumika katika riwaya za awali. Hata hivyo, kwa sasa mbinu hii imeshika hatamu katika kuelezea maisha ya jamii zetu. Watunzi wengi wa sasa hutumia mbinu hii kama uhalisiamazingaombwe ambao humaanisha mtindo au aina ya Fasihi, ambamo mazingaombwe, uchawi au mambo

ambayo hayafanani na ya kawaida yaliyozoeleka kwa hadhira hutokea sambamba na yale ambayo ni ya kawaida. Pia, mambo hayo hutokea katika mandhari au mazingira ambayo kwa kiasi kikubwa sana yana uhalisi tunaoujua katika jamii halisi.

4.3.2.3 Dhana ya Mapenzi na Ngono

Mapenzi na ngono ni miongoni mwa kionjo cha uandishi katika riwaya za sasa. Riwaya hizi, zinaakisi dhana ya mapenzi na ngono kwa uwazi zaidi ikilinganishwa na riwaya za awali. Yaani, riwaya za awali zilikuwa zikizungumzia mapenzi kwa uficho kiasi kwamba hata mtu kugundua ni mapenzi yanayozungumziwa ilikuwa ni vigumu katika riwaya hizo. Tukirudi katika riwaya za sasa, mapenzi yanachukuliwa au yanazungumzwa kama kitu cha kawaida, ndiyo maana yanajadiliwa kwa uwazi zaidi. Sababu kubwa ni kutokana na utandawazi unaotufanya kuchukulia dhana hizi kama kitu cha kawaida tu katika jamii zetu. Viashiria vya mapenzi na ngono ni kama uchi au utupu ambavyo hudhihirika waziwazi katika riwaya husika.

4.3.2.4 Matumizi ya Nyenzo za Kisayansi na Teknolojia

Nyenzo za kisayansi na teknolojia zinajumuisha matumizi kama vile ya baruapepe, kompyuta na simu. Matumizi haya yanajitokeza zaidi katika riwaya za sasa kwa sababu, hiki ni kipindi ambacho maendeleo ya sayansi na teknolojia yameshika hatamu ulimwenguni. Jamii imeshuhudia mabadiliko makubwa sana ya kimaisha yanayosababishwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Kwa kufanya hivi, watunzi nao hawakuweza kukwepa kutumia kionjo hiki kwa sababu wanatunga kazi zao katika karne ya maendeleo ya sayansi na teknolojia. Hali hii inaleta tofautu kubwa kati ya utunzi wa riwaya za sasa na riwaya za awali.

4.3.2.5 Kuyajadili Maisha kwa Kina

Riwaya za sasa kwa kiasi kikubwa zinayajadili maisha kwa kina kulingana na hali halisi ya maisha jinsi ilivyo. Riwaya hizi zinachambua matatizo mbalimbali yaliyopo katika

jamii huku zikionesha suluhisho la matatizo hayo. Kwa kuwa riwaya ni usawiri wa maisha ya kila siku jinsi yalivyo na watunzi nao hutunga kwa kuangalia maovu mbalimbali yaliyopo katika jamii. Riwaya hizi huvuka mipaka ya kinchi na hata kujadili matatizo yanayozikumba nchi nyingine. Nchi nyingi zinakabiliwa na matatizo kadha wa kadha hivyo, ni jukumu la mtunzi kujadili matatizo hayo kwa kuwa ndio maisha halisi ya kila siku.

4.3.2.6 Matumizi ya Ndoto

Ndoto ni mfuatano wa picha, mawazo, hisia au mihemuko ya muda mfupi inayoambatana na mizunguko ya macho, ambapo hutokea bila hiyari kwenye akili za mtu aliye usingizini. Kwa maana hiyo, ndoto ni kama njozi au maono. Riwaya nyingi za sasa hutumia matumizi ya ndoto ikitofautishwa na riwaya za awali. Matumizi ya ndoto hizi ni kubashiri yajayo katika maisha yetu. Ndoto hizi huambatana na maudhui fulani katika kazi husika. Ndoto hizo hujengwa katika masimulizi ambayo husimuliwa na mtunzi kindoto.

4.3.2.7 Dhima na Nguvu ya Asasi za Dini

Ni miongoni mwa kionjo cha uandishi katika riwaya za sasa. Dini inadhima kubwa katika jamii hasa kuwataka watu kutenda yanayotakiwa kwa misingi ya dini. Kionjo hiki kinatufafanulia namna ambavyo suala la dini lilivyo na nafasi kubwa katika jamii zetu kiasi kwamba dini hizi hutumika katika kuficha maovu. Watu hutumia dini kama mwavuli wa kujikinga ili kufanya mambo yaliyo kinyume na dini. Riwaya za sasa hutumia kionjo hiki ili kufufua maovu yafichwayo kwa kutumia dini katika jamii zilizo nyingi. Binadamu wamegeuka kuwa wanyama, wako radhi hata kutumia suala la Mungu ili kufanikisha malengo yao.

4.3.3 Vionjo vya Uandishi katika Riwaya Teule

Kila mwandishi wa riwaya hupenda kutumia vionjo fulani katika uandishi wake. Vionjo hivyo mara nyingi ndivyo husaidia katika kutambulisha waandishi tofauti tofauti. Vionjo hivyo huwa ni vya kimaudhui na kifani. Vifuatavyo ni vionjo vya kiuandishi katika riwaya husiku.

4.3.3.1 Vionjo vya Kiuandishi katika Riwaya ya *Adili na Nduguze*

Riwaya ya *Adili na Nduguze* kwa kiasi kikubwa imesanwa kwa kufuata vionjo vya kiuandishi vya awali. Riwaya hii ya awali imetamalakiwa na vionjo vifuatavyo:

4.3.3.1.1 Usimulizi wa Kimaonyo na Maadili

Muda wote wa uhai wake Shaaban Robert alisisitiza walimwengu kuwa na maadili mazuri. Kwa kiasi kikubwa riwaya hii imejengwa katika misitizo wa utuwema katika jamii. Mwandishi anaamini kuwa utuwema katika jamii ndio msingi wa maisha na kupata maendeleo. Kulithibitisha hili mwandishi anamtumia muhusika Adili akiwa na utu na upendo kwa nduguze na jamii kwa jumla. Anasema:

> Adili alikuwa si mtu ovyo, alikuwa na moyo mwema, usiokata tamaa, mvumilivu, mwenye huruma, uliotayari kusamehe. Kama nusu ya watu wa duniani wangekuwa na mioyo kama wa Adili nusu ya maisha yao ingetoweka na bila shaka wangeishi maisha ya peponi hapa katika ardhi… (uk. 44).

Pia, usimulizi wa kimaadili hasa utuwema unapatikana katika riwaya hii kupitia mfalme Rai. Alikuwa ni kiongozi aliye na utu wa kujali wanajamii wenzake, mkubwa kwa mdogo katika uongozi wake. Ni kiongozi aliyejawa na maadili mema ya kuongoza vyema katika nchi yake ili kupata jamii mpya yenye maendeleo.

> Rai, mfalme wa Ughaibu, alikuwa mfalme namna ya peke yake duniani. Alikuwa na tabia iliyohitilafiana kabisa na tabia za utu duniani. Tabia yake ilijigawa katika theluthi tatu mbalimbali kama rangi ya ngozi ya punda milia… Rai alikuwa kiongozi mwadilifu na mfalme mwema sana. Hakusita kufanya kazi ndogo wala kubwa kwa mikono yake mwenyewe. Kazi nyingi za ufalme alizitenda yeye mwenyewe (uk.1, 2).

Hapa mwandishi ameonesha jinsi matendo mema yanavyowafanya wanajamii waweze kuishi kwa amani katika jamii zao. Pia, hakuacha kuonesha faida mbalimbali zinazopatikana katika jamii kunapokuwa na uongozi mzuri kama uongozi wa Mfalme Rai. Faida za uongozi bora ni kama vile kuondokana na umasikini, matabaka na unyanyasaji.

4.3.3.1.2 Matumizi ya Nduni ya Fasihi Simulizi

Matumizi ya nduni hii katika riwaya hii yanajitokeza zaidi katika utumizi wa wahusika wanyama na matukio ya kuogofya ya mwanamke kugeuka kuwa tandu. Fasihi Simulizi ndio hutumia nduni hii katika kusimulia. Waandishi wa riwaya za awali walitumia mbinu hii kama kionjo kimojawapo cha uandishi katika riwaya zao. Riwaya hii ya *Adili na Nduguze* inalithibitisha hili kwa kusema:

> …Sasa manyani yalichukuliwa mezani kula chakula kwa vijiko na nyuma. Yaliposhiba yalinyweshwa maji. Midomo yao ilifutwa kwa leso za Hariri. Kisha yalifungwa minyororo kama yalivyokuwa. Mambo haya yalipotendeka Ikbali alikuwa amesimama kimya anachungulia. Adili alikusanya vyombo ili atoke nje, Ikbali alitangulia kuondoka mlangoni… Manyani yalipomuona mfalme yalifanya ishara mbili. Kwanza yaliinua juu mikono yao kama yalivyokuwa yakiomba, pili yalilialia kama yalivyodhulumiwa. Ishara ya kwanza ilionyesha ombi la msaada, na ile ya pili ilionyesha mashtaka… Adili aliyageukia manyani akauliza kama yaliyosemwa yalitokea au hayakutokea. Manyani yaliziba nyuso kwa viganja vya mikono yao kwa aibu (uk. 6, 9, 19).

Vilevile, nduni nyingine ya Fasihi Simulizi iliyotumika ni usihiri. Usihiri huu unajitokeza pale ambapo msichana aligeuka akawa tandu na msichana kugeuka kuwa tuta la mchanga. Katika ulimwengu halisi mtu hawezi kugeuka kuwa tandu au tuta la mchanga ni katika usihiri tu ambao hujumuisha uchawi ndani yake. Mwandishi anasema:

> …Adili alipanda juu ya jabali. Huko aliona tandu linakimbia. Rangi yake ilipendeza sana. Iling'ara kama kioo. Nyuma yake lilifuatwa na nyoka aliyetisha kabisa. Nyoka alipolifikia aliliuma kichwani… Ghafula tandu lilijigeuza mwanadamu, yaani msichana mzuri. Uso wake ulivuta macho ya Adili kwa haiba yake kubwa… Baada ya hapo msichana alielekeza kidole chake cha shahada chini. Mara moja ardhi ilipasuka akaingia ndani yake. Alipokwisha jitia ndani ardhi ilijifunga sawia. Msichana hakuonekana tena. Adili alifahamu hakuwa msichana ila jinni… (uk.17-18).

Riwaya hii imetumia nduni ya usihiri au uchawi kwa kuonesha jinsi tandu anavyojigeuza na kuwa msichana. Fasihi Simulizi ndiyo iliyokuwa ikitumia nduni hii hasa. Safari nazo zimetumika katika riwaya hii ambapo wahusika walisafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa lengo la ukombozi. Kwa mfano, safari ya akina Adili na wenzake. Mwandishi anasema:

> Adili alisumbuka safarini kwa sababu ilikuwa mara yake ya kwanza kusafiri baharini. Baada ya safari ya siku tatu walifika bandarini… Waliondoka pale wakaenda mji wa pili… Baada ya safari ya siku moja walifika jabalini. Nahodha aliamuru kutua tanga na kutia nanga… (uk. 17).

Katika nukuu hii mtunzi anaonesha safari za mhusika Adili na wenzake. Safari hizi zilikuwa zinafanyika kwa lengo la kutafuta ukombozi katika jamii husika. Watunzi wengi wa riwaya za awali hasa Shaaban Robert ameitumia mbinu hii ya nduni za kifasihi Simulizi katika kazi zake. Mfano mwingine ni kupitia riwaya zake za *Kusadikika* na *Kufikirika*.

4.3.3.1.3 Matumizi ya Wahusika Bapa

Riwaya hii imetumia wahusika ambao ni bapa. Wahusika wake hawabadiliki hata kidogo katika kuendelezwa au kukua. Mwandishi ametumia wahusika bapa kama vile Adili na mfalme Rai ambao walikuwa ni wema tangu mwanzo wa riwaya hadi mwisho wa riwaya bila ya kubadilika. Pia, amewatumia wahusika Hasidi na Mwivu kama wahusika waovu tangu mwanzo wa riwaya hadi mwisho wa riwaya. Lengo la mwandishi ni kuonesha falsafa yake ya wema hushinda ubaya siku zote. Kionjo hiki kwa kiasi kikubwa kimetumika katika riwaya hii.

4.3.3.2 Vionjo vya Kiuandishi katika Riwaya ya *Utubora Mkulima*

Utubora Mkulima ni riwaya iliyojigeza katika vionjo vya kiuandishi vya riwaya ya awali. Mwandishi Shaaban Robert ametumia vionjo mbalimbali vya kiuandishi katika riwaya yake vinavyomtambulisha kama mwandishi wa zama za awali za kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili. Vionjo hivyo ni:

4.3.3.2.1 Usimulizi wa Kimaadili na Maonyo

Maadili ndiyo ilikuwa nguzo au silaha kubwa ya mwandishi Shaaban Robert. Muda wote wa uhai wake Shaaban Robert alisisitiza jamii kuwa na maadili mazuri. Takriban ni kazi zake zote zimezungumzia suala la maadili kama ilivyo katika riwaya ya *Utubora Mkulima*. Mhusika Utubora anajitokeza kama kiwakilishi cha mtu mwenye maadili kwani alipendwa na kudhaminiwa na watu wote. Aliwapenda na kuwaheshimu wakubwa kwa wadogo ndiyo maana sifa zake zilivuma duniani kote. Twamwona Utubora akifanikiwa sana kutokana na utuwema wake ung'arishwao na maadili mema katika jamii yake. Kwa mfano mwandishi anasema:

> Hapana mwanaume mbaya kwa wanawake wote; wala mwanamke mzuri kwa wanaume wote. Ukikosa huyu, utapata yule. Hii ilikuwa ndiyo desturi ya kijana huyu ya kuangalia na kupima mambo siku zote, na kwa desturi hii aliweza kushinda taabu nyingi sana katika maisha yake ya kila siku…Jambo hili la hasara lilikimbiwa siku zote na Utubora hata akawa mtu wa matendo mengi mema… kwa kweli alikuwa na moyo kama wa malaika ambao hupendezwa na kila kitu (uk. 11, 20, 35).

Mwandishi wa riwaya hii anaitaka jamii kuwa mpya. Hasa wanajamii kuwa na utu katika maisha na kujaliana na kuheshimiana. Mwandishi Shaaban Robert anafanya hivyo kupitia mhusika Utubora ambaye anamchora kwa sifa za utu, ujasiri, ukweli na uaminifu. Riwaya za awali zilisistiza sana maadili katika jamii ndiyo maana na mwandishi huyu akatumia kionjo hiki cha uandishi katika utunzi wake. Pia, suala hili linajidhihirisha anaposema:

> … Alipenda sana kusaidia mtu ye yote aliyekuwa na adili na uaminifu… Mimi nafikiri kuwa kuishi bila kujali mashaka ya watu wengine si maisha kamili… Tabia ya Utubora ilivutia watu wengi waliokutana naye, ingawa yeye mwenyewe alikuwa haujui mvuto aliokuwa nao. Baadhi ya watu walipendezwa tu na Utubora bila kujua sababu, lakini wengine waliona uanadamu uliokamilika kwa mtu huyu… (uk. 22, 28, 42, 43).

Haya yanatudhihirishia kuwa riwaya hii imesanwa kwa kuzingatia kionjo hiki cha maadili kwani mhusika Utubora anajitokeza kuwakilisha maadili hayo. Mhusika huyu ana tabia nyingi zinazofaa kuigwa katika jamii. Shaaban Robert anasisitiza sana utuwema miongoni mwa wanajimii kama Utubora alivyokuwa.

4.3.3.2.2 Matumizi ya Wahusika Bapa

Wahusika bapa katika kazi za kifasihi ni wahusika wasiobadilika kitabia na hawakui wala kuendelezwa. Senkoro (2011) anasema wahusika wengi wa kazi za Shaaban Robert, hasa wa riwaya zake, ni wahusika bapa kutokana na uhusiano wao wa kingano uwafanyao wema wawe wema hivyo hivyo, tangu mwanzo hadi mwisho, na wabaya wabaki kuwa wabaya tangu alfa hadi omega. Riwaya hii ya *Utubora Mkulima* imetumia mbinu hii ya wahusika bapa kupitia mhusika wake Utubora. Mhusika huyu amepewa uhusika bapa kwani ni mwema tangu mwanzo wa riwaya hadi mwisho wa riwaya. Utubora hajabadilika kitabia wala kukua na kupevuka kitabia. Mhusika huyu amekutana na changamoto nyingi za kimazingira zinazomzunguka lakini hakubadilika na kuwa mwovu. Lengo la mwandishi ni kuonyesha falasafa yake ya wema siku zote hushinda ubaya.

4.3.3.2.3 Matumizi ya Nduni za Fasihi Simulizi

Mtunzi katika riwaya hii ametumia nduni hizo kama kionjo cha uandishi katika riwaya za awali. Kionjo hiki kinajitokeza pale mtunzi anapotumia ufutuhi pamoja na wahusika wanyama katika riwaya yake. Mwandishi anasema:

> …Sauti za ndege na minyororo ya ng'ombe sivyo vitu vilivyoko mrima tu. Kuna ngurumo za samba na mivumo ya chui vilevile ambayo hutishia pengine… (uk.3).

Nduni hii ilikuwa ikitumika katika Fasihi Simulizi ambapo msimulizi alikuwa akisimulia mathalani ni hadithi hutumia wahusika wa aina hii pamoja na ufutuhi ndani yake. Waandishi nao hawana budi kutumia kionjo hiki katika utunzi wao kwa sababu Fasihi Simulizi imetoa mchango mkubwa katika Fasihi Andishi.

4.3.3.3 Vionjo vya Kiuandishi katika Riwaya ya *Babu Alipofufuka*

Mwandishi wa riwaya hii ya *Babu Alipofufuka* ametumia vionjo mbalilmbali vya kiuandishi ili kufika ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Vionjo hivyo ni kama vifuatavyo:

4.3.3.3.1 Umazingaombwe

Riwaya hii imetumia mbinu ya uhalisia mazingaombwe kwa kiasi kikubwa. Kuanzia jinsi visa vilivyosanwa na mambo mengi yanatokea kiajabu ajabu na usimulizi wake ni kiajabu ajabu. Jina lenyewe la riwaya *Babu Alipofufuka* linaonesha uhalisiamazingaombwae kwani haiwezekani mtu akafa halafu akafufuka tena katika ulimwengu halisi. Pia, umazingaombwe mwingine unajitokeza pale ambapo sahani ya chakula cha mbwa wa K inatoweka kimiujiza bila ya kujulikana nani anayekula na kuondoa chakula ghafla. Mwandishi anasema:

> …K aliposikia jibwa lake Doggy likinung'unika njaa, alipandwa na hamaki. Mara hii nini tena? Nani anamcheza shere? Mwezi mzima kwa hakika kazi ni hiyo hiyo. Weka sahani za vyakula, sahani toweka… Weka sahani, sahani ondoka… Nani angeshukiwa kama si watumishi? Kwa hiyo, fukuza mtumishi mmoja ingiza mwengine mlolongo mrefu us'o kikomo… Dakika moja sahani ipo, kufumba na kufumbua haipo!...
> "I wapi sahani?"
> "Si hii hapa bwana…!" Biye bila shaka kaemewa. "Niliza… nilizani… umeshaiona."
> "Nilizani… nilizani… mimi nataka ukweli sitaki dhana na uzushi mtupu… sahani iko wapi?... chakula cha Doggy kiko wapi?... (uk. 5, 6).

Vilevile, umazingaombwe bado unaendelea kutumika katika riwaya hii kwani mwandishi amemchora muhusika K akigusa mbingu bila mbawa (uk. 11) na muhusika Proteus amechorwa kwamba anaweza kujigeuzageuza tu na anaweza kuwa mti badala ya bahari

ya Hindi (uk. 11). Kwa jumla riwaya hii umazingaombwe upo na umetumika mwingi sana kama K kutokewa na babu yake katika gari yake na kufanya mazungumzo. Mbinu hii ya umazingaombwe hutumiwa na waandishi wa zama hizi kwa lengo la kufikisha ujumbe kwa jamii kuhusiana na matatizo mbalimbali yanayoikumba jamii. Matukio ya kimazingaombwe bado yanaendelea kutokea katika kasri ya K mwandishi anasema:

> …Kitendawili cha sahani za vyakula vya doggy; tabia mbaya ya kutibukwa na tumbo wakati usiofaa, kutokwa na harufu mbaya kinywani… Na siku hizi hali hiyo humjia kila anapokuwa na wasiwasi au hamaki. Kile kicheko ambacho kwa mara ya mwanzo amekisikia leo, kina sauti iliyofanana na yake mwenyewe. Kicheko asikojua kilikotokea. Je anajicheka mwenyewe nafsi yake ina nini leo? Wakati huu Biye alikuwa ameshafika mlangoni, na mara alihujumiwa na harufu ile kali ya karaha. Alifanya pua yake na kuemewa kama anachofikiri kweli kinatokea. Huwaje mtu mzima kufanya mambo ya kinyandu? Huwaje mtu kama K kupitwa na … kwa nini iweje? Kwani wao si viumbe wa Mungu ingawa wanajipata na kujiweza? … (uk. 8).

Mwandishi anatuonesha matukio ya kiajabu yanaendelea kumtokea K katika kasri lake. K anashikwa na kikohozi yabisi, kichefuchefu kinafuata na kisha tumbo linamchiririka kwa sauti thelathini na nne ya mnung'uniko. Baada ya K kujizoazoa msalani, anajikuta ameenea uchafu msambani, makalioni, mapajani na miguuni na ghafla masikio yake yanazibukia kicheko kizito cha tashtiti kinachokuja kwa sauti yake yeye mwenyewe na kujaa ndani mote. Mambo mageni yanakuwa yakimwandama kila siku hasa anapokuwa na wasiwasi au hamaki. Kicheko anachokisikia kina sauti inayofanana na yake mwenyewe lakini hajui kinatoka wapi. Matukio ya kiamzingaombwe bado yanaendelea kujitokeza pindi maneno yanapojidhihirisha kwa bi Nyakanga na Zuhura. Mwandishi anasema:

> Ni-me-o-na… kwa ma-ndiga ya-ngu ki-su ki-na-ke-ke-ta shi-ngo… da-mu mbi-chi i-na-mwa-i-ka… na m-ke-ke-taji ni su-ru-ru … hu-yu Su-ru-ru - a-li-ye- ku-wa mu-me we-nu… Ha-ja-ku wa-che-ni yu-no, nyingi n'do m-me – mwa-cha a-na-ngo-ja ku-li-pa ki-sa-si yu-no (uk. 52).

4.3.3.3.2 Matumizi ya Wahusika wa Ajabu

Wahusika ni watu, ama viumbe waliokusudiwa wawakilishe dhana mawazo au tabia za watu, katika kazi za Fasihi. Riwaya ya *Babu Alipofufuka* imetumia wahusika wa ajabu ajabu ambao kwa hakika wanawakilisha tabia za watu halisi katika jamii husika. Mtunzi ametumia wahusika wa aina hii akiwa na lengo la kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Kwa mfano matumizi ya wahusika wa ajabu katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* wahusika kama mazimwi. Mwandishi anasema:

> …Siku hizi k kinyinginya change anaweza kuketi meza moja na watu ambao miaka michache iliyopita ilikuwa miko kukaa nao mazimwi aliwaita… Leo K akiwatazama wale aliokuwa akiwaita mazimwi jana, huona kumbe sura zao zinafanana ya yake… Mzula, dereva wake, aliibuka ghafla kama anavyoibuka siku zote kwa wasifu wa jivuli la mahepemahepe. Akapeperuka kwenda kumfungulia mlango wa nyuma K naye akatumbukia ndani… (uk. 10, 12, 17).

Wahusika hawa ni wa ajabu ajabu na wanashirikiana na mhusika wa kawaida ambaye ni ngumu sana kushirikiana naye katika ulimwengu halisi. Wahusika hawa wanalengo la kufikisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa. Pia wahusika wa ajabu wanajitokeza pale mwandishi anaposema:

> Baina yangu na K, nafasi nyembamba kama unyuzi. Bahati mbaya kwelikweli.Nilidhani pumzi zangu zingetosha kuniunganisha naye. Labda zingeweza kuanzisha mawasiliano yoyote, lau madogo, lakini wapi! Kwenye mwanya wetu mwembamba hajawahi kujipenyeza shetani seuze malaika. N'namkodolea macho K. N'nampungia mkono. N'namkodolea macho K. N'nampungia mkono. N'najikaza kumshika kichwa hata n'nampigia kelele kumwita- mawe! (uk. 1).

Katika nukuu hii mwandishi anaonesha ni kwa jinsi gani ametumia kionjo hiki kama jinsi kinavyotumiwa na watunzi wa riwaya za sasa. Wahusika wa ajabu kama mashetani, mizuka na mizula imetumika katika riwaya hii.

4.3.3.3.3 Dhana na Dhima ya Mapenzi Na Ngono

Waandishi wengi wa riwaya za sasa kama mwandishi Said A. Mohamed ametumia kwa kiasi kikubwa kionjo hiki cha uandishi. Miongoni mwa viashiria vya kionjo hiki ni

pamoja na uchi au utupu. Riwaya hii ya *Babu Alipofufuka* kionjo hiki kinajitokeza pale mtunzi anaposema:

> …Juba lake la hariri wazi, na ndani hakuvaa chupi… Kazi ya kumuhasi kila mwanaume… Au mwendawazimu akitembea kama alivyozaliwa, na kuusifu uume wake… Alikuwa kavaa chupi iliyoroa damu chapachapa… Walikuwa wakitoa ishara za mapenzi (uk. 3, 11, 24, 25, 27)

Viashiria vyote hivi vinaonesha ni kwa jinsi gani watunzi wa zama hizi wanavyoyazungumzia mapenzi kwa hali ya uwazi zaidi kuliko awali. Hapo awali kazi za akina Shaaban Robert zilizungumzia mapenzi kwa namna ambayo hata msomaji asingeweza kujua kama ni mapenzi ndiyo yanayozungumziwa.

4.3.3.3.4 Matumizi ya Nyenzo za Kisasa na Teknolojia

Matumizi ya nyenzo za kisasa na teknolojia ni miongoni mwa kionjo cha uandishi katika Fasihi mpya. Riwaya ya *Babu Alipofufuka* imetumia pia kionjo hiki kuonesha upya katika utunzi wa kazi.

> Wakati huu alihitajia limonsin lake na habari zikaenda haraka kwa kompyuta… Habari huenda kwa kompyuta siku hizi! Waliposikia kazungukwa na wahuni kule njiani, ilibidi waje hapo huku wamevaa hofu, wasiwasi na kujali (uk. 16, 29).

Mbinu hii ya matumizi ya nyenzo za kisasa na teknolojia imeanza kutumika baada ya kugundulika kwa vifaa vya kisasa kama kompyuta. Hapo zamani kwa kuwa kifaa hiki hakikujulikana waandishi hawakutumia kionjo hiki katika uandishi wao kwa kutojulikana kwake. Lengo hapa ni kuonesha maendeleo yaliyotokea katika uandishi ndiyo maana kumekuwa na badiliko katika utunzi huo.

4.3.3.3.5 Kuyajadili Maisha kwa Kina

Kipengele hiki ni miongoni mwa vionjo vya kiuandishi katika riwaya hii. Maisha hujadiliwa kwa kina na waandishi ili kuonesha matatizo mbalimbali yanayoikumba jamii. *Babu Alipofufuka* ni miongoni mwa riwaya ambayo imefanikiwa zaidi kujajadili maisha

kwa kina kwa kuonesha matatizo kama vile uongozi, uwekezaji na athari zake, utandawazi na hata uporaji wa mali ya uma. Mwandishi anajadili matatizo haya kwa kuonesha jinsi hali halisi ilivyo jinsi wenye navyo wanavyojilimbikizia mali huku wasionacho wanabaki kuteseka na kunyang'anywa mali zao. Pia, mwandishi anazungumza kuhusu athari za soko huria ambazo kwa kiasi kikubwa huwaangamiza wale wenye hali ya chini.

Mwandishi anasema kwamba, huu unaoitwa uchumi huria haulengi kuzisaidia nchi changa isipokuwa kuzinyonya rasilimali zao na kuendelea kuyaneemesha mataifa yaliyoendelea yanayojulikana kama mataifa ya ulimwengu wa kwanza. Kama wananchi wa mataifa yanayoendelea, tunachoambulia ni kuuza utu wetu na rasilimali zetu. Haya yanajidhihirisha mwandishi anaposema:

> Huu ndio utamaduni wetu waliokurithisheni, matumizi ya vitu, si utengenezaji wake. Mmekulia kuona anasa, fahari na utumikizi wao… Afrika imegeuka kuwa jalala (dampo) la bidhaa za nje. Mbaya zaidi wanauza kwa bei ya juu… Kila tunachokitumia hakina asili yetu (uk.13, 113, 38).

Pia, mwandshi anazidi kukemea athari za utandawazi hasa kiuchumi kupitia sauti ya Mzuka. Anasema:

> Kukuruhusu… kujiachia na kukubali kupandwa juu ya mabega… kukubali kufunguliwa kichwa na kuchotwa akili zote; kuchotwa na kunyang'anywa hata mazinduzi ya kuishi… hili ni kosa la dunia mlio nayo (uk. 79).

Utamaduni wa kuiga unatutafuna wenyewe bila hata ya kujua. Mwandishi analizungumza hili kwa kuruhusu kuchotwa akili zetu na kuiga kila wenzetu wa Ulaya wanachofanya ni vitu vya ajabu na vinaturudisha nyuma kimaendeleo bila ya sisi wenyewe kujua.

4.3.3.3.6 Matumizi ya Ndoto

Mwandishi katumia ndoto katika utunzi wake. Ndoto hizi hutumika katika kutabiri nini kitakachotokea kwa mhusika katika riwaya hiyo. Hiki ni miongoni kionjo cha uandishi

katika utunzi wa Said A. Mohamed. Mwandishi huyu amefanikiwa kutumia kionjo hiki katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* kama anavyosema:

> … Hivyo ilikuwa sala yake ya mwisho kabla ya kulala siku hizo kabla ya kuota... ndoto za kuruka angani kesho atakapoamka… Na huyu hapa ndiye yeye. Ndoto si ndoto tena. Limonsin!... Hii ni ndoto tu ya muda mfupi ingepita, itapita! (uk. 13, 18, 22).

Ndoto hizi kwa kiasi kikubwa zinaambata na dhamira ya ukombozi. Mhusika huota ili kukumbuka matukio ambayo aliyafanya ya kunyanyasa na kuwaonea watu wasiokuwa na hatia katika maisha. Kwa jumla Said A. Mohamed ametumia ndoto kama nyenzo ya kuuelezea uhalisia kwa namna pindu.

4.3.3.4 Vionjo vya Kiuandishi katika Riwaya ya *Utengano*

Riwaya ya *Utengano* imetumia vionjo vya kiuandishi ambavyo huleta upya katika riwaya hii. Vionjo hivyo ni hivi vifuatavyo:

4.3.3.4.1 Kuyajadili Maisha kwa Kina

Mwandishi huyu anayajadili maisha akionesha jinsi wananchi walivyopambana na kupigana kuwaondoa wakoloni. Baada ya uhuru viongozi wakapewa dhamana ya kuwaongoza wananchi. Viongozi hawa wanaongoza kwa mabavu huku wao wakifaidi na wananchi walala hoi kutofaidi. Mwandishi anamchora muhusika bwana Maksuudi kama kiongozi msaliti kwa wananchi wake. Bwana Maksuudi na Zanga wamejilimbikizia mali za umma kwa ubadhilifu wanaoufanya kutokana na nyadhifa zao. Kwa mfano, mwandishi anasema:

> … Lakini nililokwitia hapa linazidi kuliko habari ya uchaguzi, yaani ni jambo la kidugu, jambo la damu. Unajua kuwa mimi mwaka huu nitasimamia uchaguzi wa ubunge. Na pia unaelewa kwamba kuna kesi mbaya ya magendo inayonikabili mbele yangu, ingawa najua ninyi polisi hamna ushahidi, lakini pindi ikitoka habari na kuisikia kesi hii wananchi, jambo hilo litaniharibia kura zangu, kwani hivi sasa nina tamaa ya ushindi… (uk. 74-75).

Mtunzi anatudhihirishia jinsi viongozi walivyo na tamaa na uchu wa kuongoza huku wakiwanyanyasa wananchi. Kiongozi anakashifa ya magendo na wakati huo huo bado anataka kugombea tena ili apate nafasi ya kuendelea na magendo yake. Wanaofaidi ni tabaka la juu wakati tabaka la chini ni kuteseka na kuhangaika na maisha. Baada ya miaka mitano kiongozi huyo ambaye hajawafanyia chochote wananchi wake waliomchagua anarudi tena kuomba kura.

4.3.3.4.2 Dhana na Dhima ya Mapenzi na Ngono

Ni miongoni mwa kionjo cha uandishi katika riwaya hii ya *Utengano*. Mtunzi anamchora mhusika Kazija na Mussa wakihitajiana kimapenzi. Watunzi wa sasa wanapenda kujadili kionjo hiki kwani ndicho kilichoteka akili na masikio ya watu au wanajamii kwa kiasi kikubwa. Mapenzi na ngono katika jamii hii ya sasa yana nguvu kubwa kuliko kitu chochote. Katika riwaya hii Mussa na baba yake ambaye ni bwana Maksuudi wanajikuta wote wakiwa na uhusuano wa kimapenzi na msichana mmoja ambaye ni Kazija. Jambo kama hili kwa jamii ya sasa ni kawaida sana na hakuna hata anayeogopa. Kuthibitisha hili mwandishi anasema:

> … Come on darling, alimbembeleza kwa sauti yake nzito iliyojikokota.
>
> ‘Hebu miye usinipake mate ya kilevi.’
>
> Leo siyo?’
>
> ‘Leo tokea hapo. Kwani lini? Leo ndio leo, asemaye kesho mwongo.’…
>
> Come on, wacha tustarehe.’
>
> ‘Ustarehe sasa hivi, ngoja tu.’
>
> ‘Ningoooje niiiini?’ Mussa alijaribu kuvamia, lakini sasa alikamata hewa…
>
> ‘Ko-ko-ko…’ mlango uligongwa taratibu. Kazija aliruka kwenye kitanda kama mkizi, akamkamata mkono Mussa, ‘Upesi.’ Mwenye nyumba kaja… (uk. 7, 9).

Mapenzi kama haya yapo katika jamii zetu. Mapenzi ya kustarehe tu bila ya kuwa na woga wowote. Magonjwa yamekuwa ni mengi kiasi kwamba hata wanandoa na wasi wanandoa wanalia kwa kuambukizwa magonjwa hatari kama vile UKIMWI ambao hauna tiba.

4.3.3.4.3 Matumizi ya Ndoto

Mtunzi huyu katika riwaya yake ametumia kionjo hiko cha ndoto. Ndoto hizi zinaonekana kwa Maimuna ambaye anaota kuhusiana na mnyama wa kitisha anayemfukuza kwa kasi ya ajabu. Doto hizi zimetumika kama kuelezea uhalisia kwa namna pindu katika maisha. Anasema:

> Chatu kubwa lilikuwa likimfukuza Maimuna. Alikimbia mbio, lakini kila alipotazama nyuma chatu lilimwandama. Alifukuzwa kwenye uwanda usio kikomo wenye majani na maji maji yanayoteleza. Nyoka alipata kasi zaidi na Maimuna alirejeshwa nyuma. Kila mara alianguka na kujiokota mbio mbio. Hata hivyo alikupuka uzuri. Pumzi zilimfoka. Akahema huku moyo wake ukipiga upesi upesi. Mara kwa ghafla ulimzukia ukuta mrefu kama mnazi. Ilimbidi asite. Akatapatapa. Hajui akimbilie wapi. Na nyuma chatu linakuja kama upepo. Alipiga kelele. Sasa aligeuka akalikabili chatu. Hajiwezi. Pumzi zimemuisha. Mwili umemnyong'onyea kwa hofu na machofu… Ilikuwa wakati huu ndipo alipoamka, kaloa jasho mwili mzima. Moyo ulikuwa ukimuenda mbio na alikuwa pumzi juu juu. Kanga yake iliyojikunja kama peto la nyoka ilimkaa juu ya kifua. Upesi aliirushia mbali hiyo kanga... (uk. 132, 133, 134).

Ndoto hizi za Maimuna zinaonesha jinsi mtunzi alivyo mahiri katika kionjo hiki. Mtunzi ametumia ndoto hizi ili kueleza hali halisi ilivyo katika jamii. Ndoto hizi kwa kiasi kikubwa huambatana na maudhui ya kutafuta ukombozi ambao Maimuna alitakiwa akujikomboa kutoka pale alipokuwa.

4.3.4 Kulandana kwa Vionjo vya Uandishi katika Riwaya za Shaaban Robert na Said A. Mohamed

Ijapokuwa waandishi hawa ni wa zama mbili tofauti, Shaaban Robert akiwakilisha zama za nyuma na Said A. Mohamed akiwakilisha zama za sasa bado wanafanana katika kipengele hiki cha vionjo vya kimaudhui.

4.3.4.1 Kulandana Kwao katika Vionjo vya Kimaudhui

Kwa jumla, watunzi wote wamesawiri athari za mifumo ya kiuchumi katika jamii na ngazi ya kimataifa pia. Waandishi hawa pia wanashambulia na kukemea matatizo mbalimbali yaliyopo katika jamii huku wakipaza sauti zao kwa watu wa tabaka la chini ambao ndio wanaonyanyasika kwa hali ya juu huku tabaka la juu ndio wanaofaidi mema ya nchi kwa kiasi kikubwa. Waandishi hawa wanatoka katika zama tofauti, lakini kwa kiasi kikubwa wamejadili matatizo yanayokabili jamii kwa jumla kama vile uongozi, utamaduni, mapenzi, athari za uwekezaji na utandawazi katika jamii ya sasa. Kwa mfano Shaaban Robert anawataka viongozi wawe waadilifu katika kuongoza kwao. Vivyo hivyo, Said A. Mohamed anawataka viongozi kuwa waadilifu katika uongozi. Mwandishi anasema:

> Rai, mfalme wa Uhaibuni, alikuwa mfalme namna ya pekee yake duniani. Alikuwa na tabia iliyohitilafiana kabisa na tabia za watu wengine wa zamani zake. Tabia yake ilijigawa katika theluthi tatu mbalimbali kama rangi ya ngozi ya punda milia. Kwa theluthi ya kwanza alikuwa msuluhifu akapendwa na watu, kwa theluthi ya pili alifanana na Daudi akaheshimiwa kama mtunzaji mkuu wa wanyama, na kwa theluthi ya tatu alikuwa kama Suleimani akatiiwa na majina… (uk. 1).

Kwa upande wa Said A. Mohamed anaonesha jinsi muhusika K alivyokuwa akiongoza kimabavu hata akawa anasaini mikataba feki ili kujinufaisha. Mwisho wake huwa ni aibu. Mwandishi anawataka viongozi wa jamii kuwa waadilifu kwani wamepewa dhamana ya kuwaongoza wananchi. Mwandishi anasema:

> … FFK ni upeo wa utamaduni. Hivi leo ukitaka kuuangalia upeo wa sanaa tazama mwili wa mwanadamu katika utupu wake. Tazama umbo la mwanadamu; jinsi Mungu alivyotuumba. Ukitaka kuona hivyo nenda FFK… Ni kitu kipya FFK, na kitu kipya kina uzuri wake, hasa kibiashara… (uk. 44).

Hapa mwandishi amewachora viongozi waliojaa usakiti na uonevu katika kuongoza jamii. Mwandishi anakemea vikali viongozi wenye tabia kama hizi za kujilimbikizia mali kwa kusaini mikataba feki ambayo mara nyingi wao ndio hunufaika zaidi. Watu wa tabaka la

chini wanateseka huku wa tabaka la juu wanakula raha. Suala hili limewafanya waandishi hawa kulandana katika kionjo hiki kimaudhui kwa kujadili na kuonesha mifano ya kiongozi anavyotakiwa kuwa.

Kufanana kwingine kuanapatikana katika baadhi maudhui ya kazi zao ambayo yamebeba athari za mafundisho ya dini ya Kiislam. Waandishi hawa wote wawili wameathiriwa na dini kiasi kwamba msikiko mkubwa pia unapatikana katika kazi zao walizozitunga kwani walizaliwa na kukulia katika dini na mazingira ya Uislam. Kazi zao zinawataka wanajamii kuendana na misingi ya dini ya Uislam kama kuswali na hata jinsi ya kutenda kama jinsi dini hiyo inavyomtaka mwanadamu kutenda. Pia, hata kwa upande wa wahusika wanawake, wamezungumzia sana suala hili jinsi mwanamke wa Kiislam anavyotakiwa kuwa na maadili katika jamii. Kwa mfano Shaaban Robert katika baadhi ya majina ya wahusika wake kama vile Utubora, Adili, Karama, Fadhili na Auni. Kwa upande wa Said A. Mohamed ametumia wahusika kama vile Zuhura, Maimuna, Farashuu, Musa, Kazija na Asumini majina yote haya yana ufungamano wa kimaana na maudhui ya dini ya Uislam. Kwa mfano, katika riwaya ya *Adili na Nduguze* na *Utubora Mkulima* wahusika wakuu wake wanakumbana na matatizo mengi katika jamii wakisababishiwa na wanajamii au hata ndugu lakini wanaenenda jinsi dini inavyomtaka mtu awe. Mwandishi anasema:

> …Adili alikuwa mwema na msamehevu. Alibaini kama Ikbali alilaumika kwa kuficha siri, kadhalika yeye mwenyewe alilaumika kwa ukatili… Adili aliomba Mungu awabariki ndugu zake ugenini, naye ampe riziki yake kwao…Adili alikuwa tayari siku zote kugawana na mtu ye yote tonge moja la chakula lililokuwa mkononi mwake. Alipoona ndugu zake katika matambaa hakuweza kuhimili… (uk. 8, 12).

Shaaban Robert anaonesha ni kwa kiasi gani alivyoshika dini kiasi kwamba anawavisha wahusika wake matendo ya kidini. Adili ananyanyaswa na ndugu zake lakini bado anawapenda na kuwathamini. Kwa kila anachokipata na kuwa msamehevu kama dini inavyotuasa kusameheana. Mwandishi huyu anasisitiza suala la kupendana, kujaliana na

kuthaminiana katika dunia hii kwani visipokuwepo vyote hivi hata maovu yatazidi katika jamii. Mtunzi wa kihalisia anapaswa kuijua jamii yake na jinsi maisha yalivyo kwa jumla. Shaaba Robert anawakilisha uhalisia, kwani alichokitunga ni ukweli; na ndivyo binadamu anavyotakiwa kumcha Mungu. Mfano mwingine unapatikana katika riwaya ya *Utengano* ambapo mwanamke anafukiza udi nguo zake ndipo avae. Jambo kama hili kwa mwanamke wa Kiislam ni kawaida na ndivyo inavyotakiwa kuwa katika dini yake anasema:

> …Hivi sasa, kabati li wazi, amekabiliana na kioo, Kazija anamaliza hatua yake ya mwisho ya kujikwatua. Kajikatia kanga ya moto ya kifua iliyokwisha fukizwa. Mgongoni kanda za kanchiri zinaonekana zimesaki kwenye misirimbi ya nyama zake za bega. Mkono unaopuna uso wake kwa shada la kitambaa ulikuwa umeshungulika kuiweka sawa podari… (uk. 1).

Udi kwa mwanamke wa Kiislam ni suna kwake. Mwandishi anaijua vyema dini hii ndiyo maana ametumia maneno kama haya kufikisha ujumbe wake kwa jamii aliyoikusudia kwani anatunga kulingana na jamii ilivyo na kwa wakati huo udi ni kitu kinachotumika katika mazingira ya Uislam. Pia, katika riwaya ya *Utubora Mkulima* suala hili la dini linajitokeza mwandishi anaposema:

> …Hasa katika wakati ujao alikusudia kuwa huru, kuishi maisha yake mwenyewe katika ulimwengu wa Mungu kama babu yake Adamu alivyoishi. Basi alikuwa na mawazo nana hii njiani mpaka akafika nyumbani kwake… llisadikika kuwa miji mikubwa ilikuwa maangamizi ya maisha ya watu ambao kwa haraka ya kujitafutia fahari na vyeo vyao wenyewe walikuwa hawaoni kusudi la Muumba, kuwa watu walilazimu kuishi katika ulimwengu kwa kula matunda ya ardhi, na kuwa wakati wote uliotumiwa hapa ulikuwa wa kujiandaa tu kwa maisha ya wakati ujao… Vitabu vya dini tangu zilipokuwa dhaifu hata zikawa maarufu duniani; tangu zilipokuwa za watu wachache wanyonge hata zikawa mali za atu kadha wa kadha wa hali mbalimbali (uk. 9, 19, 23).

Katika suala hili la dini Haji (2015) anamnukuu Said A. Mohamed katika mazungumzo yake akizungumzia suala la dini kuwa:

> Kazi zangu nyingi zikiwemo mashairi, riwaya na tamthiliya huwa nakipachika kipengele cha dini ili kuonesha ukweli na namna ya watu waovu wanavyoichukulia dini hii adhimu[9].

Nukuu hii inatuangazia ni jinsi gani suala la dini hasa ya Uislam lilivyomshughulisha mwandishi huyu katika kazi zake nyingi akionesha jinsi watu wanavyoichukulia na jinsi wanavyotakiwa kuenenda katika jamii. Kwa mfano, Bwana Maksuudi alitumia mwamvuli wa dini ili kuficha maovu yake yasijulikane katika jamii.

4.3.4.2 Kulandana Kwao katika Vionjo vya Kifani

Kufanana kwo kunapatikana katika kuzisana kazi zao kwa kutumia mbinu ya uhalisia mazingaombwe, waandishi hawa wanatoka katika zama mbili tofauti zama za nyuma za kufungwa na mikatale ya kikanuni ikiwakilishwa na Shaaban Robert wakati Said A. Mohamed anawakilisha zama za sasa. Waandishi wote hawa wametumia mbinu hii ya uhalisia wa ajabu kama mbinu mojawapo ya kufikisha ujumbe katika jamii zao. Ijapokuwa mbinu hii ndio imeshika hatamu sana katika utunzi wa wakati huu wa sasa, huko nyuma Shaaban Robert aliitumia katika kusana kazi zake. Matumizi ya matukio ya ajabu na hata wahusika wa ajabu yametumika katika kazi zao kiasi kwamba hata kuna wakati kazi zinakuwa ngumu kuelewa kutokana na matumizi makubwa hayo ya uajabu katika kazi zao hizo. Kwa mfano katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* mwandishi ametumia mbinu hii kwa kiasi kikubwa katika kazi nzima akionesha uhalisia mazingaombwe na nafasi yake katika jamii. Anasema:

[9] Mazungumo binafsi kati ya Haji na Prof. Said A. Mohamed yaliyofanyika tarehe 07/03/2015 mjini Zanzibar.

> …K aliposikia jibwa lake Doggy likinung'unika njaa, alipandwa na hamaki. Mara hii nini tena? Nani anamcheza shere? Mwezi mzima kwa hakika kazi ni hiyo hiyo. Weka sahani za vyakula, sahani toweka… Weka sahani, sahani ondoka… Nani angeshukiwa kama si watumishi? Kwa hiyo, fukuza mtumishi mmoja ingiza mwengine mlolongo mrefu us'o kikomo… Dakika moja sahani ipo, kufumba na kufumbua haipo!...
> "I wapi sahani?"
> "Si hii hapa bwana…!" Biye bila shaka kaemewa. "Niliza… nilizani… umeshaiona."
> "Nilizani… nilizani… mimi nataka ukweli sitaki dhana na uzushi mtupu… sahani iko wapi?... chakula cha Doggy kiko wapi?... (uk. 5, 6).

Mwandishi ametumia mbinu hii ya kihalisia mazingaombwe kwa kutumia wahusika wa ajabu ajabu kama mazimwi, maiti na mizuka katika kazi yake kwa lengo la kufikisha ujumbe kwa jamii aliyoikusudia. Kwa hali halisi, maiti na mazimwi hayawezi kuelezeka katika ulimwengu halisi. Msanii anaonesha ukomavu wa mbinu hii kwa kuitumia ili kufikisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa. Kwani, wapo wanaotenda jinsi mhusika K alivyokuwa akitenda kuwanyanyasa wananchi wake kwa kuwakaribisha wawekezaji na kuwatesa wazawa. Uhalisia ajabu mwingine unapatikana kupitia muhusika K alipokufa na baada ya kufufuka akajikuta amerudia hali yake ya utoto, kupaa kwa limonsini na K kuishi na watu kama mizuka, mafuvu na maiti.

Shaaban Robert naye ametumia mbinu hii ya uhalisia mazingaombwe katika riwaya ya *Adili na Nduguze* pale ambapo ndugu zake na Adili wanabadilika na kuwa manyani kama adhabu waliyopewa. Anasema:

> …Manyani mawili yaliyofungwa viuno minyororo ya dhahabu yalikuwa yamelala kitandani. Adili aliweka sinia juu ya meza. Nyani moja lilipofunguliwa lilirukaruka likalia kinyonge. Adili allikamata akalifunga miguu ya mbele na nyuma kwa kamba. Aliplitupa chini alishika mjeledi kwa mkono wa kulia akalipiga mpaka likazirai. Nyani jingine lilipigwa likazirai vile vile. Manyani yalipozinduka yalinasihiwa. Adili aliapa kuwa hakufurahi kuyaadhibu, na kwamba alitazamia faraja yao kutokea karibu… (uk. 6).

Kwa hali ya kawaida hatutarajii binadamu kubadilika na kuwa nyani kama ndugu zake na Adili walivyobadilika. Mbinu hii inatumika kuonesha uhalisia katika maisha tunayoishi kwa njia ya uajabu. Upo uajabu mwingine wa mwanamke kugeuka kuwa tuta la mchanga

katika riwaya hii. Pia katika riwaya hii ya *Adili na Nduguze* umazingaombwe unajitokeza pindi msichana alipojigeuza tandu. Mwandishi anasema:

> …Ghafula tandu lilijigeuza mwanandamu, yaani, msichana mzuri. Uso wake ulivuta macho ya Adili kwa haiba yake kubwa. Mbele ya mwanamke mia moja wazuri, msichana huyo angalitokea, wote wangalijichulia wenyewe kwa kujiona hawakulingana naye kwa uzuri… Baada ya hayo msichana alielekeza kidole chake cha shahada chini. Mara moja ardhi ilipasuka akaingia ndani yake. Alipokwisha jitia ndani ya ardhi ilijifunga sawia. Msichana hakuonekana tena. Adili alifahamu kuwa alikuwa si mwanadamu ila jini. Kitambo kidogo aliona nyoka aliyemuua anawaka moto. Mara moja alikuwa majivu matupu. Kufumba kope na kufumbua mahali palipokuwa na majivu palitokea chemchemi ya maji safi. Mambo haya yalikuwa muujiza mkubwa sana kwa Adili… (uk. 18).

Kwa hali ya kawaida mtu hawezi kujigeuza tandu na kupasua ardhi na kujifukia. Mbinu kama hii inatumiwa na waandishi kwa lengo la kuonesha uhalisia mazingaombwe ambao kwa kiasi kikubwa ulikuwa unatumika katika Fasihi Simulizi hapo awali.

4.3.5 Kutofautiana kwa Vionjo vya Kiuandishi kati ya Shaaban Robert na Said A. Mohamed

Waandishi hawa kwa kiasi kikubwa wanatofautiana katika vionjo vya kiuandishi kimaudhui na kifani. Tofauti hiyo ni kama ifuatavyo:

4.3.5.1 Kutofautiana Kwao katika Vionjo vya Kimaudhui

Waandishi hawa hutofautina katika kiwango chao cha utunzi. Kwa upande wa Shaaban Robert amehubiri sana suala la utu wema na mapenzi miongoni mwa wanajamii. Suala hili ndilo linalothibitisha falsafa yake ya siku zote wema hushinda ubaya. Falsafa hii inajitokeza katika kazi zake za kifasihi takribani zote. Haya yanajidhihirisha kupitia katika riwaya ya *Adili na nduguze* ya Shaaban Robert iliyojengwa katika msingi wa utu wema. Mhusika Adili anapewa uhusika huu wa utuwema kama alivyowafanyia nduguze. Yapo mengi mabaya waliyomtendea ndugu zake lakini hakulipiza ubaya bali aliwafanyia wema mkubwa. Mwandishi anamchora kiongozi mfalme Rai akiwa na utuwema katika uongozi wake. Mwandishi analithibitisha hili kwa kusema:

> Rai alikuwa kiongozi mwadilifu na Mfalme mwema sana. Hakusita kufanya kazi ndogo wala kubwa kwa mikono yake mwenyewe. Kazi nyingi za ufalme alizitenda yeye mwenyewe. Zile ambazo hakuwahi kuzitenda yeye mwenyewe alipenda kuziona kwa macho yake zilivyofanywa. Kwa bidii zake kubwa aliweza kushiriki katika mambo mengi ya maisha akasaidia maendeleo makubwa ya nchi yake hakulazimishwa mtu yeyote kutenda tendo fulani, lakini alishawishi kila moyo wa mtu kuiga alivyotenda kwa hiari yake mwenyewe. Alikuwa na mvuto mkubwa juu ya mioyo ya watu. Alitumia mvuto huu juu ya watu mpaka nchi yake ilikuwa haina mvivu, goigoi wala mwoga… (uk. 2).

Pia, katika riwaya ya *Utubora Mkulima* falsafa ya Shaaban Robert ya utuwema inazidi kujidhihirisha pale mwandishi anaposema:

> …Utubora alistahili sana ijara kubwa kama hiyo kwa sababu ya sifa alizo kuwa nazo. Alikuwa mtu imara mbele ya telezi nyingi, kama vile hiana na mengine; mvumilivu mbele ya majaribu magumu kama rushwa; hodari mbele ya mashaka mazito, mfano wa kushika amana au dhima kubwa; mwaminifu kama mchana; na msiri kama usiku. Kwa kushika majira alikuwa kama saa; na mahudhurio yake mema katika kazi hayakuwezekana kushindwa na watumishi wengine… Tabia ya Utubora ilivutia watu wengi waliokutana naye, ingawa yeye mwenyewe alikuwa haujui mvuto aliokuwa nao. Baadhi ya watu walipenezwa tu na Utubora bila sababu, lakini wengine waliona uanadamu uliokamilika kwa mtu huyu (uk. 1, 43).

Utubora anaonekana ni kiongozi mwema na makini katika kazi. Shaaban Robert anasisitiza utuwema katika jamii kuwa ndio msingi wa maendeleo kama jinsi Utubora alivyokuwa mwema na kuleta mafanikio makubwa sana katika maisha yake. Maelezo haya yanadhihirisha ni kwa jinsi gani Shaaban Robert alivyokuwa akizungumzia suala la utuwema katika jamii.

Kwa upande wa Said A. Mohamed, kwa kiasi kikubwa, ameshambulia mifumo ya kijamii kama vile utamaduni, matendo yasiyotija ya viongozi na kuguswa kwa kiasi kikubwa na wanawake na kuishadidia falsafa yake ya mwisho wa ubaya aibu. Ndiyo maana katika kazi zake kama vile *Utengano* na *Babu Alipofufuka* falasafa hii inajitokeza. Kuthibitisha hili katika riwaya ya *Utengano* mwandishi anasema:

> Dakika zilipita kuongeza masaa. Mussa bado alikuwa mvunguni. Alikuwa kama mahoka. Nadhari iliyokuwa imempotea kwa muda mrefu, taratibu ilimrejea. Sasa mazungumzo ya bi Kazija na Bwana Makusudi aliyasikia waziwazi… Bwana Makusudi aliruka na kumkabili mume mwenzie. Kazija aligeuka taratibu. Mussa alihiziki. Kumbe mume mwenzie ni babaake, babaake bwana Maksuudi. Bwana Maksuudi alipigwa na mshangao wa ghafla. Walikutana uso kwa uso. Maksuudi alinyongea na Mussa alibwagika na miguu ilimnyong'onyea. Zile hamaki zake zikatafuta pahala. Hakujua wapi. Kazija alikwisha simama, akaanza kucharaza mambo yameshaanza kuhongera, bado kukamilika tu… (uk. 13).

Mwandishi anakemea vikali tabia za wanaume ambao wanaacha wake zao nyumbani na kwenda kutafuta vimada wa nje. Matokeo yake wanajikuta wakikutana na watoto wao kwa mwanamke mmoja. Suala hili linasababisha kutofautiana kati ya Shaaban Robert na Said A. Mohamed katika kipengele cha vionjo ya kimaudhui.

4.3.5.2 Kutofautiana Kwao katika Vionjo vya Kifani

Kwa upande mwingine, tofauti ya kifani inatokea katika suala la utumizi wa lugha. Katika kipengele hiki, kwa kiasi kikubwa, Said A. Mohamed anatumia lugha ya lahaja ya Kipemba wakati Shaaban Robert anaandika kazi zake kwa kutumia lahaja ya Kimtang'ata. Kazi nyingi alizozitunga jagina huyu zina ukomavu wa lugha fasaha ya Kiswahili. Kwa mfano riwaya ya *Adili na Nduguze* na *Utubora Mkulima*.

Tofauti nyingine ipo katika lugha ya wahusika wanawake. Shaaban Robert hajatumia lugha kali sana kwa wahusika wanawake. Wakati Said A. Mohamed ametumia lugha ya vijembe kwa wahusika wanawake kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, mazungumzo ya Bi Kocho, bi Farashuu na hata Kazija. Asingekuwa anaijua vizuri lugha ya wanawake angeshindwa kuwachora vile walivyo katika riwaya ya *Utengano*. Ufuatao ni mfano wa mazungumzo ya bi Kocho na bi Farashuu:

> Nikwambie nini bibi we, Binti Kocho alianza kucharaza, “nimemtoa mtawa wa watu. Nimempa maneno matamu. Nikamwonesha sanamu la mashujaa. Nnikamtajia mapenzi. Nikamuona kajaa tele… hatoki bibi, hatoki.’ ‘Lo ama wewe mchawi, sikudhani kama utaweza kumtoa kwa mizungu namna hiyo. Cheleko mama cheleko, nakuvisha kilemba’. Pongezi hizo zilimwingia gegoni Binti Kocho. Akakenua. Kisha akaendelea kumwaia Farashuu yale aliyoyasaza, ‘Basi si hayo tuu …’
> ‘Ehe, na yepi? Farashuu hamu ilimwenda.
> ‘Nimekuja kuchukua ukunga.’
> ‘Mwenye uchungu nani?
> ‘Bi Tamia… (uk. 31).

Mazumgumzo haya yanaonyesha ni kwa jinsi gani Said A. Mohamed alivyo fundi wa lugha za wanawake kwani mazungumzo anayoyazungumza Bi Kocho na Bi Farashuu yamejaa maneno ya kebehi, vijembe na kejeli kwa wanawake. Kwa kiasi kikubwa, hivi ndivyo wanawake walivyo katika jamii zetu.

Kutofautiana kwao kifani pia kunajitokeza katika kipengele cha wahusika. Shaaban Robert ametumia wahusika ambao ni vigumu kuaminika katika jamii hii ya sasa. Matendo wanayobebeshwa wahusika wake ni vigumu kuaminika. Unakuta kama ni mwema atakuwa hivyo hadi mwisho wa riwaya. Kwa mfano Adili katika riwaya ya *Adili na Nduguze* na Utubora katika riwaya ya *Utubora Mkulima*. Pia, Shaaban Robert ametumia wahusika wanyama kama vile manyani katika *Adili na Nduguze* ambayo ilikuwa ni nduni ya Fasihi Simulizi.

Said A. Mohamed wahusika anaowatumi katika kazi zake nyingi ni wa kawaida tu ambao kwa kiasi fulani huaminika na wapo katika jamii kwani wanapewa uhusika chanya na hasi, kuna wakati huwa wanabadilika kulingana na mazingira. Kwa mfano, Maimuna, Maksuudi, Zuhura Mapozi na K. Kwa minajili hii mbinu hii ya kuwaumba wahusika inawafanya waandishi hawa watofautiane.

Upande wa mandhari nao unaleta tofauti kati ya waandishi hawa wawili. Kwa kiasi kikubwa Shaaban Robert hupenda kutumia mandhari za kidhahania zaidi katika kazi

zake. Kitu ambacho kuna wakati inakuwa ngumu kujua haya mazingira ni ya wapi. Kwa mfano *Kufikirika* na *Kusadikika* kazi zote hizi zimebeba mandhari za kidhahania katika utunzi wake. Kwa upande wa uteuzi wa mandhari za Said A. Mohamed ni mandhari zinazoeleweka na hasa hutumia mandhari za Zanzibar ambako ndiko anakotokea. Kwa mfano kwenye *Utengano* na *Tata za Asumini*.

Kutofautiana kwingine katika kipengele hiki cha fani ni katika matumizi ya safari na ndoto. Watunzi hawa wametumia mbinu hii ya kifani katika kusana kazi zao. Kwa upande wa Shaaban Robert ametumia kwa kiasi kikubwa mbinu ya safari. Kazi zake nyingi zimejengwa katika safari lengo likiwa ni kuyafikia maudhui ya kutafuta ukombozi wa jamii mpya. Kwa mfano, katika riwaya ya *Adili na Nduguze* jinsi watu wanavyotumwa kwenda sehemu tofauti tofauti. Mwandishi anasema:

> Ikibali alitakiwa na Maarifa kwenda janibu kuchunguza kodi. Ikibali alikuwa mshauri katika halmashauri ya Ughaibu na mshairi wa mfalme… Alipofika Ughaibu alitoa habari za ujumbe wake. Alitaka sana kuficha siri ya manyani na adhabu yao, lakini hakuweza… Adili alisumbuka safarini kwa sababu ilikuwa mara yake ya kwanza kusafiri baharini. Baada ya safari ya siku tatu walifika bandarini. Bandari yenyewe ilikuwa ya kwanza katika bandari walizokusudia kwenda. Walishuka wakafanya biashara… (uk. 4, 7, 17).

Kwa upande wa Said A. Mohamed hutumia ndoto. Takribani kazi zake nyingi hutumia motifu hii ya ndoto ili kuelezea maudhui ya ukombozi. Ndoto hizi hujengwa katika wahusika wake kwa lengo la kufikisha ujumbe. Kwa mfano, katika riwaya ya *Utengano* ndoto za Maimuna. Anasema:

> Chatu kubwa lilikuwa likimfukuza Maimuna. Alikimbia mbio, lakini kila alipotazama nyuma chatu lilimwandama. Alifukuzwa kwenye uwanda usio kikomo wenye majani na maji maji yanayoteleza. Nyoka alipata kasi zaidi na Maimuna alirejeshwa nyuma. Kila mara alianguka na kujiokota mbio mbio. Hata hivyo alikupuka uzuri. Pumzi zilimfoka. Akahema huku moyo wake ukipiga upesi upesi. Mara kwa ghafla ulimzukia ukuta mrefu kama mnazi. Ilimbidi asite. Akatapatapa. Hajui akimbilie wapi. Na nyuma chatu linakuja kama upepo. Alipiga kelele. Sasa aligeuka akalikabili chatu. Hajiwezi. Pumzi zimemuisha. Mwili umemnyong'onyea kwa hofu na machofu… Ilikuwa wakati huu ndipo alipoamka, kaloa jasho mwili mzima. Moyo ulikuwa ukimuenda mbio na alikuwa pumzi juu juu. Kanga yake iliyojikunja kama peto la nyoka ilimkaa juu ya kifua. Upesi aliirushia mbali hiyo kanga... (uk. 132, 133, 134).

Motifu ya ndoto kwa kiasi kikubwa inatumiwa na mwandishi huyu katika kazi zake nyingi. Utunzi wa namna hii ni utunzi wa waandishi wa zama hizi katika kuelezea hali halisi ya maisha jinsi ilivyo. Pia, katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* matumizi ya ndoto yanapatikana pale mwandishi anaposema:

> …Hivyo ilikuwa sala yake ya mwisho kabla ya kulala siku hizo kabla ya kuota ndoto za kuruka angani kesho atakapoamka… Na huyu hapa ndiye yeye. Ndoto si ndoto tena. Limonsin!... Hii ni ndoto tu ya muda mfupi ingepita, itapita! (uk. 13,18, 22).

Waandishi hawa wanatofautiana katika kipengele hiki kinachotumika kama mbinu ya kiutunzi katika kazi za kifasihi.

4.4 Sababu za Mabadiliko ya Kiuandishi katika Riwaya ya Kiswahili

Fasihi ya Kiswahili kwa kiasi kikubwa imepiga hatua na kubadilika kwa kiwango cha hali ya juu ikilinganishwa na Fasihi ya hapo awali ya zama za akina Plato na Aristostle za kufungwa na mikatale ya kikanuni, na kanuni hizo zilimtaka kila mtunzi au mwandishi kuzifuata kila anaposana kazi ya kifasihi. Miongoni mwa sababu kuu za kubadilika kwa mikondo ya kiuandishi hasa katika Fasihi ya Kiswahili ni:

4.4.1 Mabadiliko ya Kijami au Historia ya Jamii

Jamii imepitia katika hatua mbalimbali kama vile kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni, baada ya uhuru na kipindi cha utandawazi. Katika kila kipindi kulikuwa na Fasihi yake

ambayo ilijipambanua katika kipindi husika. Fasihi ya kabla ya ukoloni ilitawaliwa na Fasihi Simulizi iliyokuwa ikiwasilishwa kwa njia ya mdomo ambayo ilikuwa ndio mfumo wa elimu unaojitosheleza katika kutoa mafunzo kwa mtu kutoka kuzaliwa mpaka kufa. Kwa mfano, kipindi hicho mtoto alipozaliwa alikutana na nyimbo za kubembelezea ambazo zilikuwa na dhamira ya kuelimisha, kubembeleza na kuburudisha.

Kadiri jamii inavyobadilika ndivyo na kazi ya Fasihi zinavyopokea mabadiliko. Fasihi ya wakati wa ukoloni, kwa kiasi kikubwa, ililenga kumtukuza mtawala wa kikoloni na kumpumbaza Mwafrika amuone mtu mweupe kwamba ndiye kila kitu. Pia, dhamira hizi zililenga kukuza utamaduni wa mtu mweupe kuliko Mwafrika. Mfano wa kazi za kifasihi zinazojitokeza katika kipindi hiki nyingi zilikuwa zimetafsiriwa tu ni kama *Alfu Lela Ulela* na *Hekaya za Abunuasi*. Pia, katika kipindi hiki ilikuwepo Fasihi ambayo ilipinga utawala wa mkoloni kwa kuwabeza na kuwakashifu juu ya utawala wao. Mfano wa kazi hizo za Fasihi ni *Kusadikika, Kufikirika* na *Adili na Nduguze.* Katika kipindi cha uhuru ni kipindi cha kushangilia uhuru na kazi nyingi zilikuwa zikiupongeza uhuru huo. Pia, zipo zilizokuwa zikiwabeza wale waliokuwa bado wakiufuata Uzungu. Mfano wa kazi za kifasihi zinazopatikana hapa ni *Mashairi ya Saadan Kandoro* (Senkoro, 1987). Baada ya hapo ndipo zilipokuja kazi za kihalisia zikijadili na kuchambua uozo uliopo katika jamii. Kwa mfano, riwaya ya *Babu Alipofufuka* inachambua maovu yaliyokithiri katika jamii, mwandishi anasema:

> Afrika imegeuka kuwa jalalal (dampo) la bidhaa za nje. Mbaya zaidi wanauza kwa bei ya juu… Kila tunachokitumia akina asili yetu… Huu ndio utamaduni wetu waliokurithisheni matumizi ya vitu si utengenezaji wake… Mmekulia kuona anasa fahari nautumikizi wao (uk. 13, 38,113).

Nukuu hii, inatuthibitishia kuwa uandishi umebadilika kutoka enzi za kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni. Kwa kuthibitisha hili Said A. Mohamed anasema kuwa:

> Jamii hubadilika kutoka kipindi kimoja kwenda kingine. Akatoa mfano hata mawe tunayoyaona hayakuwa hivyo hapo awali. Pia, huuliza wanafunzi wake kuna kitu kisichobadilika katika dunia. Jibu lake ni kuwa kila kitu hubadilika katika dunia. Vivyo hivyo, Fasihi nayo hubadilika[10]

Nadharia iliyotumika kuchambulia data katika utafiti huu inamtaka matunzi kuandika kiuhalisia na wakati huo kujua mabadiliko ya historia au vipindi mbalimbali vya jamii yake kwani uhalisia ni maisha ya kawaida wanayoishi watu. Nadharia hii ina msingi wa ushabihi ukweli na utunzi wa kimuwakati hivyo mabadiliko ya kijamii yanaendana na utunzi huo. Ndiyo maana na fasihi nayo hubadilika kulingana na kipindi maalum kwa kuzingatia utunzi wa kumuwakati huku msanii akishabikia ukweli wa mambo yaliyotendeka katika jamii yake.

4.4.2 Ongezeko la Wasomi

Kufikia miaka ya 80 kulikuwa na wimbi kubwa la ongezeko la wasomi waliosoma ndani ya nchi na nje ya nchi. Wasomi hao ndio waliokuwa chachu ya mabadiliko katika uandishi wa kazi za kifasihi. Hii ilitokana na kuvumbua maarifa mapya yanayohusiana na utunzi wa kazi za kifasihi. Wasomi hawa ndio waliochangia katika kuanzisha na kuitisha mijadala, midahalo na mahojiano mbalimbali yaliyokuwa yakihusisha mustakabali mzima wa kiutunzi wa kazi za kifasihi au kisanaa. Kwa mfano, ongezeko hili la wasomi ndilo lililosababisha watunzi kujadili kuhusu suala la mgogoro wa ushairi na kujiuliza kwa nini kusiwe na upya katika kazi za Fasihi kama vile ushairi na hata tamthiliya na riwaya. Je, ni lazima kuendelea kujikita katika urari wa vina na mizani, vivyo hivyo kwa utanzu wa tamthiliya na riwaya kuna ulazima wowote wa kubakia katika ukanuni kama ilivyokuwa awali.

[10] Mazungumzo binafsi kati ya mtafiti na Prof. Said A. Mohamed yaliyofanyika tarehe 5/1/2016 mjini Zanzibar.

Miongoni mwa wasomi hao ni kama vile Euphrase Kezilahabi, Mugyabuso Mulokozi, Kulikoyera Kahigi na Fikeni Senkoro waliohoji juu ya utunzi wa kazi za kifasihi. Lengo likiwa ni kutaka kuyachambua na kuyajadili maisha kama jinsi yalivyo bila ya kupindisha ukweli huo. Wasomi hawa ndio chachu ya kuendeleza mikondo ya kiuandishi katika Fasihi ya Kiswahili kwa kuja na dhana ya umajaribio katika Fasihi ya Kiswahili. Kuthibitisha hili Khamis Tatu anasema:

> Kuibuka kwa wimbi la wasomi wengi ndiko kunasababisha uandishi kubadilika. Wasomi hawa huchambua na kujadili hizi kanuni za kiuandishi zina tija gani. Kitu cha msingi ni mwandishi awe huru kuandika anavyotaka, lengo ni kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa jamii[11]

4.4.3 Umajaribio

Senkoro (2011) anaifasili Fasihi ya Kiswahili ya kimajaribio kuwa ni uandishi usiofungwa na mikatale ya kikanuni kama ilivyokuwepo awali. Mathalani, katika ushairi, yeye anaita ushairi huru usiofungwa na kanuni za urari wa vina na mizani kama wa akina M.M Mulokozi na K.K Kahigi. Kuukacha ukanuni huu ndiko kulikozaa Fasihi ya Kiswahili ya kimajaribio mnamo miaka ya (1960-1980). Anaona kuwa umajaribio huu unaweza kubainishwa au kudhihirika kwa kutumia nduni, vipengele au kaida za Fasihi Simulizi. Hapo awali nduni hizi zilikuwa hazitumiki lakini sasa zinatumika kwa wingi. Vipengele hivyo au nduni hizo za Fasihi Simulizi anazozizungumzia ni kama vile mianzo na miisho ya kifomula, marudiorudio, taharuki, ucheshi na wahusika wa ajabu katika kazi za kifasihi. Hivyo basi, katika utafiti huu mtafiti aligundua ya kuwa kwa kiasi kikubwa mbinu hii inatumiwa sana na waandishi walio wengi katika zama hizi za kiuandishi.

Kufikia miaka ya kuanzia 70 na 80 ndipo kulipozuka kipindi hiki cha umajaribio katika kazi za kifasihi. Kuvunjwa kwa silisila za ukanuni katika Fasihi ya Kiswahili au

[11] Mazungumzo binafsi kati ya mtafiti na Khamis Tatu yaliyofanyika Chuo Kikuu cha Dodoma tarehe 1/2/2016 mjini Dodoma.

uchopekaji wa mbinu mpya katika Fasihi ya Kiswahili na kuleta mitindo mipya kama vile taharuki, taswira, wahusika wa ajabu ajabu yote hii ilichangiwa na mbinu hii ya umajaribio katika Fasihi ya kiswahili. Katika kipindi hiki kwa kiasi kikubwa jamii ilishuhudia mabadiliko makubwa ya utunzi katika kazi za kifasihi kwa kugubikwa na upya. Fasihi ya Kiswahili ina tanzu mbili ambazo ni fasihi simulizi na Fasihi Andishi. Fasihi Simulizi ina mchango mkubwa sana katika Fasihi Andishi. Hivyo basi, Fasihi Simulizi inajumuisha kumbo za semi, nyimbo, majigambo, matambiko. Wakati, fasihi andishi inajumuisha kumbo kama vile tamthiliya, ushairi, na riwaya.

Kwa upande wa Fasihi Andishi hapo awali kumbo hizi za ushairi, tamthiliya na riwaya zilitawaliwa na ukanuni kutoka kwa urasimi mkongwe ambao ndio ulikuwa msingi mkuu katika uandishi. Hivyo, mtunzi yeyote yule alipaswa kufuata kanuni hizo za kiutunzi. Sheria hizo zilikuwepo sana katika kumbo ya ushairi na tamthiliya ndipo baadaye riwaya ilifuata. Miongoni mwa wafuasi wa ukanuni huo ni akina Shaaban Robert na Saadan Kandoro (Senkoro, 1987).

Khamis (2007) anafafanua umajaribio kuwa ni mwondoko wa utanzu fulani wa Fasihi kutoka sura iliyozoeleka kwendea sura mpya inayoanza kujishikashika. Kwa maana hiyo, umajaribio huu unajitokeza katika utanzu husika kwa kutumia mbinu ambazo awali zilikuwa hazitumiwi katika utanzi huo husika. Kila utanzu katika Fasihi hapo nyuma ulikuwa ukitawaliwa na kanuni zilizosimikwa na wanamapokeo kama vile Aristostle, Plato na Socrates ambazo kanuni hizo kila mtunzi ilimbidi kuzikuata katika utunzi wake. Baada ya kuja umajaribio ndipo kanuni hizo zilivunjwa na kupata muondoko au sura mpya katika utanzu husika kama ni ushairi, tamthiliya na riwaya.

Vile vile, Wamitila (2003) anaueleza umajaribio kuwa, ni ukiukaji wa kaida za utungaji na muundo wake. Kwa maana hiyo, umajaribio ni uvunjwaji wa kanuni ambazo zilikuwa zimezoeleka tangu awali ya kuwa ndizo msingi wa kufuatwa katika utunzi wowote ule na

msanii yoyote yule alipaswa kutunga kwa kufuata kanuni hizo. Mara baada ya umajaribio kuja ndipo kanuni hizo zilipovunjwa na kupata kitu kipya katika Fasihi ya Kiswahili. Msanii anayetunga kazi ya kihalisia anapaswa kutunga kwa utunzi wa kimuwakati na wakati huu umajaribio ndio umeshamiri kwa wingi katika kuelezea hali halisi ya ulimwengu jinsi ulivyo bila ya kupindisha ukweli wowote. Kipindi hiki ndipo zinapatikana riwaya za kimajaribio kama vile *Nagona* na *Mzingile*, *Babu Alipofufuka* na *Bina- Adam*. Kwa mfano, katika riwaya ya *Nagona* umajaribio unapatikana kupitia utumizi wa mbinu ya uhalisiamazingaombwe. Mwandishi anasema:

> …Kichomi kilianza kuniuma ubavuni. Nilipiga magoti chini. Kwa maumivu nilianza kutembelea magoti. Nilisikia vicheko vya watu. Nilijaribu kuongeza mwendo. Nilisikia vicheko kutoka karibu katika kila mti… Hakuna maji hapa. Maasi ya karne nne yamegeuza maji ya nchi hii kuwa damu tupu… Nilipofika karibu ya mto nilishangaa. Mto ulikuwa umejaa damu tupu ambayo ilikuwa ikitiririka kwa nguvu (uk. 1, 6, 11).

4.4.4 Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia

Maendeleo haya kwa kiasi kikubwa yamechangiwa na utandawazi. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004) inaeleza kuwa utandawazi ni mfumo wa mahusiano ya kimataifa katika nyanja mbalimbali kama vile biashara, uchumi au siasa uliowezeshwa na maendeleo ya teknolojia ya habari yanayofanya mataifa kuwasiliana kwa urahisi. Baada ya fasihi kukumbwa na majilio ya sayansi na teknolojia kwa kiasi kikubwa, Fasihi hiyo imebadilika ikilinganishwa na ilivyokuwa hapo awali kipindi cha kabla ya majilio hayo. Hapo awali kabla ya maendeleo ya sayansi na teknolojia hata kiwango cha utunzi kilikuwa cha hali ya chini sana ikilinganishwa na sasa baada ya mjilio hayo ya sayansi na teknolojia. Baada ya jamii kuhama na kuhamia katika mfumo wa sayansi na teknolojia ndipo kipindi hiki nyenzo za KITEHAMA zilipogundulika na kusababisha jamii kuhamia katika mfumo wa habari na mawasiliano. Baada ya ugunduzi ndipo utumizi wa kompyuta uliposhamiri kwa kiasi kikubwa hadi kufikia matumizi ya Fasihi ya Kiswahili kukua kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na awali (Ponera, 2014).

Kutokana na maendeleo haya vifaa kama vile simu, redio, runinga na mitandao ya kijamii imeshamiri kwa wingi kitu ambacho husababisha taarifa kusambaa kwa haraka zaidi na kuwafikia watu wengi kwa wingi zaidi na kwa muda mfupi. Kwa kiasi kikubwa majilio haya ya sayansi na teknolojia yamechangia sana katika kubadilisha hali ya uandishi katika Fasihi ya Kiswahili. Kupitia hili Said A. Mohamed anathibitisha kwa kusema kuwa:

> Utandawazi umechangia kwa kiasi kikubwa kubadilisha vionjo vya kiuandishi kutokana na muingilianao wa tamaduni tofauti tofauti katika dunia hii. Dunia imekamatana katika Fasihi kutokana na suala la utandawazi unaochangiwa na sayansi na teknolojia[12]

4.4.5 Kuibuka kwa Majanga na Magonjwa

Jamii imeshuhudia kuibuka kwa majanga kama vile matetemeko, njaa, ajali na magonjwa mbalimbali kama UKIMWI, ebola na virusi vya zika. Kuibuka kwa mabaa haya kumechangia kwa kiasi kikubwa kubadilisha hali ya uandishi katika Fasihi ya Kiswahili. Watunzi walio wengi wamefuata mlengo huu wa kujadili magonjwa hatari kama UKIMWI kwani hauna kinga wala tiba pindi mtu anapoupata. Lengo na nia ikiwa ni kuelimisha jamii kuhusiana na hali hii wakitoa njia za kujikinga na jinsi ya kuzuia maambukizi mapya na majanga hayo ya njaa na matetemeko. Mtunzi anayetungwa kwa uhalisia inambidi kuangalia jamii yake kihalisia na kuyajadili matukio jinsi yanavyotokea katika jamii yake na kwa wakati huo bila ya kupindisha ukweli halisi wa maisha jinsi yalivyo. Kwa mfano katika riwaya ya *Kisiki Kikavu* mwandishi anaeleza kuhusu janga la UKIMWI kupitia mhusika Kalabweli. Mwandishi anasema:

> …Mpenzi wangu nimekupa zawadi nyingi leo. Ninakuaga. Sijui kama tutaonana tena. Sitaki kukusahau tulivyokaa vizuri mara kwa mara, na ndiyo maana nimekumbuka kukupa mwaliko wa kuja huko niendako mimi. Fedha za ile hundi ni zawadi ya jeneza lako. Maiti yako isije ikakosa kuwekwa katika jeneza zuri hapo utakapokufa hivi karibuni, maana mimi mpenzi wako ninakufa kwa UKIMWI. Na ninajua na wewe, kama wale wenzako watano, unao ugonjwa. Usiogope. Usilie. Bado kidogo tutaonana tena, wapi sijui. Tutatambuana? Nadhani. Buriani.
>
> Wako anayekufa, Kalabweli.

[12] Mazungumzo binafsi kati ya mtafiti na Prof. Said A. Mohamed yaliyofanyika tarehe 5/1/2016 mjini Zanzibar.

Kupitia nukuu hii, Shima Getruda anaidhihirishia jamii kiasi gani waandishi wamebadilika katika utunzi wao. Ugonjwa wa UKIMWI umewashughulisha waandishi wengi huku wakionesha chanzo cha ugonjwa na madhara ya ugonjwa huu. Anatubainishia kwa kusema kuwa:

> Waandishi wa sasa hivi wanaangalia suala linalosumbua jamii. Gonjwa kama la UKIMWI limewashughulisha waandishi wengi kwa sababu ni ugonjwa hatari usio na tiba. Ndiyo maana waandishi wengi wanajishughulisha kuandika kuhusu suala hili[13]

Kwa maelezo haya, inaonesha ni namna gani watunzi wanavyobadilika kulingana na wakati huku wakizingatia mambo mazito yanayoikumba jamii. Matatizo hayo ndiyo yanayowashughulisha kwa lengo la kutoa funzo katika jamii iliyokusudiwa kupata ujumbe huo.

4.5 Muhtasari wa Sura ya Nne

Katika sura hii malengo ya utafiti pamoja na maswali ya utafiti yamefafanuliwa na kujibiwa kikamilifu. Yaani, Kubainisha mikondo mbalimbali ya kiuandishi inayojitokeza katika riwaya ya Kiswahili, kulinganisha na kulinganua vionjo vya kiuandishi katika riwaya za Shaaban Robert na Said A. Mohamed na kuchunguza sababu za kuwapo kwa mabadiliko ya kiuandishi katika riwaya za Kiswahili. Sababu kubwa ya waandishi hawa kutofautiana katika utunzi ni kutokana na hali halisi ya maisha jinsi yalivyo. Maisha sio kitu kinyoofu, hivyo, maisha yakibadilika na watunzi nao hubadili hali za utunzi wao kulingana na maisha yanavyokwenda. Na ikumbukwe kuwa msanii anatakiwa kuiakisi jamii yake kwa kusana matukio kama jinsi yalivyo katika ulimwengu halisi. Kwa kufanya hivi, mtafiti amefikia malengo yake kwa kuchambua na kupitia malengo yake na maswali ya utafiti huu.

[13] Mazungumzo binafsi kati ya mtafiti na Shima Getruda yaliyofanyika tarehe 10/2/2016 Chuo Kikuu cha Dodoma mjini Dodoma.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii imegawika katika sehemu tano. Sehemu ya kwanza inaeleza muhtasari wa tasnifu. Sehemu ya pili imechambua utoshelevu wa nadharia iliyotumika katika uchambuzi wa data. Sehemu ya tatu inafafanua mchango wa utafiti huu katika jamii. Sehemu ya nne inatoa maoni mbalimbali kuhusiana na utafiti huu. Sehemu ya tano inataja mapendekezo kwa tafiti zijazo.

5.2 Muhtasari wa Utafiti

Tasnifu hii imechunguza juu ya mabadiliko ya vionjo vya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili ulinganisho kati ya Shaaban Robert na Said A. Mohamed. Mtafiti ametumia riwaya mbili teule kwa kila mwandishi ambazo ni *Adili na Nduguze* na *Utu Bora Mkulima* za Shaaban Robert kwa upande wa Said A. Mohamed ni *Babu Alipofufuka* na *Utengano.*

Sura ya kwanza imezungumzia kuhusu utangulizi wa tasnifu hii ambapo istilahi mbalimbali zilizotumika katika utafiti huu zimefafanuliwa. Vipengele vingine ni usuli wa tatizo, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, historia za waandishi teule na muhtasari wa sura hiyo.

Sura ya pili imezungumzia mapitio ya maandiko ambayo yamegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni, sehemu ya kwanza, inahusu mapitio ya maandiko juu utunzi wa kazi za Fasihi kwa ujumla. Sehemu ya pili inahusu mapitio ya maandiko mbalimbali yanayohusu utunzi wa kazi za kifasihi. Mapitio yaliyopitiwa ni pamoja na majarida mbalimbali, tovuti, vitabu, na tasnifu za watafiti mbalimbali. Maandiko hayo yamegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni maandiko yanayohusu utunzi wa kazi za fasihi kwa ujumla, maandiko

yanayohusu maendeleo ya riwaya kwa ujumla na maandiko kuhusu waandishi hawa teule waliochaguliwa na mtafiti katika utafiti huu. Katika kupitia maandiko haya mtafiti amepitia maandiko yaliyoko maktabani kuhusiana na mada husika na kuchambua yale yanayomuhusu na kuyatumia kama mapitio yake. Maandiko haya tuliyoyapitia ndiyo yaliyopaswa kuziba mapengo ya utafiti ambayo ni wataalamu hawa hawajatoa kipaumbele katika kuchunguza sifa bainifu za zama mbalimbali za kiuandishi zinazojitokeza katika riwaya ya Kiswahili. Pili, hawajachunguza sababu za kuwapo kwa mabadiliko ya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili kama ilizungumziwa basi walizungumzia juu juu tu. Utafiti uliofanyika unakusudia kuziba mapengo kwa kuchunguza mikondo mbalimbali ya kiuandishi inayojitokeza katika riwaya ya Kiswahili kwa kuwalinganisha Shaaban Robert na Said A. Mohamed katika riwaya zao teule ambazo ni *Adili na Nduguze*, *Utu Bora Mkulima*, *Babu Alipofufuka* na *Utengano*. Pia, kuchunguza sababu za kuwapo kwa mabadiliko ya kiuandishi katika riwaya za Kiswahili.

Sura ya tatu imezungumzia mbinu na mpango mzima wa utafiti huu jinsi ulivyofanyika. Sura hii imechambua na kujadili kwa kina mpango wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, mbinu za ukusanyaji data kama vile za uwandani na maktabani, zana za utafiti, mawanda ya utafiti, uthabiti na uhalali wa utafiti, maadili ya utafiti pamoja na changamoto katika utafiti huu.

Sura ya nne imewasilisha matokeo ya utafiti kama jinsi yalivyopangwa na mtafiti katika utafiti huu kwa kuzingatia maswali ya utafiti huu kwa kuanza na mikondo ya kiuandishi inayojitokeza katika riwaya ya Kiswahili ikifuatiwa na kufanana na kutofautiana kwa waandishi hawa haalafu sababu za mabadiliko ya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili na. Sura ya tano imezungumzia muhtasari, hitimisho pamoja na mapendekezo kwa tafiti zijazo kwa wanazuoni wanaotaka kufanya ufafiti katika uga wa fasihi hasa ya Kiswahili upande wa riwaya.

5.3 Hitimisho

Katika utafiti huu mtafiti amegundua kuwa kuna mabadiliko makubwa sana ya kiutunzi yaliyojitokeza katika riwaya ya Kiswahili. Mabadiliko hayo yamechangiwa sana na hitoria za jamii, ongezeko la wasomi, umajaribio na kuibuka kwa magonjwa. Pi, utafiti huu umegundua kuna kiasi kikubwa cha kufanana na kutofautina kiutunzi kati ya Shaaban Robert na Said A. Mohamed katika kiwango cha kimaudhui na kifani. Utunzi wa zama za awali una mchago mkubwa katika utunzi wa sasa kwa kuwa waandishi hawa hupata chachu kutoka kwa waandishi wa nyuma. Suala la msingi katika utunzi haijalishi mtunzi atafuata zama za nyuma au sasa kinachotakiwa ni kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa.

5.3.1 Utoshelevu wa Nadharia Iliyotumika katika Utafiti

Nadharia iliyotumika katika utafiti huu ni uhalisia. Nadharia hii imejikita katika utunzi wa ushabihi ukweli na utunzi wa kimuwakati huku ikimtaka mtunzi kusawiri mambo kama yalivyo katika jamii yake husika. Nadharia hii imesaidia kwa kiasi kikubwa katika kukamilisha tasnifu hii kwa sababu ilitusaidia katika kubainisha mikondo mbalimbali ya kiuandishi inayojitokeza katika riwaya ya Kiswahili huku ikitusaidia kulinganisha na kulinganua vionjo vya kiuandishi kwa watunzi wawili waliochaguliwa. Kwa maana hiyo, mtunzi wa kazi za kifasihi hutakiwa kusawiri ukweli katika maisha yao halisi hivyo kufanya nadharia ikidhi malengo ya utafiti huu.

5.3.2 Mchango wa Mpya wa Tasnifu Hii

Kwa kiasi kikubwa, utafiti huu umetoa dira kwa wanazuoni wa uga wa Kiswahili, hasa upande wa fasihi kwa kuonesha ni jinsi gani riwaya ya Kiswahili imepiga hatua katika utunzi wake. Kwa kufanya hivi, mtafiti amejadili jinsi gani utunzi wa riwaya ya Kiswahili ya karne ya akina Aristostle na Plato ulivyokuwa unafungwa na mikatale ya kikanuni ukitofautisha na utunzi wa karne ya sasa. Watunzi wa zama hizi kwa kiasi kikubwa

wanachangiwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia pamoja na ongezeko la wasomi na wanazuoni wanaojadili mambo kwa utandawazi zaidi na hata kuvuka mipaka ya kitaifa na mataifa na kiuhalisia zaidi. Pia, utafiti huu kwa kiasi kikubwa utatumika kama rejeleo kwa ajili ya wanazuoni wanaotaka kuzamia kuhusu riwaya ya Kiswahili kwa lengo la kuiendeleza Fasihi ya Kiswahili.

5.4 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo

Mtafiti alilenga kuchunguza juu ya mabadiliko ya vionjo vya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili akiwalinganisha Shaaban Robert na Said A. Mohamed kwa kupitia riwaya zao teule alizozichagua. Kwa hivyo, kupitia utafiti huu mtafiti amegundua ya kuwa bado yapo maeneo mengi ya kuchunguza kwa lengo la kuweka hazina kubwa katika fasihi ya Kiswahili lengo likiwa ni kuiendeleza na kuikuza hadi kuvuka mipaka ya kitaifa na kimataifa.

Tasnifu hii inapendekeza ya kuwa ipo bado haja ya kufanya utafiti zaidi katika riwaya za Shaaban Robert na Said A. Mohamed kwa lengo la kuwaenzi waandishi hawa kwa mchango wao mkubwa walioufanya katika Fasihi ya Kiswahili. Hii itasaidia kufahamika na kujulikana kwa wanazuoni na wataalamu wa Kiswahili walio wengi ndani na nje ya nchi. Kwa maana hiyo, atakayefanya utafiti juu ya waandishi hawa anaweza kuangalia kazi zao za kishairi au hata tamthiliya ambazo atachunguza juu ya mabadiliko ya vionjo vya kiuandishi katika ushairi au tamthiliya ya Kiswahili. Katika utafiti huo atawalinganisha watunzi hawa nguli katika Fasihi ya Kiswahili au hata akaamua kuchagua waandishi wengine kama vile Muhamed Said Abdullah, Ben Mtobwa, Faraji Katalambula na wengi wengi wanaovuma katika uandishi wa riwaya ya Kiswahili.

Pia, tafiti nyingine zijazo zinaweza kuchunguza juu ya mabadiliko ya vionjo vya kiuandishi kwa kuwalinganisha waandishi hawa kwa kutumia kazi zao nyingine za riwaya na kuja na majibu tofauti na haya ambayo ametupatia mtafiti huyu. Maana alichunguza juu

ya mabadiliko ya vionjo vya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili akiwalinganisha Shaaban Robert na Said A. Mohamedi kwa kutumia riwaya zao teule za *Adili na Nduguze*, *Utu Bora Mkulima*, *Babu Alipofufuka* na *Utengano*.

MAREJELEO

Bertoncini, E. (1989), *Outline of Swahili Literature* (*Prose, Finction and Drama*), E. J. Brill, Leiden.

Chuachua, R. (2010), "Suala la Itikadi katika Nathari za Shaaban Robert", Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Daudi, H. A. (2013), "Nafasi ya Kejeli na Dhihaka Katika Tamthiliya Teule za Said Ahmed Mohamed", Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Faustine, S. (2012), Matumizi ya Mtindo wa Uhalisiamazingaombwe Katika Riwaya Teule za E. Kezilahabi: Dhima na Athari Zake kwa Hadhira, Tasnifu kwa Ajili ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Finnbogason, J. (2007), *The Introduction to Literature*: Canada, The Nelson Thomas Learning.

Gibbe, A. G. (1978), *Shaaban Robert: Mshairi*, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar es Salaam.

Gromov, M. D. (2002), *Post Modernistic Elements in Recent Kiswahili Novels*, Nairobi, (Haijachapishwa).

Haji, A. (2015), Matumizi ya Utanzia Katika Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed, Tasnifu kwa Ajili ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Hussein, E. (1971), *Mashetani*, Oxford University Press, Nairobi.

…… (1976), *Jogoo Kijijini na Ngao za Jadi*, nairobi: Oxford University Press.

Kezilahabi, E. (1975), *Gamba la Nyoka*, Eastern Africa Publication, Arusha.

.....(1990), *Nagona*, Dar es Salaam Universty Press, Dar es Salaam.

..... (1991), *Mzingile*, Dar es Salaam Universty Press, Dar es Salaam.

…….. (1975), *Rosa Mistika*, Dar es Salaam University Press, Dar es Salaam.

Hug, H. (1986), *A handbook to Literature*, Mcmillan Publishing Company, New York.

Khatib, M. (2011), "Chanjo za Matakwa ya Mwanaume katika Mwili wa Mwanamke Ulinganisho wa Ushairi wa Muyaka bin Haji na Shaaban Robert", Tasnifu ya Uzamivu Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Khamis, S. (1980), *Utengano*, Longhorn Publisher, Nairobi.

.....(2007), “Vionjo vya Riwaya Mpya ya Kiswahili” katika *Kioo cha Lugha* no. 5, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu Dar es Salaam.

.....(2001), *Babu Alipofufuka*, Jomo Kenyata Foundation, Nairobi.

.....(2005), *Sign of New Features in Kiswahili Novel*, Research in African Literature 36/1:92-108.

.....(2007), Utandawazi au Utandawizi? Jinsi Lugha ya Riwaya Mpya ya Kiswahili Inavyodai, Katika *Mulika* Juzuu ya 70, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kothari, C. (2002), *Research Methodology*: *Methods and Techniques.* 2nd Ed. Delhi India: New Age International Ltd Publisher.

Ligopola, S. M. (2012), “Nafasi ya Mwanamke Katika Nathari Teule za Said Ahmed Mohamed: Je, ni Kumkweza au Kumbeza?”, Tasinifu ya Shahada ya Uzamili Chuo Kikuu cha Dodoma, (haijachapishwa).

Liwenga, G. (1981), *Nyota ya Huzuni*, Tanzania Publishing House, Dar-es-Salaam.

Makulla, S. A. (2012), “Athari za Uhalisia Mazingaombwe kwa Msomaji katika Kuzielewa Kazi za Fasihi za Said Ahmed Mohamedi”, Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Masingele, L. (2012), “Mabadiliko ya Riwaya ya Kiswahili Kidhamira kuanzia mwaka 1970-2011”, Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Dodoma , (Haijachapishwa).

Mkubwa, A. (2012), Ujitokezaji wa Visasili na Visawe Katika Riwaya ya Kiswahili ya Kimajaribio, Tasnifu kwa ajili ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, (Haijachapishwa).

Muhando, P. (1982), *Lina Ubani,* Dar es Salaam, Dar es Salaam University Press.

Mulokozi, M. (1996), *Fasihi ya Kiswahili*, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam, TUKI.

Mutembei, A. (2005), *Kisiki Kikavu*, Sona Printers Ltd, Dar-es- Salaam.

Mnyampala, M. (1970), *Ngonjera za Ukuta*, Kitabu cha Kwanza, Oxford University Press,Dar-es-Salaam.

Mung’ong’o, C. G. (1980), *Njozi Iliyopotea*, Tanzania Publishing House, Dar-es-Salaam.

Momanyi, C. (2001), Nafasi ya Mwanamke katika Ushairi wa Shaaban Robert, katika *Mulika* Juzuu ya 64, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Njogu, K na Wafula, M. R. (2007), *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Njogu, K na Chimera, R. (1999), *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu,* Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Oriedo, H. (2000), Fani Katika Riwaya za Shaaban Robert: *Kusadikika, Utubora Mkulima na Siku ya Watenzi Wote*, Tasnifu kwa Ajili ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, (Haijachapishwa).

Ohly, R. (1981), *Aggressive Prose,* TUKI, Dar es Salaam.

Ponera, A.S. (2010), "Ufutuhi katika Nathari za Shaaban Robert: Maana Yake, Sababu za Kutumiwa na Athari Zake kwa Wasomaji", Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

.....(2014), "Ufutuhi katika Nathari ya Kiswahili ulinganisho wa Nathari za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi", Tasnifu ya Uzamivu Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

.....(2014), *Utangulizi wa Ndharia ya Fasihi Linganishi*, Dar es Salaam, Karljamer Print Technology.

Robert, S. (1951), *Adili na Nduguze,* Nelson, Nairobi.

…….. (1954), *Utubora Mkulima,* Evans Brothers Ltd, Nairobi.

…….. (1991), *Kusadikika,* Mkuki na Nyota Publisher, Dar es Salaam.

…….. (1991), *Kufikirika,* Mkuki na Nyota Publisher, Dar es Salaam.

…….. (1949), *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*, Nelson, Nairobi

…….. (1968), *Siku ya Watenzi Wote,* Nelson, Nairobi.

Samweli, M, Selemani, A. & Kabiero, A. (2013), *Ushairi wa Kiswahili*, MEVELE Publisher, Dar es Salaam.

Seleman, O. (2012), Riwaya Mpya ya Kiswahili na Masuluhisho ya Changamoto za Utandawazi, Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, (Haijachapishwa).

Senkoro, F.E.M.K. (2006), Fasihi ya Kiswahili ya Majaribio: Makutano ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi katika *Kioo cha Lugha*, Juzuu ya 4, TUKI, Dar es Salaam.

……(1993), Fasihi, Uandishi na uchapishaji: *Makala ya Semina ya Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania,* Dar es Salaam University Press.

.....(2011), *Fasihi*, Dar es Salaam University Press, Dar es Salaam.

..... (1987), *Fasihi na Jamii,* Press and Publicity Centre, Dar es Salaam.

Taib, A. (2009), Maisha ya Shaaban Robert na Falsafa Yake Katika Maandishi Yake, katika *Mulika* Juzuu ya 28, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

TUKI (2004), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu Toleo la Pili*, Oxford University Press, Kenya.

Wamitila, K. (2003), *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia,* Nairobi Focus Publisher Ltd.


…….. (2002), *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake,* Phoenix Publishers Ltd Nairobi Kenya.

…….. (2002), *Bin- Adam,* Phonex Publisher, Nairobi.

Wanjiru, M. (2013), "Uhalisiajabu katika riwaya mpya: Babu Alipofuka (SAID AHMED MOHAMED) na Watu wa GEHHENA (TOM OLALI)", Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi, (Haijachapishwa).

VIAMBATISHO

Barua Mbalimbali za Kuruhusiwa Kufanya Utafiti



THE UNIVERSITY OF DODOMA
DEPUTY VICE CHANCELLOR ACADEMIC, RESEARCH & CONSULTANCY
OFFICE OF GRADUATE STUDIES

P.O. BOX 263
DODOMA, TANZANIA
TEL: +255 23 23002 FAX: +255 23 23000 EMAIL: ahmed_ame@yahoo.com

REF/UDOM/GS-ADMS/2015/0494 Monday, 30 November 2015

To Whom It May Concern:

RE: INTRODUCING MS.JUMANNE ARAFA

The above named student is enrolled at the University of Dodoma for the degree of Master of Arts in Kiswahili Literature with registration number HD/UDOM/393/T.2014

An essential requirement of the study programme is that each candidate is required to submit a dissertation report on a project undertaken within industry and supervised by a member of the University's academic staff. Where possible this project should relate to a practical situation in an organisation or firm selected by the candidate. Students are expected to use their own initiative to identify a possible project and negotiate access with a local firm or organization. The title of study is **"MABADILIKO YA VIONJO VYA KIUANDISHI KATIKA RIWAYA ZA KISWAHILI: ULINGANISHO WA RIWAYA ZA SHAABAN ROBERT NA SAID A. MOHAMED".**

The work may take the form of a survey, ethnography, case studies, etc. Where the report may contain confidential information and its publication could be harmful to the organization, confidentiality is assured by the University. Such reports will be seen only by the Supervisor and Examiner for examination purposes.

I would be grateful if you would provide the student with this opportunity to further her studies while at the same time gaining some useful input for your own organization through the results of the project report.

Sincerely,

Prof. Ahmed M. Ame
Director for Graduate Studies

B. Miongozo ya Hojaji

B.1 Mwongozo wa Mahojiano kwa Wataalamu na Wanafunzi wa Fasihi

Maelezo

Naitwa Arafa Jumanne, natokea Chuo Kikuu cha Dodoma. Ninasoma Shahada ya Umahiri katika Fasihi. Nafanya utafiti kuhusu mabadiliko ya vionjo vya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili. Malengo ya utafiti huu ni kuchunguza mabadiliko ya kiuandishi yajitokezavyo katika vipindi mbalimbali. Pia, kuchunguza sababu za kuwapo kwa mabadiliko ya kiuandishi katika riwaya za Kiswahili. Ni matumaini yangu nitapata ushirikiano wa hali yajuu katika kukamilisha utafiti huu.

Maswali:

1) Unaelewa nini kuhusu dhana ya vionjo vya kiuandishi?

2) Katika utafiti huu, neno vionjo linachukuliwa kama upya katika riwaya ya Kiswahili. Una maoni gani au mtazamo gani kuhusu dhana hii?

3) Je, kuna mabadiliko yoyote katika riwaya ya Kiswahili, kama yapo yataje na eleza kwa kiasi gani?

4) Je, ni sababu gani zinazofanya kuwapo kwa mabadiliko ya kiuandishi katika riwaya za Kiswahili?

5) Utunzi wa riwaya za Kiswahili za sasa unafananaje au kutofautianaje na ule wa miaka iliyopita?

6) Kwa maoni yako kuna kulandana kokote kwa namna ya kiuandishi kati ya Shaaban Robert na Said A. Mohamed?

7) Ni kazi zipi za Shaaban Robert au za Said A. Mohamed ambazo umewahi kuzisoma, kuzihakiki au kuzitafiti?

8) Baadhi ya wasomaji wa riwaya za waandishi hawa teule wanapata ugumu katika kuelewa maudhui ya kazi zao. Je? Una maoni gani kuhusu urahisi au ugumu wa kueleweka kwa riwaya za waandishi hawa?

9) Una maoni gani kuhusu faida au hasara za mabadiliko haya katika riwaya ya Kiswahili?

10) Unaweza kuwaelezeaje Shaaban Robert na Said A. Mohamed katika maisha yao? Je unadhani kuna kulandana kokote kati ya maisha yao halisi na fani na maudhui yanayojitokeza katika riwaya zao?

Asante.

B.2 Mahojiano Kwa Wananchi wa Tanga na Zanzibar

Naitwa Arafa Jumanne, natokea Chuo Kikuu cha Dodoma. Ninasoma Shahada ya Umahiri katika Fasihi. Nafanya utafiti kuhusu mabadiliko ya vionjo vya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili. Malengo ya utafiti huu ni kuchunguza mabadiliko ya kiuandishi yajitokezavyo katika vipindi mbalimbali. Pia, kuchunguza sababu za kuwapo kwa mabadiliko ya kiuandishi katika riwaya za Kiswahili. Ni matumaini yangu nitapata ushirikiano wa hali ya juu katika kukamilisha utafiti huu.

1) Tunaomba utueleze kwa ufupi kuhusu jina lako, umri wako na kiwango chako cha elimu?

2) Je, unamjua Shaaban Robert/Said A. Mohamed? kama ndivyo, eleza ulivyopata kumjua.

3) Umewahi kusoma kitabu chochote cha Shaaba Robert/Said A. Mohamed? Ni kipi/vipi?

4) Je, unaweza kuelezeaje kuhusu kuwapo au kutokuwapo kwa uhusiano baina ya mambo yaliyopo katika vitabu vya Shaaban Robert/ Said A. Mohamed na mambo yaliyoko au yaliyowahi kutendeka hapa katika jamii yenu?

5) Je, unaweza kuelezeaje kuhusu kuwapo au kutokuwapo kwa uhusiano baina ya tabia ya Shaaban Robert/Said A. Mohamed na utamaduni wa jamii yenu?

Asante kwa ushirikiano wako.